# ATHARI ZA UHAWILISHAJI WA VITAMKWA VYA KIKISA KATIKA MAANA ZIJITOKEZAZO KATIKA KISWAHILI SANIFU

**NA**

**MAKANJI NICHOLUS NANDI**

**C50/8565/2017**

**TASNIFU HII IMEWASILISHWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**2019**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kingine chochote.

____________________________ ____________________________

**Makanji Nicholus Nandi** **Tarehe**

**C50/8565/2017**

**Mtahiniwa**

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

**Dkt. Ayub Mukhwana** **Tarehe**

**Msimamizi**

**Prof. Iribe Mwangi** **Tarehe**

**Msimamizi**

## TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa wazazi wangu

**Clementina Ayuma Shikokoti**

na

**Alphonce Makanji Nandi.**

Mwanenu kasoma kwa niaba yenu!

Ahsanteni sana kwa kunivumilia kwa mengi.

Mwenyezi Mungu awape maisha marefu ili siku moja

Mpate kuyaona na kuyafurahia matunda ya masomo haya.

## SHUKRANI

Apewe sifa zisizokoma Mwenyezi Mungu kwa kunifikisha umbali huu. Shukrani kwa afya njema na maarifa ya kuyafikisha masomo yangu hatua hii. Nashukuru Chuo Kikuu cha Nairobi kwa kufanikisha shahada hii. Fursa hii imekuwa zawadi kubwa katika maisha yangu ya kiakademia.

Nina upungufu wa kauli ya kueleza shukrani zangu kwa wasimamizi wangu Prof. Iribe Mwangi na Dkt. Ayub Mukhwana. Mmeonyesha utulivu mkubwa wakati wa kunirekebisha katika mchakato wa kuandaa kazi hii. Nawashukuru sana kwa kuhakikisha naitendea haki kazi hii ya utafiti. Ahsante Dkt Ayub Mukhwana kwa uvumilivu, ushauri na maelekezo yako! Sijui tofauti kamili iliyopo baina ya usimamizi wako, urafiki na kuwa baba mwenye hekima! Ahsante sana!

Shukrani za dhati kwa wahadhiri wangu Prof. John Habwe, Prof. Mwenda Mbatiah, Prof. K.W.Wamitila, Prof. Kineene Wamutiso, Prof. Evans Mbuthia, Prof. Tom Olali, Dkt. Zaja Omboga, Dkt. Jefwa Mweri, Dkt. Basilio Mungania, Dkt. Prisca Jerono, Dkt. Hannah Mwaliwa, Dkt. Amiri Swaleh na Ms Mary Ndung'u. Uhodari na ushupavu wa kila mmoja wenu katika unoaji ndio ulionitunuku makali yalonisukuma hadi upeo huu. Ama kwa kweli ikiwa ningeruhusiwa kuandika kuwahusu, maelezo ya alama za kiakademia mlizoniachia zingetosha tasnifu nzima!

Shukrani za kipekee kwa Prof. Rayya Timammy. Ahsante sana kwa kunishika mkono tangu shahada ya kwanza na kuniongoza hadi kilele cha shahada hii. Umekuwa mlezi na mshauri mwema kwangu. Kauli zako za kila mara zimenisukuma kutia bidii. Akuzidishie Baraka Mungu!

Ahsante sana mwenyekiti wa Idara ya Kiswahili Prof. Iribe Mwangi. Ahsante sana kwa kunipa nafasi kuwa mwanafunzi katika idara hii. Ahsante kuwa tayari kusumbuliwa na barua za ufadhili kila mara. Una moyo mkubwa wa ukarimu. Umeing'aisha nyota yangu na kuniweka kwenye ramani ya dunia. Akukirimu Mwenyezi Mungu afya nzuri na neema zake kadri ya utashi wake.

Shukrani za kipekee kwa Chuo Kikuu cha Humboldt Berlin kwa kunifadhili kupata tajiriba zaidi Ujerumani. Ahsante sana kwa walimu wangu Prof. Tom Gueldemann, Dkt Christfried Naumann, Dkt. Lutz Diegner na Mzee Vitale Kazimoto kwa ukarimu wenu wa maarifa. Mlinifaa pakubwa!

Nawashukuru wazazi wangu, ndugu na marafiki walionifaa katika safari hii. Ahsanteni sana Margaret Danford na Brighton Makanji. Mmekuwa nguzo muhimu. Walionihisani kwa kweli ni wengi, hivi basi naomba mpokee shukrani zangu popote mlipo. Mungu awakirimu neema zake!

## IKISIRI

Kazi hii ilihusu uhawilishaji wa fonimu za Kikisa katika lugha ya Kiswahili Sanifu. Kazi hii ilihusisha ubainishaji wa makosa katika insha za wanafunzi na tathmini ya athari za makosa hayo katika uelewekaji wa maana katika Kiswahili Sanifu. Utafiti huu ulitumia lugha ya Kikisa kama lugha ya kwanza na lugha ya Kiswahili Sanifu kama lugha ya pili. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Uchanganuzi Makosa na Lugha Kati kubainisha athari za Kikisa zijitokezazo katika Kiswahili Sanifu wakati wazungumzaji asilia wa Kikisa wanapotumia Kiswahili Sanifu. Mbinu za usomaji matini, utumiaji wa hojaji, uchunguzi shiriki na mahojiano zilitumika katika ukusanyaji data huku mbinu za uchanganuzi wa data zikitumika kwa kuongozwa na nadharia ya Uchanganuzi Makosa na Lugha Kati. Kazi hii ilitathmini athari za uhawilishaji wa fonimu za Kikisa katika Kiswahili kwa maana ya usemi na maandishi ya mzungumzaji na mwandishi aliye mzungumzaji asilia wa Kikisa. Athari za uhawilishaji huu wa fonimu kwa maana zilichunguzwa katika kazi hii ili kutathmini uwezo wa uhawilishaji fonimu kimakosa katika kufanikisha au kutofanikisha mawasiliano baina ya mzungumzaji mahiri wa Kiswahili Sanifu na mzungumzaji wa Kiswahili aliye mzungumzaji asilia wa Kikisa. Hili limefikiwa kupitia kubainisha tofauti za maana zinazojitokeza fonimu inapobadilishwa kutokana na uhawilishaji mbaya wa fonimu za Kikisa katika Kiswahili Sanifu. Malengo ya utafiti huu yalikuwa kuonyesha tofauti za kifonimu baina ya Kikisa na Kiswahili na kutathmini athari za tofauti hizi kwa matamshi na maana zijitokezazo katika Kiswahili Sanifu. Matokeo ya utafiti huu yalibainisha hali tatu za uelewekaji wa makosa ambao ulikuwa na athari tofauti kwa mawasiliano baina ya mzungumzaji wa Kiswahili aliye mzungumzaji asilia wa Kikisa na msikilizaji mahiri wa Kiswahili Sanifu. Kazi hii ilibainisha makosa yanayosababisha athari zisizoathiri maana, zinazobadili maana na zinazopoteza maana husika kabisa. Athari zinazobadili maana na zinazopoteza maana zilitokea kuwa na athari kubwa kwa mawasiliano.

**Yaliyomo**

**UNGAMO** .......... i
**TABARUKU** .......... ii
**SHUKRANI** .......... iii
**IKISIRI** .......... iv
**Yaliyomo** .......... v
**Sura ya 1** .......... 1
1.1 Utangulizi .......... 1
1.2 Tatizo la Utafiti .......... 5
1.3 Maswali ya Utafiti .......... 5
1.4 Madhumuni ya Utafiti .......... 6
1.5 Sababu za Kuchagua Mada .......... 6
1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti .......... 8
1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada .......... 9
1.8 Misingi ya Nadharia .......... 13
1.8.1 Nadharia ya Uchanganuzi wa Makosa .......... 14
1.8.2 Nadharia ya Lugha Kati .......... 15
1.9 Mbinu za Utafiti .......... 20
1.9.1 Utafiti wa Nyanjani .......... 20
1.9.4 Mbinu za Uchanganuzi wa Data .......... 24
1.9.5 Uwasilishaji wa Data .......... 25
1.9.6 Uzingatiaji wa Maadili .......... 25
**Sura ya 2** .......... 27
2.1 Utangulizi .......... 27
2.2 Dhana ya Uchanganuzi Makosa .......... 27
2.3 Lahaja za Kiluhya .......... 31
2.3.1 Kikisa .......... 33
2.4 Kiswahili .......... 34
2.5 Uhawilishaji wa Fonimu .......... 35
2.6 Uhawilishaji wa Mfumo wa Lugha .......... 36
2.6.1 Uelewanaji .......... 37

2.7 Kuathiriwa kwa Lugha ........................................................................................................37
2.8 Uchanganuzi wa Makosa ........................................................................................................39
2.8.1 Umuhimu wa Makosa ........................................................................................................42
2.8.2 Tofauti Kati ya Makosa ya Kushtukia na ya Ujifundishaji wa Lugha ya Pili .............43
2.8.3 Aina za Makosa ........................................................................................................45
2.8.4 Kategoria za Makosa ........................................................................................................46
2.8.5 Uhawilishaji Chanya ........................................................................................................46
2.8.6 Uhawilishaji Hasi ........................................................................................................47
2.8.7 Dhana ya Uhamishaji na Kuathiri ........................................................................................................49
2.9 Masuala ya Kimsingi ........................................................................................................49
2.10 Hitimisho ........................................................................................................51
**Sura ya 3 ........................................................................................................52**
3.1 Utangulizi ........................................................................................................52
3.2 Tofauti baina ya fonimu za Kiswahili na Kikisa ........................................................................................................53
3.3 Ubadilishaji Fonimu ........................................................................................................53
3.3.1 Ubadala wa /p/ > /b/ ........................................................................................................53
3.3.2 Ubadala wa /v/ > /f/ ........................................................................................................54
3.3.3 Ubadala wa /ɟ/ > /ʧ/ ........................................................................................................54
3.3.4 Ubadala wa /g/ > /k/ ........................................................................................................55
3.3.5 Ubadala wa /s/ > /z/ ........................................................................................................56
3.3.6 Ubadala wa /d/ > /t/ ........................................................................................................57
3.3.7 Ubadala wa /ð/ > /θ/ ........................................................................................................58
3.4 Uchopekaji ........................................................................................................61
3.4.1 Uchopekaji wa /h/ ........................................................................................................61
3.4.2 Uchopekaji wa irabu /u/ ........................................................................................................61
3.4.3 Uchopekaji wa Nusu Irabu /y/ na /w/ ........................................................................................................61
3.4.4 Uchopekaji wa Irabu /i/ ........................................................................................................62
3.5 Udondoshaji ........................................................................................................63
3.5.1 Udondoshaji wa /h/ ........................................................................................................63
3.6 Uongezaji Fonimu ........................................................................................................63
3.7 Makosa Yatokanayo na Ngeli ........................................................................................................64

3.7.1 Idadi katika Kiswahili Sanifu na Kikisa ....................65
3.8 Sababu za Ufanyaji Makosa ....................66
3.8.1 Uhawilishaji Hasi ....................67
3.8.2 Ujumlishaji Mno ....................67
3.8.3 Umakinifu Kupindukia ....................68
3.8.4 Makosa Yasio na Msingi wa Kikisa ....................73
3.9 Makosa ya Kawaida ....................74
3.10 Makosa ya Kileksika ....................76
3.11 Hitimisho ....................76
**Sura ya 4 ....................78**
4.1 Utangulizi ....................78
4.2 Idadi na Asilimia za Makosa ....................79
4.3 Athari za Makosa kwa Mawasiliano ....................81
4.3.1 Athari za Makosa Zisizoathiri Mawasiliano ....................81
4.3.2 Athari za Makosa Zinazosababisha Kueleweka Vibaya ....................83
4.3.3 Athari za Makosa Zinazosababisha Kutokueleweka Kabisa ....................85
4.4 Makosa ya Kiathari na Makosa Yasiyotokana na Athari za Kikisa ....................85
4.5 Athari Chanya za Kikisa kwa Kiswahili ....................86
4.6 Asilimia ya Makosa ....................87
4.7 Athari za Mtagusano wa Kikisa na Kiswahili Sanifu ....................90
4.7.1 Kutofautisha kwa Hali ya Chini kwa Fonimu ....................90
4.7.2 Kutofautisha kwa Hali ya Juu kwa Fonimu ....................90
4.7.3 Ufafanuzi Tena ....................91
4.7.4 Ubadilishaji Fonimu ....................91
4.8 Hitimisho ....................92
**Sura ya 5 ....................93**
5.1 Utangulizi ....................93
5.2 Muhtasari na Mahitimisho ....................93
5.3 Mapendekezo ....................95
5.4 Marejeleo ....................97
**Viambatisho ....................102**

## Sura ya 1

## Athari za Uhawilishaji wa Vitamkwa vya Kikisa katika Maana Zijitokezazo katika Kiswahili Sanifu

### 1.1 Utangulizi

Kiswahili Sanifu ni lugha rasmi na ya taifa nchini Kenya. Sifa ya urasmi na utaifa inaipa lugha ya Kiswahili majukumu ya kitaifa ikiwemo kutumika katika mawasiliano mapana, elimu na taasisi za Serikali na zisizo za kiserikali. Kiswahili kinatumika kama lugha unganishi nchini Kenya na Afrika Mashariki. Matumizi ya Kiswahili husababisha mtagusano wa lugha ya Kiswahili na lugha nyingine. Lugha hizi zaweza kuwa katika kundi moja na Kiswahili kama vile lugha za Kibantu. Pia, lugha hizi zaweza kuwa nje ya kundi la lugha za Kibantu. Kivyovyote vile, mtagusano huu husababisha athari. Athari hizi zaweza kuwa hasi au chanya.

Kazi hii imechunguza athari zinazoletwa na mtagusano kati ya Kiswahili Sanifu na Kikisa. Kikisa ni lahaja mojawapo ya Kiluhya ambacho ni kundi la lugha anuwai zinazokaribiana. Utafiti huu utajikita katika Kikisa ambayo ni lahaja mojawapo ya Kiluhya. Lugha ya Kikisa imetumika kama lingua franka katika sehemu ya gatuzi la Kakamega na hivyo kuwa miongoni mwa lahaja za Kiluhya zinazozungumzwa na watu wengi zaidi. Uchunguzi wa athari za lahaja hii ya Kikisa utakuwa sehemu wakilishi ya kiasi kikubwa cha wazungumzaji wa Kikisa.

Mbaabu (1995) na King’ei & Musau (2000) wanaeleza kuwa, matatizo ya kimatamshi aghalabu ni tokeo la athari za lugha za kimsingi zinazotokana na umilisi wa matamshi ya lugha ya kwanza na mwishowe kusababisha makosa ya kifonolojia katika lugha ya pili. Athari za kimofolojia na kifonolojia zinabainika wazi katika kazi hii. Lengo kuu la kuzibainisha athari hizi ni kuziweka wazi ili kutathmini uwezo wa athari hizi kuvuruga mawasiliano kwa kukosa kueleweka au kueleweka visivyo. Athari hizi zinatatiza kwa kiasi kikubwa mawasiliano kutokana na maana aliyokusudia masemaji kutomfikia msikilizaji.

Utafiti huu unatumia nadharia ya Lugha Kati na Nadharia ya Uchanganuzi wa Makosa. Nadharia hizi mbili zimetumika kutambua na kuchanganua makosa yaliyopatikana katika data. Nadharia ya Lugha Kati imetumika kuonyesha uwezekano wa wanafunzi na wazungumzaji wa Kiswahili

Sanifu, kwa ujumla wake, kujaribu kurahisisha ujifunzaji wao wa Kiswahili Sanifu kwa kutumia baadhi ya mifumo waliyojifunza awali katika lugha ya kwanza na ambayo tayari wana umilisi nayo. Nadharia ya uchanganuzi wa makosa kwa upande mwingine, imeongoza utafiti huu kupitia hatua mbalimbali zilizopendekezwa na mwaasisi wake Corder (1974). Hatua alizopendekeza Corder zikiwemo; kukusanya sampuli ya data, kutambua makosa, kueleza makosa, kuhesabu makosa, kutambua vipengele vilivyo na matatizo na kufafanua sababu za ujitokezaji wa makosa hayo vimekuwa msingi wa utafiti huu. Hatua hizi zimewezesha ukusanyaji wa data hadi uchanganuzi wake.

Lugha ya Kiswahili inatumika katika takriban nyanja zote za maisha ya Wakenya katika mawasiliano yanayopita mipaka ya wazungumzaji wa lugha yao ya kwanza. Kwa mujibu wa Githiora (2008), lugha ya Kiswahili inatumiwa na asilimia 80 ya Wakenya kama lugha ya pili. Lugha hii ndiyo ya pili kufunzwa kwa watoto wanapoanza masomo yao baada ya kujifunza lugha ya mama ambayo huchukuwa nafasi ya lugha ya kwanza (Abdulaaziz & Osinde 1997).

Lugha nyingi zina athari kubwa katika matamshi ya maneno ya Kiswahili Sanifu (Mbaabu 1985). Lugha kama vile Kiluhya, Kikamba, Kikisii na Kikuyu huwaathiri wazungumzaji wake kwa kupatikana wakizibeba fonimu za lugha zao na kuzitumia katika Kiswahili Sanifu. Jambo hili huathiri mawasiliano na wakati mwingine kutoathiri kabisa. Athari za kuvunja au kutovunja mawasiliano huwa si za moja kwa moja.

Mwalimu aliye na athari za lugha ya kwanza anapoanza kufundisha wanafunzi hukosa kumuelewa lakini anapoendelea kwa muda wa kipindi fulani kama mwezi au hata mwaka, wanafunzi huanza kumuelewa hata anapotamka kwa athari za lugha yake ya kwanza. Hili linatokana na ufahamu wa fonimu anazozitamka visivyo na hivyo kujua jinsi ya kubadilisha wanaposikia fonimu husika zenye utata zikimtatiza mwalimu wao. Vivyo hivyo, mzungumzaji au anayetoa hotuba anapokuwa na athari, wengi hukosa kumuelewa kutokana na fonimu nyingine anazoongeza au kutoa katika lugha wanayoijua ambazo hawazitambui. Lakini kama hotuba hiyo itakuwa ndefu na waelewe mada, idadi kubwa itaanza kumwelewa kwa kuzingatia maswala mengine kama vile muktadha kwani watabaini fonimu anazohawilisha kwa nafasi ya fonimu sahihi kwa mujibu wa lugha husika. Hivyo basi, utafiti huu ulinuia kulirahisha hili kwa kubainisha na kuchanganua fonimu zinazowapa

matatizo wazungumzaji wa Kikisa katika usemi wao wa Kiswahili Sanifu na hivyo kwa yule atakayepata nafasi ya kupitia matokeo ya utafiti huu aweze kuelewa fonimu atakazotarajia zinaweza kubadilishwa na kujua fonimu zake sahihi na hivyo kuelewa haraka mzungumzaji hata anapokuwa na athari nyingi za Kikisa.

Lugha ya Oluluyia ni mojawapo ya lugha za Kibantu katika kundi la Benue Kongo tapo la NaijaKongo (Haspelmath, Dryer, & Comrie, 2008). Oluluyia ni lugha yenye lahaja 17 (Marlo 2007). Oluluyia ni kundi la lugha zinazokaribiana ikiwemo lugha ya Kikisa (Osogo, 1966 Were, 1967, Itabete 1974, Angogo, 1983, Marlo 2007). Idadi kubwa ya Wakisa wenye kuzungumza Kikisa wanapatikana katika gatuzi la Kakamega eneo bunge la Khwisero. Idadi ya Waluhya ni 5,338,666 (hesabu ya watu 2009). Kikisa kina wazungumzaji takriban 137,000 (hesabu ya watu 2009). Kuna majina mbalimbali ya kutambua lahaja hii kama vile Olushisa, Shisa na Olukisa (Ondondo, 2015). Lugha ya Kiswahili ni lugha ya taifa na lugha rasmi nchini Kenya (Katiba ya Kenya 2010). Lugha ya Kiswahili hutumika kama lingua franka nchini Kenya na nje ya mipaka ya Kenya (Massamba 1990, Okombo 2001, Iribemwangi na Mukhwana 2011). Lugha ya Kiswahili inapotekeleza majukumu haya ya kuwa lugha ya taifa, lugha rasmi na lingua franka hutagusana na lugha nyingine. Mtagusano huu husababisha uathirianaji. Uathirianaji huu ndio unaoleta makosa.

Lugha mojawapo inayotagusana na Kiswahili nchini Kenya ni Kiluhya. Kiluhya ni lugha mojawapo ya lugha arobaini na tatu zinazozungumzwa nchini Kenya (Abdulaziz na Osinde 1997). Githiora (2008) anasema, Kiluhya si lugha moja bali ni kundi la lugha zinazokaribiana. Idadi kubwa ya wazungumzaji wa Kiluhya wanapatikana magharibi mwa Kenya. Wengine hutoka sehemu zao asilia na kwenda katika miji kama vile Kisumu, Nakuru, Nairobi na Mombasa. Katika miji hii, lugha zinazotumiwa ni tofauti kwa mfano Kisumu (kijaluo), Nairobi (mchanganyiko) na Mombasa (Kiswahili kwa wengi) (Abdulaziz na Osinde 1997, Githiora 2008). Ni kutokana na kuhama makao asilia ambapo watu hujipata katika hali ya ulazima wa kutafuta lugha nyingine inayoweza kuwapa nafasi ya kutangamana zaidi na hata kusaka kipato. Lugha inayoweza kutekeleza hili kwa urahisi inakuwa Kiswahili kutokana na hali kuwa inafunzwa kama somo la lazima katika shule za msingi na za upili na inatumiwa na kueleweka na zaidi ya asilimia 80 ya Wakenya (Abdulaziz 1972, Heine & Mohlig 1980, Abdulaziz na Osinde 1997, Githiora 2008). Hata hivyo, Kiswahili kinapotumiwa na watu hawa kwa utangamano tofauti huibuka katika

matamshi na matumizi ya maneno kwani wengi wao kwa mfano Nairobi na Kisumu si wazungumzaji wazawa wa lugha hii hivyo basi si lugha yao ya kwanza.

Kikisa na Kiswahili ni lugha za Kibantu. Kwa sababu hii zinakaribiana sana kisarufi na hata katika uundaji wa ngeli za nomino mbalimbali na kisintaksia. Hali hii inaweza kuwafanya watumizi wa Kikisa kujipata katika urahisi wa kutumia Kiswahili lakini kwa wakati huo huo wakipata urahisi wa kuhamisha fonimu na miundo ya maneno ya Kikisa na kuitumia katika Kiswahili kama walivyoeleza Richards (1974) na Mbaabu (1985).

Utafiti huu basi, ulinuia kuangazia leksemu za Kikisa zinavyohusishwa na maana katika Kiswahili Sanifu na leksemu nyingine za Kiswahili zinavyochanganywa na fonimu za Kikisa ili kupata urahisi wa kutamka. Utafiti huu umeangalia jinsi athari hizi, zinazotokana na lugha ya kwanza ya Kikisa, zinavyoathiri maandishi ya wanafunzi haswa katika uandishi wa insha katika shule za msingi na za upili.

Utafiti huu ulilenga kuonyesha hali tatu ambazo ni: wakati neno linapotumiwa na kueleweka, linapotumiwa na kubadili maana na linapotumiwa na kutoeleweka kabisa. Utafiti huu ulichukua mwelekeo wa kisemantiki kwa kujikita kwenye maana za maneno katika Kiswahili Sanifu na jinsi maana za maneno hayo hubadilika wakati mzungumzaji anapohawilisha fonimu za lugha ya kwanza ambayo ni Kikisa katika Kiswahili Sanifu.

Kwa kutumia Nadharia ya Lugha Kati ya Selinker na Nadharia ya Uchanganuzi wa Makosa ya Ellis, utafiti huu ulitafiti athari za Kikisa (lahaja ya Kikisa) katika ujifunzaji wa Kiswahili Sanifu kama lugha ya pili ya wanafunzi walio wazungumzaji asilia wa Kikisa.

Utafiti huu umechukuwa mkondo wa kisemantiki katika uchanganuzi wa athari za Kikisa kwa Kiswahili Sanifu. Fonimu za Kikisa zilizochunguzwa ni zile haswa zinazoleta tofauti za kimaana pekee. Kwa mfano: Koti (goti): makoti (magoti) linatoa maana mbili tofauti sana. Katika mazungumzo ya kawaida ya Wakisa wanapozungumza Kiswahili kauli kama *'alishika koti lake'* kwa maana ya '*alishika goti lake'* zilijitokeza. Kwa kuangalia kwa makini, anayesikiliza akiwa ni ambaye anakielewa Kiswahili Sanifu ataona sentensi sahihi kwa viwango vyote vya kisarufi. Lakini maana iliyolengwa kupitishwa itakuwa tofauti kabisa na atakayoielewa msikilizaji. Mzungumzaji ataridhika kwamba amefikisha ujumbe na msikilizaji ataridhika kuwa ameupata

ujumbe vyema; lakini la kushangaza hapa ni kuwa, wawili hawa huenda watakuwa na maana tofauti ya sentensi hii. Watatoka pale na jumbe tofauti kabisa, mmoja akiwa na maana ya koti kuwa kiungo cha mwili na mwingine akiwa na maana ya koti kuwa vazi. Hali hii inaonyesha umuhimu wa kuwepo utafiti kuhusu swala hili ili kuonyesha wazungumzaji na wasikilizaji wa Kiswahili mambo ya kuepuka au kutarajia kutoka kwa mzungumzaji aliyeathirika kimatamshi wa Kikisa kama lugha yake ya kwanza. Hili linawezesha ujumbe sahihi kuwafikia watu kwa kuwafanya wasikilizaji kuwa makini na hata kuuliza maswali wanapogundua huenda kukawa na utata kimaana.

### 1.2 Tatizo la Utafiti

Mtagusano kati ya lugha mbili au zaidi husababisha uathirianaji kuwili. Hii ina maana kwamba lugha mbili zinapotagusana, moja huweza kuathiri nyingine kwa namna fulani huku nayo ikiweza kuathiriwa na ile nyingine. Athari hizi hutokea kutokana na maingiliano ambayo huwapa matatizo watu wanaojifundisha lugha ya pili ikiwemo ile ya Kiswahili Sanifu (Mbaabu 1985). Mtagusano na mwingiliano huu wa lugha moja na nyingine unaweza pia kuwa msingi wa ujifunzaji wa lugha ya pili kwa kuwa mchakato wa uhamishaji kutoka lugha ya kwanza hadi ya pili humsaidia mtu anayejifundisha lugha ya pili kwa upande mmoja na kwa upande mwingine kuwa chanzo cha ufanyaji wa makosa katika lugha ya pili (Richards 1974). Utafiti huu umechochewa na hali kwamba, ili kuwe na kujifundisha kwema kwa lugha ya Kiswahili Sanifu sharti matatizo ya kisemantiki yanayotokana na athari za kimofofonolojia yaweze kutambulika na kushughulikiwa kikamilifu.

Lugha ya Kikisa, kama lugha nyingine, imekuwa na mwingiliano na lugha ya Kiswahili. Tafiti mbalimbali zimefanywa kuhusu athari zitokanazo na lugha tofauti nchini Kenya kwa Kiswahili zikiwemo; Chepkwony (1993), Onyango (1997), Rapando (2005), Mudhune (2008), Mbula (2011) na Gaithuma (2016). Kwa uelewa wetu, hapana utafiti wowote wa kina uliofanywa kuhusu athari za matamshi ya Kikisa kwa kujifunza kwema kwa lugha ya Kiswahili Sanifu. Hivyo basi, utafiti huu ulifanywa kwa kutumia lugha ya Kikisa kama kielelezo.

### 1.3 Maswali ya Utafiti

(i) Je, kuna tofauti kati ya fonimu za Kiswahili na Kikisa?

(ii) Je, athari za kimatamshi husababisha tofauti zipi za kimaana na kimuundo?

iii) Je, ni athari zipi za kimatamshi zinazojitokeza katika insha za Kiswahili za wanafunzi wazungumzaji wa Kikisa?

(iv) Je, tofauti za kimatamshi na kimaandishi huathiri vipi uelewa wa msikilizaji na msomaji wa Kiswahili Sanifu?

**1.4 Madhumuni ya Utafiti**

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza athari za kimaana zinazojitokeza kutokana na tofauti za fonimu zilizohawilishwa kutoka Kikisa na kutumika kimakosa katika Kiswahili Sanifu. Hili limeafikiwa kwa malengo mahususi yafuatayo:

(i) Kutambulisha tofauti za kifonimu baina ya Kiswahili na Kikisa.

(ii) Kubaini mabadiliko ya kimaana na kimuundo yanayotokea mzungumzaji wa Kiksa anapotumia Kiswahili Sanifu.

(iii) Kuonyesha athari za lugha ya kwanza katika lugha ya pili kwa misingi ya Kikisa na Kiswahili Sanifu kwa kutumia insha za wanafunzi walioathirika kimatamshi.

(iv) Kuchunguza athari za tofauti za kimatamshi na kimaandishi zinavyoathiri uelewa wa msikilizaji na msomaji mahiri wa Kiswahili Sanifu.

**1.5 Sababu za Kuchagua Mada**

Tafiti nyingi zimefanywa kuhusu uathirianaji lakini hakuna utafiti wa kina uliofanywa kuhusisha Kiswahili na Kikisa. Utafiti huu umefanywa ili kujaza pengo la kielimu. Utafiti huu ulishughulikia pia pengo lilopo la kiutafiti linalohusisha athari za lugha ya kwanza kwa Kiswahili kisemantiki. Tafiti za awali zinahusu athari za kimofofonolojia lakini hazihusishi athari hizo na uelewekaji wa maana kwa namna utafiti wa sasa unavyofanya katika kulishughulikia swala hili la athari za lugha ya kwanza kwa Kiswahili.

Utafiti huu ulifanywa ili kuongeza maarifa. Utafiti huu unaongeza maarifa kuhusu uchanganuzi wa makosa katika Kiswahili na kuibua mkondo wa kuyachunguza makosa zaidi ya kuyachanganua tu, kwa kujaribu kuyahusisha na vipengele vingine vya kisarufi kama vile semantiki.

Utafiti huu utawasaidia walimu wa Kiswahili kwa kuwaonyesha makosa yanayofanywa na wanafunzi kutokana na athari za Kikisa , sababu za makosa haya kujitokeza jinsi yanavyotokea ili

kuwapa fursa ya kubuni mbinu bora za kuwafunza wanafunzi wenye hali kama hii wakiwa tayari kuzikabili changamoto hizi katika kufunza kwa lugha ya pili.

Utafiti huu pia utawahamasisha wanaounda mtaala wa elimu kuweza kutilia maanani changamoto zinazowakumba wanafunzi katika ujifunzaji wa lugha ya pili na hivyo kuweka mikakati ya kulikabili hili na kuunda mtaala utakaowasaidia wanafunzi kusoma kwa kutumia mbinu na vifaa vya kimasomo vinavyoweza kuwaimarisha katika Kiswahili kukiwemo mazoezi mengi ya sauti zinazochanganywa na wanafunzi.

Utafiti huu unaunga mkono hoja kuwa wanafunzi hufanya makosa katika uandishi na hata mazungumzo yao ya lugha ya pili. Hivyo basi, ni kazi ya walimu kuwarekebisha. Hata hivyo linakuwa swala gumu kwa walimu kueleza ni kwa nini wanafunzi wanaendelea kulirudia kosa lile lile hata wakati makosa hayo yamezungumziwa kila mara. Swala hili basi linahitaji utafiti kwanza kuelewa jinsi mwanafunzi anavyoielewa lugha na kujifunza lugha ya pili na kisha changamoto anazopitia na makosa anayoweza kuyafanya wakati wa ujifunzaji wa lugha ya pili. Utafiti huu basi unanuia kuonyesha sababu zinazowafanya wanafunzi wa lugha ya pili ambao lugha yao ya kwanza ni Kikisa wanavyobuni mbinu za kurahisisha ujifunzaji wao wa lugha ya pili na mbinu hizo wanazobuni zinavyotokea kuwaathiri kwa njia hasi au chanya.

Walimu wengi hulalamika kuwa wanafunzi hawatumii lugha ya pili kwa kufuata mifumo waliyopewa na wao lakini hili linatokana na walimu kudhani kuwa kinachomtoka mwanafunzi kinahitaji kuwa sawia na alichopewa ambalo ni wazo potovu (Lengo 1995). Ili kuondoa mawazo kama haya mada na utafiti huu ni muhimu ili kuwabainishia walimu mchakato mzima wa ujifunzaji wa lugha ya pili na changamoto zake. Utafiti huu utawasaidia walimu wenye mawazo kama haya kuwa kuna mchakato changamano ambao wanachokisema kinapitikia kabla ya kutolewa na wanafunzi wao. Hivyo uelewa mzuri wa mwalimu haumaanishi uelewa mzuri wa mwanafunzi. Matamshi mazuri ya mwalimu hayana maana ya matamshi mazuri ya mwanafunzi.

Kuchanganua makosa wanayofanya wanafunzi kutawasaidia wanafunzi kujua chanzo cha makosa hayo wanayofanya na kutafuta mbinu za kujiimarisha. Walimu wa Kiswahili wataweza kubuni mikakati ya kutumika katika ufunzaji ili kukabili changamoto hizo wakati wa ufunzaji lugha ya pili ambapo katika muktadha wetu ni changamoto zinazoletwa na athari za Kikisa.

Utafiti huu pia ni muhimu kwa mwalimu wa Kiswahili kwani walimu wengi huchukuwa muda mwingi kuelewa swali la mwanafunzi au hata kuishia kujibu swali tofauti na lililonuiwa na mwanafunzi. Kwa kumtaka mwanafunzi arudie kuuliza mara kwa mara, mwanafunzi huchoshwa na kisha kukinai na hali iwapo hivi mawasiliano yatakatika na ujifunzaji kukatishwa. Kwa kujibu swali tofauti na alivyoulizwa mwalimu, malengo ya kipindi au masomo kwa jumla hayatafikiwa kwani wanafunzi hawataweza kuelewa. Utafiti huu ulinuia kuepusha hali hii. Katika taaluma ya ualimu, pana walimu wanaofunza Kiswahili huku wakiwa na athari za lugha ya kwanza kama vile Kikisa. Utafiti huu utawasaidia wanafunzi kutumia muda mfupi kumwelewa mwalimu wao sio tu wa somo la Kiswahili bali masomo yote pia. Hali hii itaboresha na kukuza uelewanaji.

Lubangah (2018) anasema kuwa, ni vigumu kutambua tofauti zilizopo baina ya lahaja za Kiluhya zinapoishia kwa mfano mpaka kati ya Kimarama-Lushisa na Kiwanga-Kibukusu. Anakiri kuwa Kikisa kinakutana na Kimarama eneo la Bukura ambapo ni vigumu kutofautisha wanaozungumza Kikisa (kutoka Khwisero) na Kimarama (kutoka Butere) hata kwa kuzingatia maneno wanayozungumza. Hivyo basi utafiti huu ulilenga kusaidia katika ufundishaji wa Kiswahili sio tu kwa wanafunzi kutoka jamii ya Kikisa bali kutoka lahaja nyingine zilizo na ukaribu na Kikisa kwa kuwa huenda makosa yakawa sawa kutokana na athari za lugha wanayozungumza na ukaribu kiisimu.

### 1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu unahusu uhawilishaji wa fonimu za Kikisa katika Kiswahili ambao husababisha athari za kimatamshi. Athari hizi za kimatamshi husababisha makosa yafanywayo na wazungumzaji wa Kikisa katika Kiswahili. Utafiti huu ulihusisha wanafunzi wa shule za msingi na upili na walimu wao pekee. Wanafunzi wa shule za msingi walitumika kuonyesha ikiwa athari hizi za ujifunzaji wa Kiswahili kwa wazungumzaji wa Kikisa zinajitokeza moja kwa moja mwanafunzi mwenye asili ya Kikisa anapoanza kusoma lugha ya pili. Wanafunzi wa shule za upili wakitumika kuonyesha uwezekano wa athari hizi kupotea au kujiendeleza na hata kukomaa kiasi cha kutorekebika. Hivi, utafiti huu umeweza kujitokeza na sababu za hali hizi mbili.

Utafiti huu ulijikita kwa walimu na wanafunzi wanaozungumza Kikisa kama lugha yao ya kwanza pekee. Uzungumzaji wa Kikisa kama lugha ya kwanza ulipewa kipaumbele ili kuweza kubaini athari za Kikisa bila kuzihusisha athari hizo na lugha nyingine yoyote. Walimu na wanafunzi

waliolengwa zaidi ni wanauwililugha haswa wa Kikisa kama lugha ya kwanza na Kiswahili kama lugha ya pili. Walimu walioshirikishwa katika utafiti huu walikuwa ni wazungumzaji asilia wa Kikisa wanaofundisha Kiswahili katika Eneo Bunge la Khwisero.

Utafiti huu ulifanyika katika shule za msingi na upili zilizo katika eneo bunge la Khwisero katika Kaunti ya Kakamega. Hili linatokana na hali kuwa Wakisa wengi hupatikana hapa na hivyo Kikisa hutumika kama lugha ya mawasiliano. Hili liliwezesha kupata wanafunzi ambao wametangamana zaidi na Wakisa wenzao na huzungumza Kikisa na marafiki na wazazi wao.

Utafiti huu umehusisha athari zinazopatikana katika vipengele vyote vya kisarufi lakini zinazotokana na uhawilishwaji wa fonimu pekee. Hii ni kwa sababu utafiti huu ulikuwa na mwelekeo wa kisemantiki kwa kuwa haukunuia kuchunguza fonimu zinavyohawilishwa kutoka lugha ya Kikisa hadi Kiswahili pekee bali pia kutathmini jinsi fonimu hizo zinavyoathiri maana katika tungo. Hata hivyo, viepengele vingine vya kisarufi vimetajwa kwa sababu, athari za kifonolojia, husababisha athari za kimofolojia, kisintaksia na vilevile kisemantiki. Hivyo basi, vipengee vingine vya sarufi havijashughulikiwa katika utafiti huu kwa kina bali kwa kutaja tu.

### 1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

Katika sehemu hii tumegawa yaliyoandikwa kwa misingi ya kimaudhui na kiwakati ili kuonyesha maendeleo ya kitaaluma na kiwakati.

Chepkwony (1993) alifanya utafiti unaohusu makosa ya kifonolojia yanayotokea katika wanaojifunza na watumizi wa Kiswahili Sanifu ambao ni wazungumzaji asilia wa Kinandi. Utafiti wake ulionyesha jinsi lugha ya Kinandi inavyoathiri matamshi ya fonimu za Kiswahili. Utafiti wa Chepkwony unaendeleza dhana ya kuathiriwa kwa Kiswahili Sanifu na lugha za kwanza nchini Kenya. Unaonyesha jinsi lugha ya kwanza inavyoweza kuathiri matamshi ya fonimu za Kiswahili. Utafiti wetu ni tofauti na huu kwa kuwa unachunguza zaidi ya athari za kimatamshi tu. Utafiti wa sasa unachunguza zaidi kwa kufafanua athari za athari hizi za kimofofonolojia kwa maana ya maneno na kwa utungo za Kiswahili Sanifu.

Jacobs (1994) anaeleza kuwa, tofauti za kifonimu zinazua tofauti za kimaana. Ikiwa matamshi ya maneno katika lugha fulani yanatofautiana sana na matamshi sahihi ya lugha hiyo lengwa kufikia kiwango cha kutoweza kutambulika, uelewa hupotea. Wazo hili limeelezwa pia na Lanham (1990).

Utafiti huu unaliangazia swala linaloibuka kutokana na kauli za wasomi tuliowataja hapo juu kuonyesha mabadiliko ya kimaana yanayotokea kutokana na mabadiliko ya fonimu faafu katika Kiswahili kutokana na athari za Kikisa.

Jacobs (1994) anafafanua zaidi kuhusu uathirianaji kwa kuonyesha matokeo mabaya ambayo mtagusano mbovu wa kimatamshi unayo kwa ubora wa kozi katika vyuo vikuu, taasisi na vyuo vya mafunzo ya ualimu ambalo ni jambo linaloonyesha uzito wa swala hili la athari za lugha ya kwanza kimatamshi kuathiri maana na hivyo kupoteza uelewa. Hivyo basi, utafiti kama huu una athari za kisayansi na kiutekelezi kwa Kikisa cha sasa, ufunzaji wa Kiswahili Sanifu kwa Wakisa sasa na matumizi ya Kiswahili kwa Wakisa katika sehemu za mawasiliano kwa sababu kutoka nje ya matamshi bora ya Kiswahili kwa Mkisa kunaweza kuleta maana tofauti ambayo inaweza kusababisha kutokuelewana ambako huvunja ubora wa mawasiliano katika mazungumzo (Lanham, 1967). Uelewa wa kina na kindani zaidi wa hali halisi ya utamkaji mbaya na sababu za utamkaji huo, kwa kuangalia hali ya lugha ya kwanza, kwaweza kusababisha ufunzaji mzuri katika uwanja huo wa fonetiki kwa wazungumzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili. Utafiti huu hivyo basi, utatoa maelezo zaidi kuhusu maswala ya mawasiliano na ufunzaji. Kutokana na utafiti huu mambo muhimu kuhusu hali na changamoto zinazohusiana na athari za lugha ya kwanza kwa matamshi ya lugha ya pili zitabainishwa.

Jacobs (1994) anasema kuwa, uelewa huamuliwa na uwekaji pamoja wa sheria nyingi za elementi za kifonolojia. Kuna sababu nyingi zanazokuwa kizingiti cha uelewa. Elementi hizi za kifonolojia ndizo zitakazofuatiliwa na utafiti huu ili kubaini zinavyosababisha kuelewa au kutokuelewa kwa msikilizaji.

Dhana nyingine inayohusiana na utafiti huu ni dhana ya uathirianaji hasi. Weinreich (1953) anafafanua kuathiriwa (kihasi) kwa lugha kama:

> 'Shida za athari za kifonimu zinahusisha namna ambavyo mzungumzaji anavyochukulia na kuzalisha fonimu za lugha moja ambazo zaweza kuwa zimewekwa kimahsusi kama za ziada, kwa misingi ya nyingine, kuitwa za msingi. Kuathiriwa huku kunatokea wakati mwanauwililugha anapotambua fonimu ya mfumo wa lugha ya pili na katika kuitamka, anaiwekea sheria za kifonetiki za lugha ya kwanza'. (tafsiri yetu)

Tunapozungumza kuhusu athari zinazotokana na mtagusano kati ya mifumo miwili ya kifonolojia, (Weinreich, 1953) anatofautisha kati ya aina nne za kimsingi ifuatavyo:

a) *Kutofautisha kwa hali ya chini kwa fonimu*: Hutokea wakati fonimu mbili za mifumo ya lugha ya pili ambazo fonimu lingani katika mfumo wa lugha ya kwanza hazijatofautishwa huchanganywa.

b) *Kutofautisha kwa hali ya juu kwa fonimu*: Huhusisha ulazimishaji wa tofauti za kifonemiki kutoka kwa mfumo wa lugha ya kwanza kwa fonimu za mfumo wa lugha ya pili, pale ambapo hazihitajiki.

c) *Kufafanua tena kwa tofauti zilizopo*: Hutokea wakati mwanauwililugha anapotofautisha fonimu za mfumo wa lugha ya pili kwa nduni ambazo katika mfumo huo ni za pamoja na hazihitajiki, lakini ambazo ni muhimu katika mfumo wa lugha ya kwanza.

d) *Ubadilishaji wa fonimu*: Huhusisha fonimu ambazo zinafanana kabisa katika lugha zote mbili lakini ambazo kutamkwa kwao kwa kawaida kunatofautiana.

Kauli za Weinreich zitatufaa pakubwa katika kuendeleza utafiti huu. Kwa kuzingatia aina hizi nne za kimsingi za athari, tutaweza kutambua wanafunzi wanapochanganya mifumo ya fonimu katika lugha ya pili, kuongeza sauti katika maneno ambazo katika lugha ya pili hazihitajiki na utata wa kutamka fonimu zinazopatikana katika lugha zote mbili lakini matamshi yake ni tofauti kama vile fonimu /b/ inayotamkwa kama /β/ katika Kikisa.

Onyango (1997) alitafiti kuhusu tofauti zilizopo baina ya Kiswahili na Kinyala kwa lengo la kuonyesha uziada wa kisarufi katika Kiswahili cha wanafunzi Wanyala. Utafiti wa Onyango ulionyesha kuwa makosa yanayofanywa na wanafunzi wanaozungumza Kinyala kama lugha yao ya kwanza katika Kiswahili Sanifu yanatokana na athari ya za Kinyala. Makosa yalipatikana katika kategoria ya virejeshi, nafsi na tarakimu. Utafiti wa Onyango utatufaa katika kueleza jinsi Kiswahili kinavyotagusana na lugha mbalimbali na hivyo kuathiriwa na kuathiri. Utafiti huu ulitusaidia kuonyesha kuwa tayari kuna athari za Kiluhya katika Kiswahili Sanifu. Utafiti wa sasa unatofautiana na wa Onyango kwani huu wa sasa unajikita katika uhawilishaji wa fonimu na kufafanua athari zake kimaana. Hili tofauti na utafiti huu wa Onyango.

Chimerah (1998) alitoa fafanuzi za maana ya lugha ya kwanza na lugha ya pili na mazingira ambamo lugha hizi hukua. Kuhusu lugha ya mama, Rocha anaeleza kuwa hii ni lugha ni lugha anayojifundisha mtu kwa mara ya kwanza maishani mwake. Fasili hii inaungwa mkono na Wolff

(2016) anapofafanua kuwa lugha ya mama barani Afrika ni tofauti na lugha ya mama bara Ulaya. Wolff anaeleza kuwa lugha ya mama ni lugha ya kwanza anayojifunza mtu kwa mara ya kwanza ambayo aghalabu huwa ni lugha ya baba au ukoo wa baba. Chimerah (1998) anaendeleza mjadala wake kwa kauli kuwa lugha ya pili ni lugha anayojifundisha mtu baada ya lugha ya kwanza. Mara nyingi, lugha ya kwanza hujifunzwa katika njia zisizorasmi kama vile kwa kuwasikiliza wenzake wanapocheza pamoja au kabisa kukaa katika mazingira panapotumiwa lugha husika. Hata hivyo, lugha hizi huweza kufundishwa pia kwa njia rasmi shuleni kama vile Kiswahili darasani. Kauli na maoni ya Chimerah (1998) yalitufaa sana katika utafiti huu. Mawazo haya kuhusu lugha ya kwanza na lugha ya pili ndio msingi wa maana ya maneno hayo yalivyotumiwa katika muktadha wa utafiti huu.

Mudhune (2008) alichunguza athari za Kidholuo kwa wanaojifunza Kiswahili. Utafiti wake uliweka bayana makosa yanayofanywa na wajifunzaji wa Kiswahili walio wazungumzaji asilia wa Dholuo. Matokeo ya Utafiti huu yalionyesha kuwa wajifunzaji wa Kidholuo walihamisha vipengele vya kisarufi katika Kidholuo hasa katika kiwango cha fonolojia hadi katika Kiswahili Sanifu. Utafiti huu wa Mudhune ulibaini kuwa makosa ya kifonolojia yanakuwa mengi hata zaidi wanafunzi wanapokutana na sauti ambazo zipo katika Kiswahili lakini hazipo katika Kidholuo. Utafiti wa sasa una tofauti kubwa na huu wa Mudhune. Utafiti wa sasa unaangazia vipengele vyote vya sarufi vinavyoathiriwa na uhawilishwaji wa fonimu za lugha ya Kikisa kwa Kiswahili. Utafiti huu aidha, ulizamia swala la athari za kisemantiki zinazotokana na athari hizo za lugha ya kwanza. Jambo hili la kuhusisha athari za lugha ya kwanza na athari zake katika lugha ya pili kisemantiki halijashughulikwa kabisa na utafiti huu. Utafiti huu wa Mudhune ulikuwa wa muhimu kwetu katika kujifunza kuhusu athari za kifonolojia na jinsi zinavyojitokeza katika Kiswahili.

Kikisa, kama lugha inayochunguzwa athari zake kwa Kiswahili Sanifu, imeandikiwa machache na Ondondo (2015). Ondondo (2015) alibainisha ngeli kumi na sita za Kikisa. Alichunguza mofolojia na mfumo wa maneno ya Kikisa. Utafiti wake unaonyesha Kikisa kina mfumo kama ule wa lugha nyingine zote zilizo za Kibantu. Utafiti wa Ondondo utatofautiana na huu wa sasa kwa misingi kuwa huu unahusisha Kikisa na Kiswahili na sio alivyochunguza yeye. Utafiti wake unayaangalia maneno na mifumo yake ilhali huu unaangalia maana ya maneno kutokana na athari za kubadili fonimu yanayotokana na athari za Kikisa. Utafiti wake utakuwa wa muhimu katika kutuonyesha maneno ya Kikisa, mifumo na ngeli zake. Ngeli hizi zitatumika kuonyesha utata unaojitokeza

wakati ngeli hizo zinapojaribu kutumiwa katika Kiswahili na wanafunzi wa Kiswahili kama lugha ya pili.

Wafula na wenzake (2016) walifanya utafiti kuhusu leksikosintaksia ya lahaja za Kiluhya. Matokeo ya utafiti wao yalidhihirisha kuwa lahaja za Kiluhya ni za nasaba moja kwani zina sifa nyingi zinazofanana. Walisema kuwa, lahaja za Kiluhya zina mifumo sawa ya kisintaksia na vilevile kileksia (Wafula et al, 2015). Matokeo ya utafiti huu yanazidisha kuonyesha umuhimu wa utafiti wa sasa kwani matokeo yake yanaweza kutumiwa na walimu wa lahaja takriban zote za Kiluhya kufunza na kurekebisha makosa yanayotokea mara kwa mara.

Utafiti wa Wafula (2016) unaendelezwa na utafiti wa Lubangah (2018) ambao unahusu glosia katika lahaja za Kiluhya. Anasema kuwa ni vigumu kutambua tofauti zilizopo baina ya lahaja hizi zinapoishia kwa mfano mpaka kati ya Kimarama-Lushisa na Kiwanga-Kibukusu. Lubangah anasema kuwa Kikisa kinakutana na Kimarama eneo la Bukura ambapo ni vigumu kutofautisha wanaozungumza Kikisa (kutoka Khwisero) na Kimarama (kutoka Butere) hata kwa kuzingatia maneno wanayozungumza. Utafiti wa Lubangah unaongeza umuhimu wa utafiti huu wa sasa. Hili lina maana kuwa matokeo ya utafiti huu yataweza kuwasaidia walimu katika ufunzaji wa sio tu watoto kutoka jamiilugha ya Kikisa bali kutoka lahaja nyingine zilizo na ukaribu na Kikisa kwa kuwa huenda makosa yakawa sawa kutokana na athari za lugha wanayozungumza na ukaribu kiisimu. Utafiti wa Lubangah hata hivyo, utakuwa tofauti na huu wa sasa kwa sababu utafiti wake unaangazia glosia na unafanywa kutumia lahaja mbili kiulinganishi kinyume na utafiti wa sasa unaoangalia Kikisa bila kukilinganisha na lahaja nyingine ila kuzingatia mifumo ya fonimu za Kikisa zinavyoathiri maana katika Kiswahili Sanifu zinapohamishwa na kimakosa.

## 1.8 Misingi ya Nadharia

Utafiti huu utaongozwa na nadharia mbili : Nadharia ya uchanganuzi makosa na nadharia ya lugha kati. Nadharia hizi zilitusaidia kuonyesha makosa yanayofanywa na wanafunzi wanapozungumza Kiswahili Sanifu kutokana na athari za Kikisa na utafutaji wa lugha hizi mbili katika juhudi za kuboresha ufahamu wao wa lugha ya pili ambayo ni Kiswahili Sanifu.

### *1.8.1 Nadharia ya Uchanganuzi wa Makosa*

Ellis (1994) anasema, makosa ni kutoka nje ya kanuni za lugha lengwa. Ni matokeo ya mchakato wa matatizo yanayowazuia wanafunzi kupata maarifa ya sheria za lugha lengwa zinazowafanya kutafuta mbinu mbadala ambayo haijakubalika wanayoipata kuwa rahisi.

Brown (1980) anasema, uchanganuzi wa makosa ni njia ya kuangalia, kuchanganua na kupanga makosa mbalimbali kutoka kwa sheria za lugha ya pili na kuweka wazi mifumo inayowezesha hali hii. Ni mbinu inayofasiri mifumo isiyokubalika inayotumiwa na wanafunzi wa lugha ya pili.

#### *1.8.1.1 Mchakato wa Utafiti Kuhusu Makosa*

Corder (1984) anabainsiha michakato mitano inayoweza kutumiwa kutambua makosa yanayofanywa na wanafunzi ikiwemo: Ukusanyaji wa data, ubainishaji wa makosa, ufafanuzi wa makosa na tathmini ya makosa.

*Ukusanyaji data***:** Sampuli zinazofaa kuchukuliwa kutoka kwa watifitiwa kwa kufuata sheria na vigezo vyote vinavyofaa. Ukusanyaji wa data unafanywa kwa makini ya kutambua maana lengwa ya mzungumzaji ili kubaini makosa kamili katika neno au kauli yake.

*Ubainishaji wa makosa:* Mtafiti anahitajika kubainsha makosa kwa kuangalia kile alichotoa kama jibu mtafitiwa na kile alichodhamiria ili kupata makosa kwa usahihi.

*Ufafanuzi wa makosa:* Ufafanuzi wa makosa ni wa kiulinganishi kwani huhusisha kulinganisha makosa yaliyofanywa na wanafunzi na mifumo sahihi katika lugha lengwa. Huonyesha kiwango cha makosa anayofanya mwanafunzi wa lugha ya pili kwa kuzingatia matarajio ya lugha ya pili na yale aliyoyaandika au aliyoonesha. Baada ya makosa kubainishwa hufafanuliwa na kuwekwa katika makundi. Hili husaidia mtafiti kubaini umbali wa makosa aliyofanya mwanafunzi au mtafitiwa kutoka kwa mfumo wa lugha lengwa unaohitajika. Mchakato huu ni wa kiulinganishi.

*Tathmini ya makosa:* Makosa yanahitaji kubainishwa na kisha kufafanuliwa. Maelezo kuhusu makosa ili kutoa tathmini hufanywa kwa kuzingatia vigezo mbalimbali kama vile:

i) *Uhawilishaji kimakosa*: Uhawilishaji kimakosa unahusisha pale mwanafunzi wa lugha ya pili anatumia mfumo wa lugha ya kwanza kuunda sentensi.

ii) *Ujumlishaji mno:* Ujumlishaji mno ni pale mwanafunzi wa lugha ya pili anapotumia kwa kupindukia sheria au kanuni moja ya kisarufi na hivyo kuishia kuunda mifumo isiyokubalika katika lugha husika.

iii) *Upuuzaji wa mipaka/vikwazo*: Upuuzi wa mipaka huhusisha kutumia sheria au kanuni mpaka mahali isipotumika.

iv) *Kutotumia kanuni kikamilifu*: Kutotumia kanuni kikamilifu ni hali inayofungamana na kutojifunza mifumo ya lugha ya pili kikamilifu kwa kutaka kutumia inayoonekana rahisi anayoona inawezesha mawasiliano.

v) *Makisio yasiyofaa ya dhana*: Makisio yasiyofaa ya dhana ni hoja inayohusu makosa yanayotokana na uelewa mbaya wa tofauti ya lugha kwanza na ya pili.

*1.8.1.2 Aina za Uchanganuzi wa Makosa*

Keshavars (1997) alipendekeza aina mbili za uchanganuzi wa makosa:

*1.8.1.2.1 Uchanganuzi wa Kinadharia wa Makosa*

Huhusisha mchakato na mikakati ya ujifunzaji lugha na mfanano wake na upokeaji wa lugha ya kwanza. Hujaribu kuchunguza kinachoendelea katika akili za wanafunzi wa lugha. Hujaribu kuondoa mikakati ya wanafunzi ya kujumlisha na kurahisisha na kuangalia kama kuna ubia katika mchakato wa kujifunza lugha yaani kama kuna mtaala wa ndani wa kujifunza lugha ya pili.

*1.8.1.2.2 Uchanganuzi wa Makosa Kiutelekelezi*

Huhusu kupanga mafunzo ya ziada na kubuni vifaa vifaavyo na mikakati ya kufunza kwa misingi ya matokeo katika uchanganuzi wa makosa kinadharia. Mtafiti hujaribu kuchanganua sababu za makosa yaliyobainishwa. Hata hivyo, haya ni ya kukisiwa tu kwa maana alichowaza mtafitiwa kimo katika ubongo wake ambao hatuwezi kuufikia. Mwalimu anahitaji kutambua makosa na vilevile kuelewa sababu za kisaikolojia zinazosababisha makosa hayo (Corder 1981).

### *1.8.2 Nadharia ya Lugha Kati*

Ellis (1989) anadai kuwa, nadharia ya Lugha Kati ni nadharia inayokita mizizi yake kwa juhudi za watafiti juu ya upataji lugha ya pili ili kuweza kubainisha daraja za maendeleo ya kujifunza ambazo wanafunzi wa lugha ya pili hupitia katika kujifunza lugha ya pili kwa ufasaha au kukaribia umilisi wa lugha hiyo ya pili.

Selinker (1992) anafafanua kuwa, Lugha Kati huibuka katika mazingira ambamo mwanafunzi wa lugha ya pili huchanganya sifa za lugha ya kwanza na hiyo ya pili. Mwanafunzi huyu wa lugha ya pili huwa hajakuwa na uwezo dhabiti ingawa yu karibu na lugha lengwa. Mwanafunzi aliye katika hali kama hii huhifadhi baadhi ya sifa za lugha ya kwanza au kujumlisha kanuni za lugha lengwa katika kuzungumza au kuandika lugha lengwa na hivyo kuibuka na uvumbuzi. Kanuni za Lugha Kati zinaundwa kutokana na:

i) Uhamishaji lugha ya kwanza,

ii) Uhamishaji wa yaliyosomwa,

iii) Mbinu za kufunza lugha ya pili,

iv) Mbinu za mawasiliano katika lugha ya pili na

v) Ujumlishaji wa ruwaza za lugha lengwa.

Lugha Kati inaweza kufikia hatima yake na kukosa kuendelea kukua katika daraja za uendeleaji.

Kwa mujibu wa Tarone (2006), dhana ya Lugha Kati iliasisiwa na mwanaisimu wa Kimarekani aliyeitwa Larry Selinker (1972). Tarone alielezea kuwa nadharia ya Lugha Kati ni mfumo wa kiisimu unaodhihirika wakati mwanafunzi wa lugha ya pili anapojaribu kuwasilisha maana katika lugha anayojifundisha. Lugha Kati ni mfumo wa kando wa kiisimu ambao ni tofauti kabisa na lugha asilia ya mwanafunzi na lugha lengwa anayojifundisha ingawa unahusiana na lugha asilia na lugha lengwa kwa vibainishi na mielekeo ya lugha kati ya mwanafunzi. Mfumo huu wa kiisimu unajumuisha sio tu vitengo vyote vya sarufi, bali pia daraja mbalimbali za mazungumzo ya Lugha Kati.

Selinker (1992) anafafanua kuwa, Lugha Kati inaona uhawilishaji wa lugha kama mchakato wa kiuteuzi na wala sio tu ufanyaji wa makosa katika lugha ya pili au shida za kujifunza lugha ya pili (Selinker 1992, Gass & Selinker 1983a, Kellerman & Smith 1986). Wazo hili linashikiliwa pia na Lado anayesema kuwa watu huwa na mazoea ya kuhamisha mifumo, maana na msambao wa mifumo na maana katika lugha ya kwanza na utamaduni wake hadi katika lugha ya kigeni na utamaduni wa lugha hiyo ya kigeni (Lado, 1957).

Nadharia ya Lugha Kati inaelezea kuwa mtu anapojifundisha lugha ya pili hawezi kupata ufahamu kamili wa lugha hiyo. Kuwa, anayefundishwa hawezi kuzungumza sawa na mzawa wa lugha hiyo. Kinachofanyika ni kuwa, lugha atakayoizungumza mwanafunzi wa lugha hiyo huwa ni lugha iliyo kati ya lugha yake asilia na lugha ya pili anayojifunza. Lugha atakayoizungumza itakuwa tofauti kisifa na lugha ya kwanza lakini haiwezi kufikia kiwango cha lugha ya pili. Hili litatokea kwa misingi kuwa vipo baadhi ya vipengele vya lugha hiyo ambavyo hataweza kuvipata katika ujifunzaji wa lugha hiyo. Hata hivyo kwa mipango dhabiti huenda msemaji akakaribia kufikia uzungumzaji na uelewa bora wa lugha ya pili. Ikiwa ulinganishi wa lugha ya kwanza na ya pili utafanywa na ufunzaji ufanyike kwa makini itakuwa rahisi kwa mwanafunzi wa lugha ya pili kuelewa. Kwa mfano hatua ya kwanza ni kuelewa uhawilishaji wa lugha. Jambo hili linasisitizwa na Selinker (1992). Kuwa, uhawilishaji wa lugha ni hatua ya kwanza na muhimu zaidi katika ujifunzaji lugha kwa kulinganisha lugha ya kwanza na lugha ya pili jambo ambalo husababisha kujitokeza kwa haipothesia muhimu katika uelewa wa fenomena ya uhawilishaji wa lugha (Gass & Selinker 1983a, Smith 1986).

Wasomi kama vile Weinreich (1953), Corder (1973), Selinker 1985), na Lewis 1988) wanashikilia kuwa kunakili ruwaza za lugha ya kwanza katika lugha ya pili kuna matokeo anuwai kwa utamkaji wa lugha ya pili.

Fledge anasema kuwa:

> Kuwepo kwa upekee katika sauti za usemi katika lugha ngeni ndiko sababu ya kutokea kwa Lugha kati na sio tokeo la athari kati ya lugha ya kwanza na lugha ya pili‘ (Fledge 1980:133). Kuwa, watu binafsi wanaojifunza lugha ya kigeni huweza kufinyanga ruwaza za kifonetiki zilizopo tayari kwa kasi tofauti, kuwa polepole katika kupata mifumo ya kifonetiki ya lugha lengwa na kuchukua mikakati tofauti ya kifonetiki ya kuzalisha sauti mpya au tofauti kifonetiki katika lugha ya pili (Fledge 1980:133).

Fledge (1980) anasema: makosa ya kimatamshi ya mwanafunzi hayawezi kila mara kuafiki fonimu zinazopatikana katika lugha ya kwanza na lugha ya pili. Kulingana Fledge na Hillenbrand (1984), msemaji anaweza kuweka fonimu katika makundi kiakustika katika lugha ya pili kama za kufanana kabisa, zilizo sawa au mpya. Wanaeleza fonimu sawa kama fonimu ya lugha ya pili ambayo inatambulika kwa namna tofauti kiakustika kuliko fonimu nyingine ambayo yaweza kutambulika kwa urahisi katika lugha ya kwanza.’

Fonimu mpya ni fonimu ya lugha ya pili ambayo haina fonimu lingani katika lugha ya kwanza na huenda isihukumiwe kama inayoafikiana na kategoria ya lugha ya kwanza. Fledge anasema kuwa, sehemu ya fonolojia huundwa upya wakati wa kujifunza lugha ya pili na kuwa kutafuta fonimu zinazokubaliana kwa lugha nyingine huwafungia wanafunzi wa lugha ya pili kutamka fonimu zilizo sawa katika fonimu za lugha ya pili lakini sio fonimu mpya za lugha ya pili (Fledge 1987). Hata hivyo, wanafunzi wa lugha ya pili ambao wana umri mkubwa wanaweza kutoa fonimu za lugha ya pili zisizokuwa katika lugha ya kwanza kikamilifu, lakini sio zile ambazo zina fonimu lingani zinazotambulika katika lugha ya kwanza.

Fledge (1980) anahitimisha mjadala wake kwa kusema kuwa:

1. Fonimu za lugha ya pili zinazotolewa na wanafunzi wa lugha hiyo huwa ni za kati baina ya zile za lugha ya kwanza na lugha ya pili.

2. Fonimu za lugha ya pili yakiwemo matamshi yasiyosahihi, hutamkwa kwa utaratibu fulani katika miktadha sawa ya kifonolojia na wanafunzi wa lugha .

3. Wanafunzi kwa upekee wao wanaweza kukumbatia mikakati tofauti ya kifonetiki ili kutoa sauti za lugha ya pili.

Katika uhawilishaji wa lugha ambao husababisha athari, makosa ya kimatamshi hutokea kwa sababu ya ruwaza za lugha ya kwanza kuhamishiwa katika lugha ya pili. Fledge anasema kuwa dhana ya Lugha Kati huwa na maana ya maendeleo ya polepole kukuza uwezo wa kiisimu katika lugha lengwa, ikiwa na maana ya sauti mpya hutamkwa kwa kutofuata ruwaza za lugha ya kwanza au hata ya pili bali kati yazo.

Selinker (1972) anataja michakato ya kisaikolojia ambayo ni muhimu katika uchanganuzi wa Lugha Kati kama vile:

1. Uhamishaji lugha hasa kanuni na mifumo

2. Mikakati ya ufundishaji mbaya wa lugha ya pili kutokana mbinu, uelewa na umilisi wa kiisimu mbaya wa mwalimu.

3. Kujumlisha zaidi kanuni za lugha lengwa

4. Kusahilisha sarufi ya lugha ya pili ili kuongeza mawanda ya mawasiliano

5. Kubuni mkakati wa mawasiliano katika lugha ya pili

*1.8.2.1 Chukulizi za Lugha Kati*

Katika mjadala wa wasomi (Selinker 1972, Lado 1957, Fries 1945, Goffman 1974) panajitokeza chukulizi za wazi kuhusu nadharia ya Lugha Kati:

i) Lugha Kati hujitokeza kati ya lugha ya kwanza na lugha lengwa ambayo inaonekana katika matokeo ya ujifunzaji wa lugha ya pili wa mwanafunzi.

ii) Kuna vipengele vya kiutambulisho vya lugha kati ambavyo havitoshani na kiwango cha vipengele vya mwanzo vya sarufi na fonolojia husika katika uchunguzi.

iii) Ufanisi wa upokeaji wa lugha ya pili kwa wanafunzi wengi wa lugha ya pili ni upangaji upya wa vipengele vya kiisimu kutoka kwa lugha kati hadi kufikia utambulisho wa lugha lengwa.

iv) Kufikia wa ukubalifu katika lugha lengwa kwa wanafunzi wengi kwawezekana kwa sababu watu wazima (asilimia tano hivi) ambao wanaonekana kupata umilisi wa mzungumzaji mzawa wa lugha husika hawajafunzwa kupitia kufafanuliwa na kuelezwa bali wameweza kuzipiku changamoto za uhawilishaji lugha (Selinker 1992).

Nadharia ya Lugha Kati na mihimili yake kama tulivyojadili ni ya muhimu sana katika utafiti huu. Ili kutimiza malengo ya utafiti huu, nadharia ya Lugha Kati kupitia kwa vipengele vilivyojadiliwa na wasomi tuliowataja, kama vile Fledge na Selinker, tunaweza kubainisha fonimu tofauti baina ya Kiswahili na Kikisa na kutambulisha makosa yanayofanywa na sababu zake zinazotokana na uhamishaji wa vipengele vya kanuni na mifumo. Vipengele hivi vya Lugha Kati vilituwezesha kubainisha makosa, kuyachanganua na kuzieleza sababu za makosa hayo haswa yanapohusiana na uhamishaji hasi unaosababisha makosa katika lugha ya pili ambayo katika muktadha huu ni Kiswahili.

Kipengele anachotaja Selinker kuhusu ufundishaji mbaya kuwa sababu mojawapo inayoweza kuleta Lugha Kati ni muhimu katika kazi hii. Ufundishaji wa lugha ya Kiswahili ni kiundo muhimu katika uelewa na matamshi ya wanafunzi. Nadharia hii ya Lugha Kati imewezesha kutathmini visababishi vya makosa ya watafitiwa ili kutoa uchanganuzi wenye maelezo ya kina kuhusu nafasi

ya ufundishaji katika upitishaji wa athari za lugha ya kwanza kwa lugha ya pili. Yaani katika muktadha huu, tumeweza kutumia nadharia hii na hasa kipengele cha ufundishaji, kufafanua nafasi ya mwalimu wa Kiswahili katika kumpokeza mwanafunzi athari za Kikisa. Mbinu za ufundishaji pia zimeweza kutathminiwa kupitia mihimili ya nadharia hii ili kubaini vipengele na masiala mbalimbali yanayosababisha na kuendeleza ukuzaji wa Lugha Kati.

Nadharia hii imekuwa muhimu katika ubainishaji wa sababu za makosa yanayofanywa na wanafunzi. Kipengele cha kubuni mikakati ya mawasiliano na usahilishaji wa sarufi ya lugha ya pili ni msingi wa utafiti huu. Nadharia hii imetusaidia kufikia lengo la kueleza sababu za ujitokezaji wa makosa. Vilevile, kutokana na utambuzi wa maswala haya, tumeweza kupendekeza mbinu za kusuluhisha au hata kuwasaidia wanafunzi kukwepa msukumo wa kubuni Lugha Kati kwa kusahilisha sarufi ya Kiswahili.

Kimsingi, nadharia ya Lugha Kati imetuwezesha kutathmini uhamishaji lugha ya kwanza, uhamishaji wa yaliyosomwa, mbinu za kufunza lugha ya pili, mbinu za mawasiliano katika lugha ya pili na ujumlishaji wa ruwaza za lugha lengwa kama sababu na chanzo cha ujuitokezaji wa makosa katika Kiswahili yanayotokana na athari za Kikisa. Uchunguzi wa vipengele hivi wakati wa ukusanyaji data na uchanganuzi wake vimetuwezesha kufikia malengo ya utafiti yakiwemo kutathmini athari za Lugha Kati kwa wanafunzi wa lugha ya pili yaani Kiswahili katika upitishaji na uelewaji wa maana ya kinachosemwa na kinachokusudiwa kusemwa. Kwa kuonyesha athari za Lugha Kati kwa Kiswahili, tumeweza kuweka wazi haja ya kuepukana na mambo yanayoweza kukuza zaidi lugha hiyo kwani ina uwezo wa kukomaa au hata kufikia hatima yake na kukosa kuendelea kukua katika daraja za uendeleaji kama anavyoeleza Selinker (1972).

## 1.9 Mbinu za Utafiti

Katika sehemu hii, tumezungumzia mahali pa utafiti, uteuzi wa sampuli, mbinu za ukusanyiaji data, uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa data husika.

### *1.9.1 Utafiti wa Nyanjani*

Tulikwenda nyanjani na kuhudhuria vikao vya mijadala miongoni mwa wanafunzi. Tuliwahoji walimu wa Kiswahili na wanafunzi wa shule za msingi na upili ili kupata msambao wa athari za uhawilishaji wa fonimu miongoni mwa vikundi husika. Mahojiano hayo yalinuiwa kusaidia katika kubainisha makosa ya kimatamshi yanayoleta utata katika maana. Wanafunzi walihojiwa kwa nia

ya kubaini athari za kimatamshi wanapojibu maswali. Pia, walisoma maneno yenye fonimu tofauti (vitate) ili kubaini uwezo wao wa kutofautisha fonimu tofauti zinazokaribiana

Isitoshe, tuliweza kupata changamoto wanazokabiliana nazo wakati wa kujifunza lugha ya pili, yaani, Kiswahili Sanifu. Pia, tulitumia uchunguzi shiriki kama njia ya ukusanyiaji wa data ambapo tulihudhuria mijadala ya wanafunzi kupata sio tu maandishi katika insha zao na majibu yao ya maswali bali pia athari zinavyojitokeza kimatamshi wanapotumia Kiswahili Sanifu kiutekelezi katika maisha yao ya kawaida shuleni wanapozungumza na kujadili. Uchunguzi shiriki ulitumika kupitia kushiriki katika mijadala ya wanafunzi ili kubaini makosa ya kimatamshi kiutekelezi na kubaini athari zake kwa maana inayoeleweka kwa wasemaji mahiri wa Kiswahili. Tulirekodi mazungumzo na mijadala hiyo kwa simu na kuhifadhi kwa ajili ya uchanganuzi baadaye. Insha za wanafunzi zilitumika kutambua ithibati za athari za Kikisa katika Kiswahili chao kimaandishi. Tulisoma insha za wanafunzi, tukazichambua ili kutambua na kuchanganua makosa katika insha hizo za wanafunzi. Huku sababu za makosa hayo kutokea zikibainishwa kupitia mlinganisho wa yanayosemwa na yaliyodhamiriwa kwa kufuata mwongozo wa Selinker (1992).

#### *1.9.1.1 Eneo la Utafiti*

Utafiti huu ulikuwa wa maktabani na nyanjani. Maktabani tulipata vitabu, majarida ya kiakademia na makala za kiusomi kuhusu mada ya utafiti na vijimada vyake kama vile uathirianaji wa lugha, lugha za Kiswahili, Kiluhya na Kikisa, nadharia ya Lugha Kati na Nadharia ya Uchanganuzi wa Makosa.

Nyanjani, utafiti ulifanyika katika Gatuzi la Kakamega, eneo bunge la Khwisero. Utafiti huu ulihusisha shule za msingi na upili zinazopatikana katika eneo bunge la Khwisero.

#### *1.9.1.2 Uteuzi wa Sampuli*

Tulitumia sampuli ya kimakusudi, sampuli nasibu na sampuli nasibu tabakishi kuziteua shule katika eneo bunge la Khwisero. Kwa ushirikiano na walimu wa Kiswahili wa shule hizi, tuliweza kupata insha za wanafunzi na kuhoji baadhi. Sampuli ya kimakusudi ilitusaidia kuwapata wanafunzi ambao walikuwa wameathirika na kwa sababu ya athari hizi za Kikisa kwa matumizi yao ya Kiswahili, matokeo yao ya mitihani yakawa yanaathirika. Hawa ndio waliohojiwa. Sampuli ya maksudi ilitumika kuwateua wanafunzi wanatumizi wa Kikisa kama lugha yao ya kwanza. Uteuzi wa kimaksudi ulitokana na uzingatiaji wa sifa kuu ya watafitiwa, ambapo walihitajika

kuwa, wazungumzaji wa lugha ya Kikisa kama lugha ya kwanza na Kiswahili Sanifu kama lugha ya pili. Tuliwahoji na kurekodi mahojiano shuleni. Sampuli nasibu tabakishi ilisaidia utafiti huu kuhakikisha kuwa kila eneo la Khwisero limeweza kutafitiwa na matokeo yake kuchanganuliwa.

Tuliwahoji wanafunzi pamoja na walimu wa Kiswahili. Walimu walihojiwa ili kupata umilisi wa walimu na kubaini ikiwa walimu wana athari zozote za Kikisa. Uchunguzi wa walimu hawa ulitusaidia kufikia lengo la kutathmini mbinu za ufundishaji na athari za ufundishaji mbaya kwa lugha ya wanafunzi. Tulichunguza pia insha zinazoandikwa na wanafunzi wanaozungumza Kikisa kama lugha yao ya kwanza. Tulichunguza insha hizo ili kupata makosa ya kisarufi yanayotokana na athari za Kikisa katika matumizi yao ya Kiswahili Sanifu.

Shule saba kutoka eneo bunge la Khwisero zilichaguliwa ili kutumika katika utafiti huu. Uteuzi wa shule hizi ulifuata uteuzi wa sampuli ya kimaeneo ambapo shule saba ziliteuliwa moja kutoka kila lokesheni saba za Khwisero. Shule zilizotafitiwa zilikuwa shule za kutwa. Uamuzi huu ulifikiwa hivi kwa sababu athari zinazochunguzwa na utafiti huu nyingine zinatokana na athari wanazopokea wanafunzi kutoka kwa wanajamii wanaozungumza kwa athari. Pia, wanafunzi wanapokuwa nyumbani ndipo wanapojipata zaidi na haja ya kuzungumza kwa Kikisa kwani mazingira hayo yanakuwa na watumizi wengi wa lugha hiyo. Kutokana na kuzungumza Kikisa na mazoea hayo ndiyo husababisha urahisi wa kujitokeza kwa athari za Kikisa katika matumizi yao ya Kiswahili Sanifu.

Tulizichunguza insha za darasa moja la shule ya msingi na moja la shule ya upili katika kila lokesheni tuliyotafiti. Shule za msingi zilitusaidia kuona makosa yanayofanywa na wanaojifunza Kiswahili Sanifu ambao bado lugha waliyo na umilisi mkubwa kwayo ni Kikisa, makosa yanayoanza mapema mwanafunzi anapoanza kujifunza lugha ya pili na kisha kutambua makosa yanayoendelea na yanayopotea wanapofika shule ya upili. Kupitia uteuzi huu tuliweza kubaini kuwa makosa katika lugha ya pili huanza moja kwa moja mwanafunzi anapoanza kujifunza lugha ya pili na kuona ni vipi mazingira yake yanavyochangia ubebaji huu wa sifa na mifumo ya lugha ya kwanza hadi lugha ya pili. Wanafunzi wa shule za upili walitusaidia kuona makosa yaliyoendelea tangu shule za msingi hadi shule za upili. Tulichunguza pia makosa yaliyopotea baada ya wao kuingia shule ya upili. Tulichunguza athari za makosa hayo kwa uandishi wao wa insha.

#### *1.9.1.3 Vifaa vya Utafiti*

Katika utafiti wetu tulitumia data msingi. Data msingi ni taarifa au maandishi asilia ambayo mtafiti hupata baada ya kufanya utafiti nyanjani hivyo habari hizi huwa hazijaathiriwa na vishawishi vyovyote.

Selinker (1992) anatoa njia tatu za ukusanyaji data pale tunapotaka kupata makosa na kubainisha uwepo wa Lugha Kati:

i) *Ushahidi wa kitajriba*: huu ni utafiti unaohusisha data inayotolewa  kutoka kwa tajiriba za mtu binafsi kuhusiana na kujifunza lugha ambapo huweza kupatikana ndani ya rekodi ya matukio ya kila siku. Utafiti huu, huhusisha yale mhusika anayojua ndio ukweli kuhusu mchakato wa upataji wa lugha ya pili na lugha kati kupitia matokeo ya tajiriba yake mwenyewe. Kwa mfano kama mwanafunzi wa lugha ya pili yeye mwenyewe huku akijumlisha tajiriba zake kuwa hivyo kwa wote wanaopitia mchakato huo (Selinker 1992).

ii) *Ushahidi kupitia utazamaji*: hii ni data inayopatikana kwa kutazama wanafunzi wa lugha wakiwa katika utendaji wa shughuli zao za darasani. Ushahidi huu unaweza kupatikana kupitia kutazama shughuli na matukio ya darasani. Ushahidi wa aina hii huhusu kile mtu anachojua kuhusu lugha ya pili na kile anachokiona kutoka kwa tajriba za kibinafsi lakini mara hii kama mtazamaji aliyeshuhudia akiwa pamoja na wanafunzi wengine wa lugha ya pili au ya kigeni. Tajiriba kama mwalimu wa kufunza lugha ya pili ndio mfano mzuri katika utafiti huu (Selinker 1992).

iii) *Ushahidi wa kiuchunguzi*: Hii ni data inayopatikana kupitia uchunguzi uliopangwa na kufanywa kwa umakini mkubwa. Utafiti huu waweza kuwa wa kihadhi au kikesi, kiidadi, kiuchunguzi au mchanganyiko wa yote. Utafiti huu huhusisha kile mtu anachokijua kuhusu michakato ya ujifunzaji lugha ya pili lakini kama mtu mwenye tajiriba tofauti. Pia, utafiti wa aina hii huhusisha zaidi kusoma katika kazi zilizochapishwa kuhusu makosa, lugha kati, kuathiriwa kwa lugha, ulinganishi wa lugha mbili, na kadhalika (Selinker 1992).

Utafiti huu bila shaka hautajikita kwa moja kati ya hizi njia za ukusanyaji data. Badala yake utatumia zote tatu ili kuweza kufikia data nyingi zaidi itakayotufikisha kwa hitimisho linaloweza kuaminika na kutegemeka maana njia zote tatu zina umuhimu wake kama asemavyo Selinker (1992).

*1.9.1.3.1 Mahojiano*

Tuliwahoji wanafunzi wa shule za upili ili kubaini athari za Kikisa katika Kiswahili na kubainisha athari zinazojitokeza kuanzia shule ya msingi hadi shule za upili. Tuliwahoji wanafunzi wa shule za msingi ili kupata athari hizi zinapoanzia na kuona ikiwa kuna tofauti inayojitokeza wanapoendelea kukua kimasomo na kuingia shule za upili.

Tulitumia mahojiano ya ana kwa ana na wanafunzi wa shule za upili na msingi. Hatukuweza kutumia mahojiano ya aina yoyote nyingine kutokana na sheria za shule nyingi zinazokataa matumizi ya simu shuleni.

*1.9.1.3.2 Hojaji*

Tulitumia hojaji zilizojazwa na watafitiwa kwa ajili ya kubaini ujitokezaji wa uhawilishaji wa fonimu katika maandishi. Hojaji zilitumika pia kubaini uelewa wa dhana zinazojitofautisha kwa fonimu moja iliyo tofauti ya maneno mawili au zaidi. Data iliyopatikana kwenye hojaji ilichanganuliwa na kuwekwa kwenye kategoria zake huku makosa yakibainishwa na kutolewa sababu za ujitokezaji wake. Hojaji ilihusisha kusoma na kuandika. Kupitia usomaji wa maneno katika hojaji, fonimu zinazowatatiza wazungumzaji asilia wa Kikisa wanapozungumza Kiswahili Sanifu ziliweza kudhihirika.

### *1.9.4 Mbinu za Uchanganuzi wa Data*

Tulitathmini kwa kina mahojiano na mijadala kutoka kwa watafitiwa tuliyorekodi ili kutambua ujuzi na umilisi wao wa lugha ya Kiswahili Sanifu na athari za Kikisa kwa utendaji wao. Pia tuliyasikiliza mazungumzo na mijadala tuliyonasa kwa makini na kuyadondoa maneno yanayoashiria athari hizi za Kikisa kwa Kiswahili Sanifu.

Tulilinganisha maneno ya Kiswahili Sanifu yaliyodhamiriwa kutumiwa na yale yaliyowekwa katika nafasi hizo. Tulibainsha maana lengwa zilivyoathirika kutokana na athari za Kikisa kwa maneno hayo ya Kiswahili Sanifu. Tulibainisha athari za makosa tuliyopata ya uhawilishaji wa fonimu kwa uelewa na vilevile mawasiliano.

Tulionyesha mabadiliko ya kifonolojia yanavyotokea katika lahaja ya Kikisa hadi katika Kiswahili Sanifu na hivyo kusababisha mabadiliko ya kisemantiki kiulinganishi kwa kuzingatia mifano ya maneno tuliyoorodhesha kutokana na mahojiano mbalimbali na watafitiwa na katika insha tulizokuwa tumezichambua. Ni kupitia kwa orodha hii ambapo tuliweza kubaini mabadiliko

yaliyotokea yanavyojitokeza na hivyo kuathiri maana za maneno na kisha jumbe husika na hivyo mawasiliano kwa ujumla.

Tulitumia mifanyiko ile mitano ya nadharia ya Lugha Kati kuchanganua na kutambua ni mifanyiko ipi iliyoweza kusababisha mabadiliko mbalimbali ya kifonolojia na kupelekea athari za kisemantiki.

### *1.9.5 Uwasilishaji wa Data*

Kutokana na data iliyopatikana nyanjani, tulichora paichati kuonyesha kila mojawapo ya athari za kisarufi na ambazo ziliathiri maana ili kuonyesha asilimia ya kutokea kwa athari hizo miongoni mwa wanafunzi na watafitiwa tuliowachunguza kwa jumla.

Data yote iliyokusanywa ilipangwa katika makundi kulingana na makosa yake kama vile semantiki, sintaksia, kimofofonolojia na leksia na kuonyesha jinsi makosa hayo yanavyoathiri maana lengwa.

Data iliwasilishwa kwa njia ya kutumia paichati iliyoonyesha asilimia za athari za kimuundo tulizotambua baina ya Kikisa na Kiswahili na athari zake. Sababu yetu ya kuchagua paichati ya asilimia ni kwamba ilituwezesha kuonyesha ni asilimia ngapi ya watafitiwa tuliowachunguza ambao walikuwa na athari mbalimbali tulizozitambua na ni sehemu gani ya muundo wa lugha ya Kiswahili Sanifu iliyoathiriwa zaidi na Kikisa. Hili lililenga kusaidia walimu wa Kiswahili walio wazungumzaji asilia wa Kikisa kuona sehemu za kusisitiza zaidi wakati wa ufunzaji wao wa Kiswahili Sanifu kwa wanafunzi wazungumzaji asilia wa Kikisa. Maelezo ya kinathari yalitumika kufafanua sehemu mbalimbali za paichati iliyotokana na matokeo ya utafiti tuliyopata kutoka nyanjani. Maelezo hayo ni muhimu katika uelewa wa paichati na yalitoa habari zaidi kuhusu data tuliyopata na kile kilichomaanishwa na sehemu hizo.

Asilimia za kila makosa na waliofanya uhawilishaji husika zaidi zilitolewa kufuatana na wazo la Selinker (1992) kuwa, utafiti wa kiuchunguzi unaweza kuhusisha idadi ili kufafanua kikamilifu athari za makosa katika lugha ya pili.

### *1.9.6 Uzingatiaji wa Maadili*

Utafiti huu ulifuata maadili yote ya utafiti. Tuliweza kupata kibali kutoka kwa uongozi wa Chuo Kikuu cha Nairobi, idara ya Kaunti ya Kakamega inayohusika na maswala ya utafiti, na kwa

walimu wakuu wa shule tulizochagua kwa ajili ya utafiti wetu. Watafitiwa waliweza kujulishwa sababu ya utafiti na wakatoa habari kwa hiari. Vilevile, watafitiwa walihakikishiwa kwamba majibu waliyotoa yalikuwa kwa ajili ya utafiti na wala hayangetumika kwingine kokote kwa sababu nyingine yoyote ile.

## Sura ya 2

## Lugha Kati na Uchanganuzi wa Makosa

### 2.1 Utangulizi

Sura hii ni ya kimsingi kuhusu utafiti mzima. Katika sura hii, tunazungumzia masuala ya kimsingi kuhusiana na mada ya utafiti ili yaje yatufae baadaye katika kazi nzima. Sura hii, inazungumzia dhana ya Lugha Kati, Uchanganuzi Makosa, Kikisa kama moja katika lahaja za Kiluhya inayotafitiwa, Kiswahili kama lugha inayojifunzwa, dhana ya Uhawilishaji wa lugha, Uelewanaji, na kuathiriana kwa lugha. Utafiti huu umerejelea wasomi mbalimbali kuhusiana na mada hizi za kimsingi na kisha tukatoa uamuzi kuhusu waliyoyasema kutokana na uelewa wa yale waliyoyasema huku malengo makuu ya utafiti huu yakizingatiwa.

### 2.2 Dhana ya Uchanganuzi Makosa

Mtu anapozungumza kwa athari fulani, wasikilizaji wake hujaribu kukisia usuli wake kijamii na kimaeneo. Pia, mavazi na rangi za watu ni vipengele vingine vya kijamii na kimaeneo viwezavyo kutambulisha watu. Hata hivyo, linalozingatiwa sana ni matumizi yake ya lugha yakiwemo matamshi yake. Utambuzi huu wa lafudhi na mahusiano yake na sehemu au wazungumzaji wa lugha fulani ya kwanza, unadhihirisha uwepo wa athari za kiisimu katika lugha ambazo huhusisha uhamishaji wa vipengele vya kiisimu kutoka kwa lugha chanzi hadi lugha lengwa (Odlin 1989).

Dhana ya uhawilishaji wa fonimu inatofautiana na ukopaji wa fonimu. Ukopaji ni athari za lugha ya pili kwa lugha ya kwanza kama vile Kiswahili Sanifu kwa Kikisa. Uhawilishaji ni athari za kiisimu zinazochunguzwa katika ujifundishaji wa lugha ya pili. Uhawilishaji wa fonimu huhusisha athari za lugha ya kwanza ya mwanafunzi kwa ujifundishaji wa lugha lengwa ambayo huwa ni lugha ya pili bila kujali ni lugha ngapi anazozijua mwanafunzi tayari (Dawkins 1916, Haugen 1953, Weinreich 1953/1968, Schmidt 1985, Thomasson & Kaufman 1988, Odlin 1989). Hata hivyo, si athari zote katika lugha zinazotokana na matapo haya mawili ya ukopaji na uhawilishaji wa fonimu kwa lugha ya pili kwani upo uwezekano wa kujifunza lugha zote mbili kwa pamoja (Taeschner 1983) au hali zote mbili zikajitokeza kwa pamoja (Kaufman 1988).

Kwa muda mrefu ufanyaji wa makosa katika insha ulichukuliwa kama jambo la kawaida (Selinker 1974). Ufanyaji huu wa makosa katika matumizi ya lugha haufanyiki darasani tu bali pia katika mazungumzo na maandishi ya watumizi wa lugha ya Kiswahili Sanifu. Mambo ya kimsingi hapa

ni je, makosa hayo ni ya kimakusudi au la? Makosa hayo yanasababishwa na nini? Ni mapuuza au ni kutojua namna sahihi au bora ya kuzungumza na kutamka maneno?

Mnamo mwaka wa 1984 wasomi takriban 30 walikutana katika Chuo Kikuu cha Edinburgh ili kuzungumzia hali ya Lugha Kati. Jambo mojawapo walilofanikiwa kuliweka wazi ni ubadilishaji wa mtazamo wa dhana ya makosa ya kiisimu kutoka kwa kitu hasi, kinachoonyesha mwanafunzi mvivu na asiyemotishika kujifunza. Walilitazama swala la makosa katika lugha kama kitu cha kawaida na muhimu ambacho kinahitajika katika ujifunzaji lugha, mhimili katika ujifundishaji wa sarufi ya kindani na mkakati wa kujifunza unaohitajika katika ujifunzaji wa lugha (Selinker 1992).

Katika ufundishaji wa lugha ya pili panabainika matatizo makubwa kwa wanafunzi na walimu. Kile kinachobainika wazi ni kuwa hakuna uhusiano wa moja kwa moja wa kinachofunzwa na wanachopokea wanafunzi wa lugha haswa lugha ya pili (Corder 1981). Mtaala unafanyiwa marekebisho na hata wakati mwingine vitabu vinavyotumika kubadilishwa au kulazimishwa kuboreshwa ili kuafiki mabadiliko katika lugha na kulenga zaidi mahitaji ya wanafunzi. Hili bado halisuluhishi makosa yanayofanywa na wanafunzi kwani bado kuna watu waliopitia shule ya msingi na hata shule ya upili ambapo Kiswahili Sanifu ni somo la lazima lakini bado wanaendeleza makosa katika lugha hiyo (rejelea Chepkwony 1993, Onyango 1997, Rapando 2005, Mudhune 2008, Mbula 2011, Gaithuma 2016). Selinker (1992) anaeleza chanzo cha tatizo hili la ujifunzaji wa lugha ya pili kwa kutoa sababu mbili: data au uwasilishaji wake una shida na hata pale data iko sawa, mbinu na vifaa haviwezeshi upokezaji kwa wanafunzi. Hili linaonyesha kuwa mwalimu atakuwa hana udhibiti wa asilimia mia wa ujifunzaji lugha ya pili bali udhibiti wake utakuwa katika mbinu na mikakati iliyowekwa (Pienemann 1989). Mbinu na mikakati hii itawekwa kutokana na tafiti kama hizi za kuchanganua makosa na kutambulisha sababu za ujitokezaji wake.

Wazo la Chomsky (1965) kuwa umilisi wa lugha ni kuujua mfumo mzima wa lugha na utendaji ukiwa kuutumia mfumo huo katika mawasiliano ni wazo la mjadala (Selinker 1992). Swali ni je, kuna uwezekano wa mwanafunzi wa lugha ya pili kuubeba umilisi wake hadi katika lugha ya pili? Na je, kuna uwezekano wa mwanafunzi wa lugha ya pili kufikia umilisi huo wa mzungumzaji mzawa wa lugha husika? Ikiwa mwanafunzi ataweza kuubeba mfumo wote wa kisarufi hadi kwa lugha lengwa itakuwa na maana kuwa umilisi wa kiisimu unaweza kuhamishwa kutoka lugha moja hadi nyingine. Hata hivyo, hili huenda likawa makisio na hisia za mtafiti au mchanganuzi tu na hivyo kuishia kwa hitimisho potovu (Corder 1981, Selinker 1992, Labov 1969).

Selinker (1992) anaongeza maoni yake kuhusu mjadala wa ufundishaji wa lugha ya pili kwa kuchangia kuwa, ili kujua ni vifaa vipi faafu katika ufunzaji wa lugha ni sharti kuchunguza kwa makini uwezekano wa uhawilishaji kwa upande wa mwanafunzi. Anaendelea kusema kuwa ni kupitia kwa uchunguzi huu ambapo tutaweza kutambua uhawilishaji na haswa 'uhamishaji hasi' ambao unahusishwa na kufanya makosa katika lugha ya pili.

Fries (1945) akizungumzia ujifunzaji na ufunzaji wa Kingereza kama lugha ya kigeni anasema kuwa katika kujifunza lugha ya kigeni kuna mambo mawili muhimu ambayo ni hatua ya kwanza na mwisho unaotarajiwa. Mwisho huu unaotarajiwa ni kujenga mazoea ya kuizungumza lugha na uwezo wa kuielewa inapozungumzwa. Fries anafafanua kuwa kufikia mwisho kwa urahisi ni kupitia kuwepo kwa mikakati ya ujifunzaji ambayo ili kupatikana vyema utafiti wa uelewa na uhawilishaji wa vipengele vya lugha ya kwanza vinavyochukuliwa kama makosa katika lugha ya pili vinafaa kutambuliwa (Fries 1945). Njia rahisi ya kuhakikisha ujifunzaji wa lugha ya pili kwa haraka ni kuwa na mikakati ya ufunzaji itakayopelekea mwanafunzi kujifunza mambo yaliyozoeleka katika lugha ya pili inayoweza kumpa msamiati kiasi cha kuweza kuwasiliana (Morley et al 1984, Fries 1945).

Fries na Fries (1961) wanaendeleza msimamo wa Fries kuwa mikakati au vifaa vya ufunzaji ni muhimu katika uelewa wa lugha ya pili. Wanasema:

> Uteuzi mzuri na upangaji bora wa mikakati ya ruwaza na vifaa faafu kwa mahitaji ya kipekee ya wanafunzi kila mwanzoni mwa ufunzaji, kutaamua ikiwa ufunzaji utafanikiwa na ikiwa ujifunzaji utakuwa rahisi au wanafunzi watachanganyikiwa hadi ufundishaji uwe mgumu na ujifundishaji usiwezekane kabisa, (Fries na Fries 1961:1).

Swala la upangaji wa mikakati na vifaa vya ufunzaji linajitokeza pia kupitia Lado (1957). Kwa mujibu wa Lado, jambo la maana katika utayarishaji wa vifaa vya kufunzia ni kulinganisha na kulinganua lugha ya kwanza na ya pili na tamaduni zake ili kubaini 'changamoto' ambazo wanafunzi watapitia katika ujifunzaji. Anaendelea kusema kuwa, ni vigumu hata kuandika mtaala au kitabu cha kuwafunza wanafunzi ikiwa lugha ya kwanza na ya pili hazijachanganuliwa. Hili ni la kimsingi sana na haliwezi kuepukika ikiwa kuna haja ya kupiga hatua katika ufunzaji wa lugha ya pili na kuzibadili njia za awali za ufunzaji ili kurahisisha mchakato huo (Lado, 1957).

Msisitizo unaojitokeza katika kazi hizi unahusu umuhimu wa kufanywa kwa utafiti ili kubaini ni vifaa na mikakati ipi iliyo bora katika ufunzaji wa lugha ya pili kwa wanafunzi. Anavyosema Fries

(1961), kuwa wanafunzi wa lugha ya Kijapani watakuwa na mahitaji yao tofauti na wanafunzi kutoka sehemu nyingine. Hivyo basi, hata ikiwa utafiti umekwisha fanywa katika athari za lugha nyingi za Kenya na Kingereza au hata Kiswahili, ni muhimu kufanya utafiti kwa Kikisa ili kuweza kuelewa mahitaji muhimu ya wanafunzi wa Kikisa katika ujifunzaji wa Kiswahili Sanifu. Hili linatokana na ukweli kuwa hakuna maneno ya lugha moja ambayo huweza kubeba maana ile ile sawa au hata vikoa sawa vya maana na matumizi ya lugha nyingine (Fries 1945). Fries anatoa mfano wa neno *'mesa'* ambalo ndilo neno la *meza* katika Kiswahili Sanifu na '*table'* katika Kingereza. Lakini anasema kuwa neno hili haliwezi kutumika kama linavyotumika katika Kingereza kimaana kwa mfano katika maneno kama vile '*timetable' 'table of figures' table of contents'*. Hali kama hii inaonekana kuwa kweli hata katika Kiswahili Sanifu. Ni muhimu basi kwa utafiti huu kwani msimamo wa kisemantiki uliochukuliwa na utafiti huu utawezesha kutoa maneno na vikoa vyake vya maana na jinsi ubebaji wa vikoa hivyo kutoka Kikisa hadi Kiswahili Sanifu utachukuliwa kama makosa na mfumo usiokubalika.

Utafiti huu unachukulia kuwa, makosa mengi yanayofanywa na wanafunzi na hata watu wanapozungumza katika Kiswahili hasa Wakisa ni kutokana na wao kuwa wanauwililugha. Utafiti huu unachukulia kuwa ikiwa Mkisa angeanza kwa kujifunza Kiswahili Sanifu pekee basi ingekuwa vigumu yeye kufanya makosa kama yaliyobainishwa katika utafiti huu. Hili linatokana na wazo la Lado kuwa makosa mengi ya kiisimu yanayosikika kutoka kwa wanauwililugha yanawiana na tofauti zilizopo baina ya lugha mbili husika (Lado 1957). Hata hivyo, hoja hii inapingwa na Selinker anayedai kuwa licha ya kuwa ujifundishaji lugha ya pili na uwililugha ni mada zinazokaribiana, hazifanani kamwe (Selinker 1992).

Uzungumzaji wa Kiswahili Sanifu kwa athari za lugha ya Kikisa umebainika katika shughuli na hafla anuwai. Kiswahili Sanifu kinatumika kama lingua franka na hivyo kuwa lugha muhimu katika mawasiliano hasa mijini palipo na wazugumzaji wa lugha tofauti za kwanza. Hata hivyo, wazungumzaji wa Kikisa huendelea kutamka fonimu mbalimbali visivyo katika Kiswahili Sanifu. Swali linakuwa ni: je, kwa shida zao za matamshi wanaweza kuelewana na wenzao wasiojua Kikisa? Wengi huelewana hata kama wakati mwingine maana hupotea ama kuchukua muda wa kuulizana kurudia kauli ile ile. Kama inavyobainika katika mahitimisho ya kazi hii ya utafiti, baada ya wazungumzaji hawa kuelewana inakuwa vigumu mzungumzaji wa Kikisa kubadilisha matatizo yake katika makosa anayofanya kwani ukuaji wa ubora wa kuitumia lugha hukoma wakati mahitaji

ya kimawasiliano yanapoafikiwa (Selinker 1992). Ipo haja basi ya kuwarekebisha wanafunzi wa lugha ya pili makosa wanayofanya kabla yawe jambo la kawaida katika uzungumzaji wao. Hii ni kauli iliyoungwa mkono na Nemser (1971) anayesema kuwa ufundishaji wa lugha ya pili kikamilifu una maana ya kuzuia au kuahirisha kwa muda mrefu iwezekanavyo uundaji wa mifumo ya kati na mifumo ya chini kwa mfumo wa lugha lengwa.

Baada ya mjadala huu kuhusu Lugha Kati na Uchanganuzi wa Makosa, sehemu inayofuatia inazungumzia lahaja za Kiluhya ambapo suala la lahaja ya Kikisa limeingizwa ili kutayarisha msomaji kwa kile kitakachosemwa baadaye kuhusu makosa katika Kiswahili Sanifu yajitokezayo katika wazungumzaji walio Wakisa yatakapoangaziwa.

### 2.3 Lahaja za Kiluhya

Kiluhya ni lugha ya Kibantu katika kundi la Benue Kongo tapo la NaijaKongo (Haspelmath, Dryer, & Comrie, 2008). Kimuundo, nomino katika lugha za Kibantu hugawika katika ngeli za majina kuanzia nambari moja hadi 24 (Guthrie 1967, Meeussen 1967, Welmers 1973, Katamba 2006). Hata hivyo, zipo tofauti katika lugha za Kibantu kuhusiana na makundi ngeli haya (Ondondo 2015:12). Kutokana na mabadiliko haya sio ngeli zote 24 zinazopatikana katika lugha zote za Kibantu (Katamba 2006).

Kiluhya kinadaiwa kuwa na lahaja zilizo na lekskosintaksia inayofanana (Wafula na wenzake 2016). Matokeo ya utafiti wa Wafula na wenzake yalidhihirisha kuwa lahaja za Kiluhya ni za mnasaba mmoja kwani zina sifa na vipengele vya kileksia na kisintakisia vinavyofanana. Mpangilio wa maneno wa Kiima, Kitenzi, Yambwa ulijitokeza katika takriban lahaja zote. Pia maneno mengi yalionekana kutokana na mzizi au muundo wa awali mmoja huku tofauti za kimatamshi mara kwa mara zikiwa ni tofauti za kilahaja tu. (Wafula et al, 2016).

Idadi kubwa ya wazungumzaji wa Kiluhya (millioni 5.3) inaufanya utafiti kuhusu athari zake kwa Kiswahili kuwa muhimu kwani huenda idadi hii ikawa na athari kubwa kwa matumizi ya lugha ya wazungumzaji wengi. Pia, kwa kuwarekebisha na kubuni mikakati ya kuwafunza vizuri, athari za lugha ya kwanza zitapunguka kwa wazungumzaji. Wingi wa wazungumzaji wa Kiluhya hawa unaonyesha idadi ya watu ambao wanatangamana na Wakenya wengine kutoka jamii lugha tofauti ambao wanahitajika kuwasiliana ipasavyo na sio tu kwa kutumia lugha kiholela. Athari za

uhawilishaji zinaweza kuwa kizingiti kwa wazungumzaji wengi katika jamii kujieleza ikiwemo hali iliyodumu kwa muda mrefu ya kuhusisha lafudhi na kiwango cha masomo na hadhi ya mzungumzaji.

Utafiti kuhusu Kiswahili na Kikisa, zikiwa lugha za Kibantu, unarahisisha ulinganisho wa mifumo ya lugha hizi mbili. Lugha hizi zinadhihirisha sifa za lugha za Kibantu ambazo zinahitajika kumsaidia mwanafunzi wa Kiswahili Sanifu aliye mzungumzaji asilia wa Kikisa kuelewa kwa urahisi mfumo wa Kiswahili Sanifu. Utafiti huu ulilizamia swala hili ili kujua ni kwa nini wanafunzi wa Kiswahili walio wa Kikisa wanapata matatizo kuzungumza lugha hii na kuiandikia kwa urahisi wakati lugha zote mbili ni za asili ya Kibantu. Ikiwa mifumo ya kileksia na kisintaksia ni sawa kama wanavyosema Wafula na wenzake (2016), utafiti huu umejaribu kutafuta sababu za ni kwa nini kuna matatizo ya kisintaksia miongoni mwa wanafunzi wa Kikisa wanaojifunza Kiswahili Sanifu.

Kuhusu mabadiliko kutokea katika lugha za Kibantu, kama anavyoeleza Ondondo (2015), utafiti huu umeweza kubainisha mabadiliko hayo kwa kutambua tofauti zilizopo kati ya Kiswahili Sanifu na Kikisa na kueleza athari za tofauti hizo kwa ujifunzaji wa lugha ya pili ambayo katika muktadha huu ni Kiswahili.

Lahaja za Kiluhya zina hali ya kufululiza moja ndani ya nyingine. Wafula et al (2016) wanasema kuwa, lahaja za Kiluhya zina mfanano mwingi kileksia na kisintaksia. Maneno na mifumo ya uundaji wa sentensi pia hufanana. Swala la lahaja za Kiluhya kuathiriana linaendelezwa zaidi na Lubangah (2018) katika utafiti wake kuhusu glosia katika lahaja za Kiluhya. Lubangah anasema kuwa ni vigumu kutambua tofauti zilizopo baina ya lahaja hizi zinapoishia kwa mfano mpaka kati ya Kimarama-Lushisa na Kiwanga-Kibukusu. Kwake, Kikisa kinakutana na Kimarama eneo la Bukura ambapo ni vigumu kutofautisha wanaozungumza Kikisa (kutoka Khwisero) na Kimarama (kutoka Butere) hata kwa kuzingatia maneno wanayotumia na maana za maneno hayo.

Lahaja za Kiluhya zinaonyesha mwingiliano mwingi kutokana na ushahidi wa kazi tulizorejelea. Mwingiliano huu unaathiri maneno, leksemu na matumizi ya lugha kwani watu wanapoendelea kutangamana kila mara hujitokeza na jaribio la kutafuta mifumo rahisi ya kuwasiliana ili

kusahilisha mchakato huo. Kwa kufanya hivi, imebainika katika utafiti huu kuwa matatizo yanayowakumba wanafunzi wa lugha ya pili kutoka katika jamiilugha za Kiluhya yanakuwa na mfanano. Kwa kufanya utafiti kwa lahaja moja ya Kiluhya, itakuwa rahisi kwa wazungumzaji wa lahaja nyingine za Kiluhya kupata mengi yanayoweza kuwa kweli kuhusu hali na mchakato wao wa kujifunza lugha ya pili.

### *2.3.1 Kikisa*

Kikisa ni mojawapo ya lahaja za Kiluhya kama tulivyotaja awali. Kikisa kinazungumzwa gatuzi la Kakamega eneo bunge la Khwisero. Ijapokuwa Kikisa hakijatafitiwa na wasomi wengi, kuna wasomi ambao wametaja machache kukihusu kama vile Lubangah (2018) akichunguza glosia na Ondondo (2015), akichunguza mfumo wa kitenzi katika Kikisa. Wasomi wengi kama tulivyotaja awali wametaja Kikisa kwa kupita tu kama lahaja mojawapo ya Kiluhya.

Ondondo (2015) alionyesha ngeli za majina za Kikisa kwa wingi na umoja wake kimofolojia lakini kwa kuhusisha kipengele cha kisemantiki.

| | **Kiambatishi** | **Kiambishi ngeli** | | **Kiambatishi** | **Kiambishi ngeli** |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | o- | MU (Binadamu) | 2. | a- | BA (wingi) |
| 3 | o- | MU (miti, mimea) | 4 | e- | MI (wingi wa 3) |
| 5 a | Ø- | LII- (matunda) | 6 | a- | MA- (wingi wa 5), (vitu majimaji) |
| 5b | e- | LI- | | | |
| 7 | e- | SHI- (nomino za jinsi) | 8 | e- | BI (wingi wa 7) |
| 9a | i- | Ø- (mikopo) | 10a | e- | TSI- (wingi wa 9a) |
| 9b | i- | ny- (haiko wazi) | 10b | Ø- | tsiiny- (wingi wa 9b) |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 9c | i- | ny- (jinsi ya kufanya mambo) | 10c | Ø- | tsiiny- (wingi wa 9c/d) |
| 9d | i- | nz- | 10d | Ø- | tsiinz- |
| 12 | a- | kha- udogoishaji | 13 | o- | ru- (wingi wa 12) |
| 15 | o- | khu- (zisizo na kikomo) | 14 | o- | bu- (za kidhahania) |
| 20 | o- | ku- (za kimajibizano) | | | |

*Chanzo cha Jedwali (Ondondo, 2015).*

Kama anavyoeleza Ondondo (2015) Kikisa kina ngeli za majina zipatazo 16. Ngeli hizi hazijaandikiwa bali zipo wazi katika lugha hiyo kama lugha nyingine za Kibantu. Maneno ya Kikisa huwa na jinsi yanavyotengeneza umoja na wingi wake. Hivyo basi, Kiswahili Sanifu kinapokuwa na ngeli huonekana kuwa ni jambo rahisi kwa mzungumzaji mzawa wa Kikisa kuzungumza Kiswahili na kuzitumia ngeli bila tashwishi. Lakini hili si jambo la moja kwa moja kwani wanafunzi wa Kiswahili walio Wakisa hujipata wakitumia ngeli za Kikisa katika Kiswahili Sanifu. Ngeli za Kikisa hazijiweki kwa makundi kutokana na sifa na misingi ile ile inayotumika katika Kiswahili kuyaweka majina katika makundi ya ngeli. Kwa mfano vitu vilivyo na uhai vinakuwa katika ngeli moja katika Kiswahili Sanifu lakini ngeli tofauti tofauti katika Kikisa.

**2.4 Kiswahili**

Lugha ya Kiswahili Sanifu inagawa nomino zake katika makundi yanayoitwa ngeli za majina yanayopangwa kwa mfumo fulani. Kama lugha nyingine za Kibantu, Kiswahili kina makundi ya kimofolojia yaliyo na sifa za kisemantiki zinazotofautisha ngeli moja kwa nyingine. Kisintaksia ni upatanisho wa kisarufi unaotumika. Ngeli za kimofolojia zinapangwa kulingana na viambishi awali katika nomino na vivumishi vyake (Amidu 2007). Kila kiambishi awali cha ngeli hupewa nambari ya kukitambulisha licha ya kuwa kwa kawaida huwekwa kama jozi la wingi na umoja wake kimofolojia na kisemantiki.

Kiswahili Sanifu huwa na ngeli za majina ambazo huwa na nomino inayosimama kama kichwa cha kishazi na ambayo hudhibiti kila kitu kinachotoa sifa zake (Amidu 2007). Hata hivyo vitambulishi vya ngeli ya 16 hadi 18 PA KU MU havitambuliki kwani ni tofauti katika kawaida ya lugha za Kibantu. Pia, baadhi ya nomino hazichukui viambishi awali. Hata hivyo, nomino hizo zipo katika ngeli hii kinyume na ilivyo katika ngeli nyingine za kimofolojia (Amidu 2007).

Kuzipa kategoria maana ni jambo la kawaida katika lugha zote (Lakoff 1986, Posner 1986, Tversky 1986, Lucy 1992, Amidu 2007). Kiswahili Sanifu kinatoa maana kwa kila kategoria kwa kutumia viambishi kwa ngeli kama vile vya wingi na umoja. Hata hivyo maana za kijinsia hazionekani moja kwa moja katika Kiswahili Sanifu licha ya kuwepo nomino zinazorejelea jinsia katika Kiswahili (Lyons 1968, Amidu 2007). Makundi tofauti ya ngeli huwa na maana tofauti kama vile kundi la kwanza la ngeli na la pili ni ngeli za nomino za vitu vyenye uhai pekee ambavyo havitapatikana tena kwa ngeli nyingine ((Lyons 1968, Hurskainen 1999).

Kwa Kiswahili Sanifu kuwa na sifa zinazowiana na Kikisa inakuwa rahisi kuona jinsi mifumo hii inavyoingiliana na kuwasaidia wanafunzi walio wa Wakisa kujifunza lugha ya Kiswahili kwa urahisi. Kiswahili Sanifu na Kikisa ni lugha ambishi bainishi, zinatumia ngeli ambazo zinafafanua zaidi sifa za nomino na isitoshe, ni lugha za Kibantu. Kwa kupata wanafunzi wakifanya makosa basi, hali hiyo ilihitaji utafiti ili kujua ni sifa zipi au vipengele vipi vya kiisimu vinavyowapeleka katika kukosa kuelewa mfumo wa Kiswahili Sanifu.

Katika sehemu zifuatazo tunazungumzia masuala ya uhawilishaji wa fonimu, uhawilishaji wa mfumo wa lugha, uelewanaji na kuathiriana kwa lugha pamoja na nadharia ya Lugha Kati.

### 2.5 Uhawilishaji wa Fonimu

Fonolojia ni kiwango cha uchanganuzi wa isimu ambacho huchambua mfumo wa sauti katika lugha fulani. Fonimu ni kipashio cha kidhahania cha sauti ambacho huweza kubainisha maana katika maneno (Mweri 2010). Lugha mbili zinapolinganishwa, fafanuzi za fonolojia ya lugha zote mbili, ya kwanza na ya pili, ni muhimu (Briere 1968). Ufafanuzi wa kifonolojia ni muhimu kwani fonimu katika lugha mbili huonyesha sifa za nje na zilizo tofauti zikiwemo sifa za kiakustika na namna ya kuzitamka. Lugha mbili zaweza kuwa na sauti zinazofanana kwa nje lakini zikawa tofauti kiakustika kwa mfano /d/ ya Kingereza na /d/ ya Kiarabu cha Saudi Arabia (Fledge 1980).

Katika utafiti wa sasa kwa mfano, /b/ ya Kiswahili Sanifu ni tofauti kimatamshi na /b/ ya Kikisa kwani ya Kikisa hutamkwa kama /β/.

Utafiti wa Fledge ulionyesha kuwa wanafunzi wa lugha ya pili hutafuta wenyewe namna ya kutamka fonimu za leksemu zilizo karibu na ile ya mfumo wa lugha lengwa. Hata hivyo, ubunifu huu huwa hautoi matamshi yaliyo sawa katika mfumo wa lugha lengwa lakini huwa na ukaribu ambao hauna sifa za lugha ya kwanza au lugha ya pili (Odlin 1989). Katika Kiswahili Sanifu, kuna neno kama vile /mpaka/ ambalo wanafunzi wengine hujipata wakilitamka kama /mbaka/.

Utafiti huu umezichunguza fonimu za Kikisa na Kiswahili Sanifu kwa kujikita kwa zile zinazosababisha utata wa kimaana. Utafiti huu umejaribu kuzichunguza fonimu hizi zinavyobadilishwa kutokana na athari za Kikisa na hivyo kusababisha mabadiliko katika maana ya neno, kueleweka vibaya kwa maana ya neno na vivyo hivyo ujumbe wa msemaji na hata kukatiza mawasiliano kabisa kwa msemaji kutoeleweka kabisa na msikilizaji wake.

### 2.6 Uhawilishaji wa Mfumo wa Lugha

Lewis (1998) anadai kuwa, 'mojawapo ya vigezo muhimu vinavyodhibiti ujifundishaji wa lugha ya pili ni uhawilishaji wa moja kwa moja wa matamshi kutoka lugha ya kwanza'.

Corder (1973) anasema 'wakati watu wanapojifunza lugha ya pili hawapokei lugha maana wanayo tayari'. Kutokana na hali hii, mwanafunzi wa lugha atatumia sheria ambazo tayari zipo na zinajulikana za lugha ya kwanza katika lugha ya pili. Iwapo mwanafunzi hataweza kuziona tofauti zilizopo katika sheria hizi basi atazitumia sheria anazozijua tayari za lugha ya kwanza katika lugha ya pili. Hili ndilo linalojulikana kama uhawilishaji; yaani, pale mwanafunzi anapohawilisha kile anachojua kukitamka hadi katika lugha nyingine.

Corder (1973) anagawanya dhana ya uhawilishaji katika matapo mawili: uhawilishaji hasi au athari mbaya (kufanya makosa katika lugha ya pili) na uhawilishaji chanya au uwezeshaji (pale sheria za lugha ya kwanza na ya pili zinafanana).

Utafiti huu umezingatia matapo yote mawili yaani umeonyesha sifa za Kikisa zinazofanana na za Kiswahili Sanifu na hivyo kuwawezesha wanafunzi kujifunza kwa urahisi mifumo ya Kiswahili Sanifu. Lugha hizi zimelinganishwa pia ili kupata tofauti zinazowapa wanafunzi matatizo katika mchakato wa kujifunza lugha ya pili. Makosa yaliyopatikana kufanywa na wanafunzi katika

Kiswahili Sanifu yalichukuliwa kama athari za mfumo waliokwisha kupokea wanafunzi wa lugha ya kwanza kama anavyoeleza Corder (1973).

### *2.6.1 Uelewanaji*

Major & Kim (1996) wanasema kuwa 'tafiti nyingi zinaonyesha kuwa watu wanaojifunza lugha ya pili huwa na ugumu wa kufikia ubora wa kiwango cha mzungumzaji mzawa wa lugha husika'. Idadi kubwa ya wanafunzi wa lugha ya pili huenda wasifikie kiwango cha juu cha matamshi kinachoweza kufananishwa na kile cha wazungumzaji wazawa. Ikiwa kiwango cha ubora wa matamshi wa mzungumzaji wa lugha husika kama lugha ya pili si sawa na ule wa mzungumzaji wa lugha hiyo kama lugha ya kwanza yeye husemekana kuwa ana lafudhi. Hata ingawa kulingana na tafiti hizo mzungumzaji wa lugha kama lugha ya pili hawezi kutamka fonimu kwa ubora kama wa lugha ya kwanza mzungumzaji wa lugha ya pili anahitajika kutamka maneno kwa namna itakayoeleweka na mzungumzaji mzawa.

Athari za lugha ya kwanza ya mzungumzaji kwa lugha ya pili huzua kile kinachoitwa uhawilishaji wa lugha ambao waweza kuwa hasi au chanya na hivyo kusababisha maudhi, kukinai, uchoshi au zaidi kutoelewana (Haasbroek & Van Wyk, 1996). Mzungumzaji anapokuwa na lafudhi nzito sana inafanya usemi wake usieleweke ambapo maana ya kuzungumza hupotea kwani nia kuu ni mawasiliano. Utafiti huu umejaribu kubaini makosa ya wanafunzi wa Kiswahili Sanifu walio wazungumzaji asilia wa Kikisa ili kujaribu kupendekeza mbinu za kupunguza athari hasi za uhawilishaji kwa Kiswahili Sanifu. Hata ingawa ni vigumu kufikia kiwango cha mzungumzaji mzawa, utafiti huu unanuia kubaini mikakati ya kupunguza mwanya baina ya mzungumzaji wa lugha ya Kiswahili Sanifu kama lugha ya pili na mzungumzaji mzawa ambao unahitajika kuanzia katika ufundishaji wa lugha hiyo shuleni.

## 2.7 Kuathiriwa kwa Lugha

Kuathiriwa kwa lugha kiisimu kunatokana na 'wakati mifumo miwili inatumiwa kwa pamoja kwa kipengele cha ya isimu' (Haugen 1953). Utafiti katika kuathiriwa au kuingiliwa kwa lugha huwa na umuhimu katika kufafanua fenomena ya mitagusano ya lugha na hutoa mambo muhimu katika mchakato wa ujifundishaji wa lugha ya pili (Gergely 2007).

Debysers (1970) anafafanua uhawilishaji lugha (kuathiriwa chanya) kama kuathiriwa ambako kunatumia mambo yaliyo sawa baina ya elementi za lugha ya kwanza na lugha ya pili na hivyo

kufanya mchakato wa ujifunzaji lugha kuwa rahisi. Kuathiriwa hasi kwa upande mwingine, ni utumiaji wa miundo isiyokubalika kutoka kwa lugha ya kwanza hadi lugha ya pili. Weinreich anafafanua kuathiriwa (kihasi) kwa lugha kwa kueleza kuwa:

> Matatizo ya athari za kifonolojia yanahusisha namna mzungumzaji anavyochukulia na kuzalisha fonimu za lugha moja ambazo zinaweza kuwa zimewekwa kimahsusi kama za lugha ya pili, kwa misingi ya nyingine, kuitwa fonimu za lugha ya kwanza. Kuathiriwa kunatokea wakati mwanauwililugha anapotambua fonimu ya mfumo wa lugha ya pili na katika kuitamka, anaiwekea sheria za kifonolojia za lugha ya kwanza. Weinreich (1953:14)

Fafanuzi hii ni muhimu katika utafiti huu. Wanafunzi wa Kiswahili Sanifu watokanao na jamii lugha ya Kikisa hujifunza kwanza fonimu za lugha hiyo na kisha kutamka kwa kuweka fonimu za Kikisa. Hii ndiyo sababu inayoweza kueleza hali inayojitokeza mara nyingi ambapo kuna watu wanaoandika vizuri sana katika Kiswahili Sanifu lakini ubora wao kimaandishi haujitokezi katika matamshi yao wanapozungumza. Kwa kusoma kazi zao wataeleweka vizuri kuliko wanapozungumza. Hata hivyo, idadi kubwa ya mawasiliano haiwezi kuwa kimaandishi pekee. Mengi ya mawasiliano ya kawaida hayahusishi kuandika bali kuzungumza na hivyo athari hasi hupata nafasi ya kujitokeza na kutoa mchango wake katika kueleweka au kutoeleweka kwa mzungumzaji.

Tunapozungumzia athari zinazotokana na mtagusano kati ya mifumo miwili ya kifonolojia, Weinreich (1953) anatofautisha aina nne za kimsingi:

a) *Kutofautisha kwa hali ya chini kwa fonimu*: Hutokea wakati fonimu mbili za mifumo ya lugha ya pili ambazo fonimu lingani katika mfumo wa kimsingi hazijatofautishwa huchanganywa.

b) *Kutofautisha kwa hali ya juu kwa fonimu*: Huhusisha ulazimishaji wa tofauti za kifonolojia kutoka kwa mfumo wa lugha ya kwanza kwa fonimu za mfumo wa lugha ya pili, pale ambapo hazihitajiki.

c) *Kufafanua tena tofauti zilizopo*: Hutokea wakati mwanauwililugha anapotofautisha fonimu za mfumo wa lugha ya pili kwa sifa ambazo katika mfumo huo ni za pamoja na hazihitajiki, lakini ambazo ni muhimu katika mfumo wa kimsingi.

d) *Kubadilisha fonimu*: Huhusisha fonimu ambazo zinafanana kabisa katika lugha zote mbili lakini ambazo kutamkwa kwazo kwa kawaida kunatofautiana.

Utafiti huu umetumia ulinganishaji wa mifumo ya Kiswahili Sanifu na Kikisa ili kutambua fonimu zake zinazosababisha utata kwa kutumika kupitia michakato iliyoorodheshwa na Weinreich (1953) yaani kutofautisha kwa hali ya juu, hali ya chini, kufafanua tena na kubadili fonimu.

### 2.8 Uchanganuzi wa Makosa

Uchanganuzi wa makosa ni swala muhimu katika mjadala wa kujifunza lugha ya pili. Kutokana na ukweli huu, uchanganuzi wa makosa umekuwa swala zito miongoni mwa wasomi na haswa wanaisimu (Wedell & Liu, 2012). Ukuaji na maendelezo ya swala hili la uchanganuzi wa makosa si wa kitambo sana lakini ukuaji wa dhana hii ni wa haraka sana huku kukishuhudiwa ongezeko la wasomi wanaolitafitia swala hili kwa kutumia vifaa mbalimbali na maarifa kuongezwa katika uwanja huu kila uchao. Kufikia sasa, matokeo ya utafiti kuhusu uchanganuzi wa makosa yanaendelea kutokea katika nyanja tofautitofauti (Widdowson, 2013).

Uchanganuzi wa makosa huwezesha ubainishaji, ufafanuzi na utabiri wa ruwaza tatanishi na zenye changamoto katika kujifunza kwa lugha ya pili na zile ambazo hazitakuwa matatizo (Lado 1957). Hata hivyo, swala la kutabiri makosa, matatizo, changamoto, athari au uingiliaji na vizingiti katika ufunzaji na ujifunzaji wa lugha ya pili linapingwa vikali na Selinker (1992). Lakini, kupinga kwa Selinker hakuna maana kuwa hili haliwezi kuafikiwa kupitia kuelewa uhawilishaji bali ana tatizo na utoaji wa kauli hii kama kauli ya mwisho, kuwa hakuna swala la uwezekano na wakati mwingine kuwepo kwa njia mbadala. Kuhusu kubaini changamoto na matatizo ya wanafunzi wa lugha ya pili, Weinreich anaongeza kuwa kwa kutathmini mifumo yote miwili ya lugha husika na kupata tofauti zake, mtafiti anapata sehemu ambazo kuna urahisi wa kupata athari za lugha ya kwanza kwa lugha ya pili (Weinreich 1953, Lado 1957).

Kwa wanaisimuhistoria, uchunguzi wa makosa unaweza kuwasaidia kupata ufahamu kuhusu uhusiano kati ya mtagusano wa lugha na ubadilikaji wa lugha. Hili linatokana na ukweli kuwa licha ya kuwepo kwa sababu nyingi zinazosababisha kubadilika kwa lugha, uwililugha una nafasi kubwa katika mchakato huu. Hili linawezesha kupata hali ya mchakato mzima wa ujifundishaji wa lugha ya pili na nadharia zake (Conrie 1984, Odlin 1989).

Ujuzi wa historia ya kiisimu na kitamaduni ya mwanafunzi wa lugha ya pili ni muhimu katika kufanikisha mawasiliano ya ujifundishaji wa lugha hiyo ya pili. Hata hivyo, uchanganuzi wa makosa yanayofanywa na wanafunzi wa hali za awali mbalimbali pia kwaweza kuwa muhimu katika kutathmini sehemu ngumu na rahisi kuelewa (Odlin 1989).

Ujifundishaji wa lugha ya pili ni mchakato wa kuboresha lugha ya pili ya mwanafunzi au kuimarisha uwezo wake katika lugha ngeni. Hili ni tofauti na upataji wa lugha ya kwanza (Hu, 1998). Upataji wa lugha hivyo basi, ni mchakato wa kupata maarifa ya kisaikolojia, kiakili, na kiisimu katika lugha ya kwanza (Lightbown, 1983). Uchanganuzi wa lugha zote mbili, unawezesha kubaini mchakato wa upataji lugha ya kwanza unavyotofautiana na ule wa kujifunza lugha ya pili na hivyo kutambua chanzo cha changamoto za ujifunzaji wa lugha ya pili.

Uchunguzi wa mchakato wa ujifundishaji wa lugha ya pili unalenga matarajio ya kupata kitu cha manufaa kwa ufundishaji na ujifundishaji wa lugha ili kuboresha ufanisi wa upokeaji wa lugha ya pili (Ellis, 2012). Watafiti wengi hutazama uchanganuzi wa makosa kama njia iliyo bora, ya ufanisi mno na kiingilio katika uchunguzi wa ujifundishaji wa lugha ya pili (Ellis, 2012).

Lado (1957) alidai kuwa kuelewa swala hili la uhawilishaji wa lugha kutampa mwalimu wa lugha kupata vifaa kamili vya kufunzia na kuweza kupata matatizo ya wanafunzi kikamilifu. Hata hivyo, anajichanganya na kusema pia kuwa wanafunzi wana tofauti zao za kibinafsi. Jambo hili linapingwa na Selinker kwani ikiwa wanafunzi wa lugha ya pili wana matatizo ya kibinafsi basi huenda tulichokiweza si kutatua matatizo yao yote kikamilifu bali matatizo yao makubwa katika ujifunzaji wa lugha ya pili (Selinker 1992).

Uchanganuzi wa makosa katika lugha kati unachukuliwa kama kifaa chenye ufanisi katika utafiti wa upataji wa lugha ya kwanza (Selinker, 1972). Hii ni kwa sababu wakati wa ujufunzaji wa lugha ya pili, mwanafunzi hujipata aghalabu kwa hali ya kurejelea dhana na misamiati ya lugha zote mbili hivyo basi kuifanya Lugha Kati kuonekana kama hatua tu katika ujifunzaji wa lugha ya pili ambayo baadaye hupotea mwanafunzi anapopata umilisi au udhibiti mzuri wa lugha ya pili.

Uelewa wa sababu za makosa yanayotokea, uchanganuzi wa makosa na urekebishaji kwa muda ufaao wa yaliyomo katika ufundishaji na mbinu au njia za ufundishaji ni mambo muhimu yanayowezeshwa na utafiti wa upataji wa lugha ya pili (Tarone, 2012). Uelewa huu waweza

kumsaidia mwalimu na watengenezaji wa mitaala kubuni mada, maudhui na mbinu mwafaka na faafu zitakazorahisisha kujifunza na kueleweka kwa lugha ya pili.

Uchunguzi wa ujifundishaji wa lugha ya pili sio tu wa kimaelezo na wa kupata tajriba au wa maelezo ya kihali bali pia unafaa kuwa wa kisayansi kupitia uchanganuzi wa kiidadi (Richards & Rodgers, 2013). Kupitia kwa mchakato kama huo, utafiti unaofafanua kwa kina kuhusu maswala yote kiutaratibu unaweza kupatikana katika muktadha wa wanafunzi wanaojifunza lugha ya pili na matokeo yao wanapotathminiwa. Kupitia uchunguzi na uchanganuzi wa hali ya ujifundishaji wa lugha ya pili na kwa kutumia mfumo wa ujifundishaji wa lugha ya pili kisayansi, tunaweza kubaini kile wanafunzi wa lugha ya pili wanachofunzwa na kile wanachotoa kama matokeo ya tathmini. Hili laweza kusaidia kuimarisha ufundishaji na upokeaji wa lugha ya pili (Cortazzi & Jin, 1996).

Ellis (1994) anataja manufaa matatu ya kubaini makosa ya wanafunzi wa lugha ya pili. Humsaidia mwalimu kujua yale wanafunzi wameelewa, humpa mwalimu uelewa wa namna lugha ya pili inavyopokezwa kwa wanafunzi na ni njia ambayo wanafunzi hujifunza sheria na kanuni za lugha lengwa.

Kupitia kwa uchanganuzi wa makosa wanafunzi wa lugha ya pili wataweza kubaini ikiwa wanafanikiwa au la katika kujifunza kwao lugha ya pili. Wanafunzi wa lugha ya pili wataweza kutathmini ufaafu wa mbinu zao za ujifunzaji na kasi yao. Hili litawasaidia kujua ni wapi watakaposisitiza zaidi na kuwa makini zaidi (Corder, 1967).

Uchanganuzi wa makosa pia ni njia isiyoweza kutupiliwa mbali kama msaada wa walimu wengi wa lugha za kigeni (Widdowson, 2013). Uchanganuzi wa makosa yanayofanywa na wanafunzi wa lugha ya pili utamsaidia mwalimu kujua jinsi ya kuboresha mikakati yake na mbinu za ufundishaji na hivyo kuboresha ufundishaji wa lugha za pili na za kigeni (Wedell & Liu, 2012).

Uchanganuzi wa makosa huhusisha nadharia za ufundishaji wa lugha ya kigeni ambapo mwanafunzi ndiye msingi wa mchakato mzima. Hili linaweza kuwasaidia wanafunzi kuhamisha fikra zao kutoka kwa mambo ya kiinje yanayowaathiri na kuwafanya warudishe makini yao kwa wao wenyewe na hivyo kupata uelewa wa ndani zaidi wa wao wenyewe kwa sababu makosa mengi yanatokea kwa sababu ya wao kuikabili lugha kwa misimamo na mitazamo yao (Jiang, 1999).

Makosa yanahitaji kuchanganuliwa ili mwelekeo faafu upewe wanafunzi wa lugha ya pili. Ukosefu wa ushauri wa kutosha kwa wanafunzi wa lugha ya pili unaweza kuwa kizingiti cha kuelewa lugha ya pili na wakati mwingine kuzua mielekeo hasi kuihusu lugha husika. Athari za lugha ya kwanza zinaweza kusababisha ukuaji wa lugha kati bila lugha kati hiyo kuimarika kuwa na sifa za lugha lengwa. Hali iwapo hivi, inaweza kusababisha kubadilika kwa lugha. Hii ndiyo sababu kuathiriana kwa lugha kunatafitiwa kama nyanja muhimu (Selinker 1992, Trudgill 1986)

Makosa yanapotambuliwa, fafanuliwa, elezwa na kutathminiwa, uchanganuzi wa makosa utaonyesha aina, mifumo na taratibu za wanafunzi wa lugha ya pili ili kuweza kutambua kwa uwazi ni kwa nini na vipi wanafanya makosa hayo na kubuni mikakati ya kuepuka (Kleinmann, 1977).

### *2.8.1 Umuhimu wa Makosa*

i) Makosa ni mfumo wa hali ya juu zaidi, ufunguo wa uendelezaji wa lugha ya pili wa mwanafunzi (Corder 1967, Corder 1981, Selinker 1992).

ii) Makosa kwa mwanafunzi wa lugha ya pili hayaepukiki kwani ni mkakati ambao mwanafunzi anatumia kujifunza. Ufanyaji huu wa makosa ni mkakati au mbinu inayotumiwa hata na watoto wadogo wanapojifunza lugha ya mama na kwa wale wanaojifunza lugha ya pili, ni njia ya mwanafunzi kujaribu haipothesia yake kuhusu muundo wa lugha anayojifundisha (Selinker 1992, Corder 1967, Corder 1981).

iii) Uchanganuzi wa makosa na ufafanuzi wake wa kina unasaidia kupata makosa ambayo ni chanzo muhimu sana katika kupata habari na ufahamu kuhusu ukuaji wa kiisimu wa mwanafunzi wa lugha (Corder 1972, Corder 1981, Selinker 1992).

iv) Tathmini ya mara kwa mara ya makosa ya kisarufi wanayofanya wanafunzi wa lugha husaidia kutambua athari za kutagusana na kutangamana na data nyingine katika ‘ hali yake ya kisarufi‘ (Corder 1981, Selinker 1992).

v) Uchanganuzi wa makosa katika lugha moja kwa kuzingatia lugha nyingine ni njia mojawapo ya kutoa habari zaidi kuhusu mifumo ya lugha zote mbili. Ni kuitazama lugha moja kwa kurejelea lugha nyingine (Corder 1981, Selinker 1992)

vi) Katika ujifunzaji na kufunza lugha hii, uchunguzi wa makosa utasaida kuteua, kupanga na kuratibu vifaa na mikakati ya hali ya ufundishaji. Uchunguzi wa uhawilishaji wa lugha na dhana ya Lugha Kati utawawezesha walimu na wanaobuni mitaala ya elimu kuweka mipangilio bora ya mandhari ya ujifunzaji lugha haswa lugha ya pili, mbinu na mikakati ya ujifunzaji na ufundishaji, jinsi ya kuwapa motisha wanafunzi kujifunza lugha ya pili, kufanya maamuzi bora kuhusu ufundishaji, (Fries 1945, Lado 1957, Corder 1981, Widdowson 1984, Faerch 1984, Selinker 1992).

vii) Uchanganuzi na uchunguzi wa makosa unasaidia kuonyesha tofauti iliyopo kati ya kile kinachofunzwa kwa wanafunzi na kile wanachopokea kutoka kwa ufundishaji huo.Utumiaji wa lugha na uteuzi wa lugha inayoafiki miktadha utaweza kuonekana (Corder 1967). Tofauti kati ya wanachofunzwa wanafunzi, wanachopokea na wanachotoa ni muhimu kutathminiwa (Gass & Madden 1985). Corder anafafanua kuwa, kinachopokelewa na mwanafunzi si sawa na kile kinachowasilishwa hivyo basi huenda mwanafunzi akawa muhimu katika kudhibiti anachopokea. Atakachopokea mwanafunzi kitabainishwa na mikakati na mbinu za kumpokeza na wala si uundaji wa mtaala ulio na kila kitu anachohitaji kujua (Tarone 1976, Corder 1981).

Utafiti huu umenufaika pakubwa na mawazo haya ya Corder na wenzake. Mawazo ya Corder yamewezesha utafiti huu kutathmini sio tu makosa yanayofanywa na wanafunzi bali pia kuchunguza sababu zake. Mawazo ya Corder yametusaidia kutathmini sio tu sababu za kiuanafunzi au za Kikisa zinazowezesha utokeaji wa makosa bali pia kutathmini mikakati ya ufundishaji na ujifundishaji. Utafiti huu umelitathmini swala la uwezekano wa walimu kuwa na athari za lugha ya kwanza ambazo zinaweza kupitishwa kwa wanafunzi wa lugha ya pili ambayo katika muktadha huu ni Kiswahili Sanifu.

### *2.8.2 Tofauti Kati ya Makosa ya Kushtukia na ya Ujifundishaji wa Lugha ya Pili*

Ni muhimu kutofautisha kati ya makosa yanayofanyika kwa kawaida na yale yanayosababishwa na athari za lugha ya kwanza kwa lugha ya pili. Hili si jambo rahisi la kufanya maana ni vigumu kujua mtu anapozungumza kwa mara ya kwanza ikiwa kuna uwezekano kuwa yeye huzungumza hivyo kila mara au ni wakati huo tu. Aghalabu yote hukubaliwa kama makosa bila utafiti wowote kufanywa ili kuchunguza ikiwa ni kutokana na athari za lugha ya kwanza kwa lugha ya pili. Katika insha kwa mfano mwanafunzi anapofanya kosa moja tu kwa insha yote huenda ana shida katika matumizi ya fonimu hiyo. Hata hivyo, kutambua ikiwa ni kushtukia tu au ni athari za lugha ya kwanza kwa lugha ya pili itakuwa vigumu. Watafiti wengine wametofautisha kwa kutumia neno

‘*sahau*‘ na ‘*kosa*‘. Hata hivyo, kubadili istlahi inayotumika kueleza makosa si suluhu la utata uliopo (Selinker 1974, Tarone 1979, Tarone 2011).

Katika mtazamo wa upataji wa lugha ya pili neno *sahau* na *kosa* ni dhana mbili tofauti (Ellis, 2012). Kusahau ni swala la kosa katika utendaji zaidi ambapo msemaji anaweza kujipata ndani kiajali kutokana na ulimi kuteleza, kuchoka au hata kutotilia maanani utendaji wake kunakosababisha uwezo wake wa kiutendaji kurudi chini (Ellis, 2012). Wakati huo utapata wanafunzi kama hawa wamekosa kutumia umilisi wao wa awali ipasavyo na hivyo kufanya makosa ambapo hawangeyafanya makosa hayo kwani wana umilisi ufaao kuitumia lugha hiyo kikamilifu.

Tukilitazama suala hili kwa misingi hii, inadhihirika kuwa, mtu yeyote anaweza kufanya makosa bila kujali ikiwa atakuwa anazungumza lugha yake ya kwanza (lugha ya mama) au lugha ya kigeni (Tarone, Bigelow, & Hansen, 2013). Hili lina maana kuwa kuteleza kwa ulimi na kufanya makosa ya kisarufi katika lugha wakati mwingine hakusababishwi na ukosefu wa umilisi au maarifa ya kutumia lugha husika bali mambo mengine huweza kutendeka kama vile kutokuwa na udhibiti wa lugha kwa muda mfupi kutokana na mambo kama upuuzi wa sheria fulani wakati wa kutumia lugha (Tarone & Liu, 1995). Haya basi ndiyo makosa ya kusahau (Cheng 2015).

Katika mchakato wa upataji wa lugha ya pili, wanafunzi huwa na mazoea ya kukwepa au kuanza sheria tofauti za matumizi ya mfumo wa lugha lengwa. Ukwepaji na uundaji huu wa sheria na mifumo mbadala hutokana na ukosefu wa umilisi wa mfumo sahihi wa lugha lengwa. Makosa kama haya wakati mwingine huwa si ya moja kwa moja kwa mzungumzaji kurekebisha hata wakati yamekwisha fafanuliwa (Ellis, 2012).

Mwanafunzi anaporudia makosa yale yale ambayo yanaonyesha ruwaza fulani kwa mfano kifonimu, huenda hapo kuna makosa yanayotokana na athari za lugha ya kwanza. Mwanafunzi husika anapohawilisha mfumo wa lugha nyingine kwa lugha lengwa basi hapo kuna athari. Hali hii hurejelewa kama makosa kutokana na athari za lugha ya kwanza kwa lugha ya pili. Haya ni makosa katika ujifundishaji wa lugha ya pili. Kulingana na Corder (1967), makosa ya ukwepaji wa mfumo katika kujifunza lugha ya pili kwa mwanafunzi huwa ni makosa ya athari za lugha ya kwanza kwa lugha lengwa.

Kile kinachojitokeza katika mjadala huu ni kuwa, tofauti kati ya makosa ya kushtukia na yale ya kiathari kutoka kwa lugha ya kwanza ni finyu kiutambuzi. Hata hivyo, kwa kufuatilia fonimu fulani kila zinapotokea tunaweza kujua fonimu zinazompa mwanafunzi wa lugha ya pili changamoto na zile alizokosea tu. Makosa yanayojitokeza kwa mara moja tu na yakarekebika katika sehemu nyingine huenda yasitoe habari kamili kuhusu athari za lugha ya kwanza kwa ujifundishaji wa lugha ya pili. Hata hivyo, ili athari isemekane kutoka kwa lugha ya kwanza, ni sharti sifa hiyo ipatikane katika lugha ya kwanza na ijitokeze katika lugha ya pili kama mfumo usiokubalika.

### *2.8.3 Aina za Makosa*

Makosa yanayofanywa na wanafunzi wa lugha ya pili yanaweza kuchanganuliwa na kisha matokeo ya uchanganuzi huo yakasaidia kuelewa vizuri chanzo cha makosa na sababu za makosa anuwai ili kufikia lengo kuu la kuwarekebisha wanafunzi ili kuimarisha ubora wa mchakato wa upokeaji wa lugha ya pili au ya kigeni (Cheng 2015).

Burt & Kiparsky (1972), wanasema makosa ya wanafunzi wa lugha ya kigeni huweza kugawika katika matapo mawili mapana:

(1) makosa changamano ambayo hujitokeza katika muundo muhimu wa sentensi na huathiri uelewa wa anayejifundisha sentensi na mawasiliano ya kawaida.

(2) makosa ya kawaida ambayo hutokea katika miundo ya lugha ya pili ya sentensi na haiathiri uelewa au kuwa kizingiti cha mawasiliano licha ya sentensi kutokuwa sawa kimuundo.

Aina nyingine za makosa yanaweza kuwekwa pamoja kwa kutumia kigezo cha wazi na isiyowazi (Corder, 1981):

a) Makosa yaliyo wazi ni yale ambayo mwanafunzi anavunja kanuni za kisarufi za lugha lengwa kama vile kanuni za kimofolojia na kisintaksia za lugha lengwa.

b) Makosa yasiyo-wazi ni yale yanayoonyesha kuwa kauli za mwanafunzi ambazo ziko sawa katika sarufi ya lugha lengwa hazitoi maana yoyote muktadha wa matumizi unapochanganuliwa (Celce-Murcia & Hawkins, 1985). Hapa, sentensi yaweza kuwa na makosa lakini isionyeshe dalili yoyote ya nje ya makosa hayo. Sentensi inaweza kuwa imejengwa kwa viambajengo sahihi kikamilifu lakini iwe na makosa kimuktadha (Corder

1981). Ukosefu wa makosa ya nje ya sentensi si thibitisho la kutosha kuwa sentensi hiyo ni sahihi. Hivyo basi, sentensi zinahitajika sio tu kuwa sahihi kisarufi lakini pia kisemantiki na kwa muktadha faafu (Corder 1981).

Selinker (1992) anataja aina mbili za makosa:

a) makosa ya kinasibu yenye ruwaza fulani (sawa na makosa yaliyo wazi ya Corder 1981).

b) makosa yasiyo hasi na pia hayaathiri ujifundishaji wa lugha ya pili. Makosa haya huishia kuwa kigezo muhimu katika ukadiriaji wa haipothesia alivyotaja Corder (1967).

Aina hizi za makosa zinadhihirisha utata uliopo katika ubainishaji wa makosa. Hata hivyo, zinatoa makundi ya kijumla zaidi yanayoweza kutumika kueleza makosa kwa urahisi. Kuna haja, hata hivyo, ya kupata makundi madogo zaidi ya kugawa makosa haya ili kuwezesha utambuzi wa haraka wa makosa na kuepuka utata.

Aina hizi za makosa zimejitokeza wazi na pia kwa njia isiyo wazi katika utafiti huu. Kwa kuangazia kipengele cha kisemantiki maneno au fungu la maneno linaonekana sahihi kisarufi lakini halina maana katika lugha Kiswahili Sanifu na hivyo kutofanikisha mawasiliano. Makosa mengine ya wazi yamebainishwa haswa ya kisarufi na fonimu zinazobadilishwa kimakosa na hivyo kubadili maana ya neno, kauli au sentensi.

### *2.8.4 Kategoria za Makosa*

Kategoria zifuatazo zinaonyesha athari anuwai ambazo mlinganisho na mlinganuo wa kiisimu unaweza kudhihirisha (Odlin 1989):

### *2.8.5 Uhawilishaji Chanya*

Athari chanya huweza kubainishwa tu kupitia kulinganisha ufanisi wa lugha ya pili kwa wanafunzi wa lugha tofauti za kwanza. Mfanano katika msamiati wa lugha ya kwanza na lugha ya pili kunaweza kupunguza muda wa kusoma na kuelewa matini au ufahamu. Mfanano wa mifumo ya vokali yaweza kufanya rahisi mchakato wa kutambua vokali katika lugha ya pili. Mfanano katika namna ya kuandika waweza kuwapa wanafunzi wa lugha ya pili urahisi wa kuanza kusoma na kuandika katika lugha lengwa. Mfanano katika taratibu za kisintaksia waweza kuwezesha upokeaji wa sarufi ya lugha lengwa maana watakuwa na urahisi wa kuelewa viunganishi na vibainishi, mfuatano wa maneno na vishazi tegemezi.

Kwa msingi kuwa lugha hizi mbili ni za asili ya Kibantu, ni kweli kuwa si kila mara lugha ya Kikisa inaleta athari mbaya kwa Kiswahili Sanifu. Ipo nafasi ya Kikisa kama lugha ya kwanza kuwasaidia wanafunzi kuelewa Kiswahili Sanifu. Corder (1967) anasema kuwa lugha ya kwanza si hasi na yenye athari hasi tu kwa lugha ya pili. Kuitazama lugha ya kwanza kwa mtazamo huu ni kosa kubwa. Uwepo wa lugha ya kwanza kwa mwanafunzi ni jambo la kusaidia ujifunzaji wa lugha ya pili (Selinker 1992, Corder 1983). Ni kweli basi kuwa, lugha ya kwanza humsaidia mwanafunzi kupata urahisi wa kuunda Lugha Kati na kupata kwa urahisi vipengele vinavyofanana katika lugha zote mbili ambavyo inakuwa rahisi kuvielewa. Lugha ya Kiswahili na Kikisa ni lugha za Kibantu na hivyo zinafanana katika vipengele na sifa mbalimbali za kiisimu. Kwa mfano, lugha zote mbili zikiwa lugha za Kibantu zinazingatia ngeli za majina ambazo hutoa ujumbe zaidi kuhusu nomino husika kama vile kundi, umoja, wingi, ukubwa na udogo. Hali hii inaleta urahisi kwa mzungumzaji wa Kikisa kama lugha ya kwanza anapojifundisha Kiswahili Sanifu. Muundo wa kimofofonolojia wa KV pia ni mfano mzuri wa kipengele cha kiisimu kinachoweza kuwa rahisi kwa mzungumzaji wa Kikisa anapojifundisha Kiswahili Sanifu kwani lugha zote mbili zina mfumo wa KV.

### *2.8.6 Uhawilishaji Hasi*

Aina hii ni rahisi kugundua kwa sababu huhusisha makosa katika lugha lengwa. Licha ya kuwa uhawilishaji hasi huonekana kama utoaji wa makosa pekee, ruwaza zake hujitokeza katika namna mbalimbali:

#### *2.8.6.1 Uzalishaji wa Chini*

Wanafunzi wa lugha ya pili wanaweza kujipata katika hali ambapo wana uwezo wa kutoa mifano michache au hata kutotoa mfano wowote wa mfumo wa lugha lengwa. Mifano michache wanayotoa wanafunzi wa lugha ya pili yaweza kuwa na makosa machache yanayoweza kulinganishwa katika lugha hizo. Hata hivyo, ikiwa tofauti ni kubwa sana wanafunzi wanakuwa mbali sana na mfumo unaokubalika. Ikiwa mifumo ya lugha lengwa ni tofauti sana na ya lugha ya kwanza wanafunzi huwa na mazoea ya kujiepusha na mifumo hiyo (Odlin 1981, Schachter 1974, Kleinmann 1977).

#### *2.8.6.2 Uzalishaji wa Juu*

Uzalishaji juu ni tokeo la uzalishaji chini. Kwa kujaribu kuepuka mifumo isiyo ya kawaida kwao, wanafunzi wa lugha ya pili hujipata wakitumia mfumo mmoja kwa wingi.

*2.8.6.3 Makosa ya Uzalishaji*

Katika kuzungumza na kuandika kuna makosa ya aina tatu yanayoweza kutokea kutokana na usawa na utofauti wa lugha ya kwanza na lugha lengwa:

i) *Ubadala*: Ubadala ni pale mwanafunzi anapotumia mfumo wa lugha ya kwanza katika lugha lengwa (Ringbom 1986).

ii) *Mikopo yenye ukaribu*: Haya ni makosa yanayoonyesha kwa ukaribu sana lugha ya kwanza. Wakati mwingine, mikopo yenye ukaribu huhusisha tafsiri ya sisisi. Mikopo yenye ukaribu hii huweza kuhusisha misemo, methali na mipangilio ya maneno (Fantini 1985).

Ubadala na uzalishaji ndizo aina mbili za makosa ambazo watafiti wengi huchunguza na ambazo huonekana kudai kuwa makosa hufanyika tu kati ya lugha ya kwanza na lugha ya pili (Odlin1989).

iii) *Uwekaji makini zaidi*: Urekebishaji zaidi wakati mwingine huwa na athari za lugha ya kwanza kwa lugha ya pili ambapo mwanafunzi wa lugha ya pili hutaka kuwa makini zaidi na hivyo kuishia kufanya makosa (Ibrahim 1978). Kwa mfano katika Kiswahili, mwanafunzi wa lugha ya Kikisa atajipata akitumia neno */papa/* kwa maana ya */baba/*. Mwanafunzi husika anaporekebishwa hujipata akibadilisha fonimu katika maneno yote ya Kiswahili Sanifu yaliyo na fonimu /p/ kuwa /b/ katika maneno kama vile *papa* (samaki) atasema *baba*, *nilibata* badala ya nilipata, *kibato* badala ya kipato na kadhalika.

*2.8.6.4 Ufasiri Mbaya*

Uhawilishaji hasi wa mifumo ya lugha ya kwanza unaweza kusababisha ufasiri mbaya wa ujumbe wa lugha lengwa. Ufasiri mbaya unamfanya mwanafunzi wa lugha ya pili kufasiri jambo tofauti kabisa na lile linalosemwa na msemaji wa lugha lengwa kimantiki. Uanuwai wa ufasiri unaweza kusababisha unasibishaji mbovu wa fonimu zilizotajwa katika lugha lengwa kwa lugha, fonimu na fonolojia ya lugha ya kwanza. Ufasiri mbaya waweza kutokea pia wakati mpangilio wa maneno katika lugha ya kwanza na lugha ya pili unapotofautiana na wakati chukulizi za kitamaduni zanapotofautiana (Odlin 1989). Utafiti huu umelifuatilia zaidi swala hili la ufasiri mbaya wa maana kwa kuhusisha fonimu za lugha ya pili na lugha ya kwanza na athari zake kwa ufasiri wa maana.

*2.8.6.5 Muda wa Kujifundisha*

Kujifundisha lugha kwa muda mchache kunaweza kumpa mwanafunzi wa lugha ya pili ugumu wakuielewa lugha ya pili vizuri na hivyo kufanya makosa mengi (Ringbom 1987, James 1971). Hali hii inaweza kuwa dhahiri miongoni mwa wanafunzi wa viwango vya chini kielimu kama vile shule za msingi na chekechea kutokana na muda mfupi wa kujifundisha na kutumia Kiswahili Sanifu.

### *2.8.7 Dhana ya Uhamishaji na Kuathiri*

Hizi ni dhana mbili zenye utata kimaana. Kuhamisha mfumo huchukuliwa na wasomi wengine kama kurejelea dhana kuwa kubeba kila kitu hadi hakuna lolote la lugha ya pili linalotumika huku wengine wakiona utata kutokana na kuwa kitu kinapohamishwa basi hakibaki tena pale. Swali la mjadala hapa ni Je, mfumo huo huachwa kutumiwa katika lugha ya kwanza ama unaendelea. Kama unaendelea hivyo basi umehamishwa au la? Ikiwa mfumo huo umehamishwa kwa lugha ya pili je, bado msamiati na mfumo wa lugha ya pili kwa ujumla hutumika au la? Jambo hili huwafanya wasomi kuepuka kuitumia dhana hii ili kuepuka utata (Corder 1983, Kellerman & Smith 1986, Caroll 1968).

Odlin (1989) anaeleza dhana hizi kwa nia ya kujaribu kuzitofautisha. Uhamishaji sio tu kuathiri. Kuathiri hutumika kueleza vipengele kama vile vya kiisimu vinavyopatikana katika lugha ya pili ambavyo vina mfanano na lugha ya kwanza ya mwanafunzi na havipo wala havikubaliki katika lugha ya pili. Kuathiri ni sawa na uhamishaji hasi kwani uhamishaji unahusisha kila kitu katika mfumo lugha na utamaduni wa lugha ya kwanza. Hata hivyo, Odlin anapendekeza matumizi ya uhamishaji hasi kwani tunaweza kutumia istlahi hii kulinganisha na uhamishaji chanya ambao humsaidia mwanafunzi wa lugha ya pili kuelewa kwa urahisi mfumo na leksemu za lugha ya pili na maana zake kwa kuzihusisha na semantiki ya lugha ya kwanza. Isitoshe, uhamishaji sio kila mara ni kutoka lugha ya kwanza kwenda lugha ya pili (Odlin 1989). Kuna uwezekano wa uhamishaji kutoka lugha ya pili hadi lugha ya kwanza.

## 2.9 Masuala ya Kimsingi

Tafiti nyingi zinachunguza sarufi na matamshi kama vipengele muhimu katika uathirianaji. Hata hivyo, kipengele cha utamaduni ni muhimu pia katika athari zinazopitishwa kutoka lugha chanzi hadi lugha lengwa. Utamaduni wa watu wanaopokea lugha ya pili ni muhimu kwani una athari zake kwa lugha ya pili ikiwemo majina ya vitu vilivyo na visivyo katika utamaduni husika. Hili

linatokana na tafiti za awali zilizobaini kuwa mtu huwa na mazoea ya kuhamisha maana na miundo na msambao wa maana na miundo ya lugha yake asilia na utamaduni wake kwa lugha na utamaduni wa kigeni. Lengo la kufanya hivi laweza kuwa kujaribu kuelewa vizuri dhana na kuelewa lugha na utamaduni kama unavyoendelezwa na wazungumzaji wazawa (Fries 1949, Lado 1957, Kaplan 1966, Odlin 1989).

Utafiti huu ulichanganua makosa yanayofanywa na wanafunzi wanaojifunza lugha ya pili lengo moja kuu likiwa kuwasaidia kuelewa sehemu zenye utata na kumsaidia mwalimu kujua sehemu za kutia msisitizo. Hata hivyo, si tofauti zote zilizopatikana baina ya lugha ya kwanza, Kikisa na ya pili, Kiswahili, zilizo na mchango katika kufanya ujifundishaji wa lugha ya pili kuwa mgumu kwa wanafunzi wazungumzaji asilia wa lugha ya Kikisa. Kwa hivyo, si moja kwa moja kuwa tofauti zilizopatikana ndizo sababu za ugumu wa kujifunza Kiswahili kwa wazungumzaji asilia wa Kikisa. Hili ni wazi kwani tofauti baina ya lugha ya kwanza na ya pili haziwezi kuwa thibitisho tosha la kuwa tunaweza kutabiri makosa watakayofanya wanafunzi na kutabiri njia ambayo ikitumika hakutakuwa na makosa yoyote (Odlin 1989, Lee 1968).

Licha ya kuangalia makosa kutokana na athari za Kikisa kwa wajifunzaji wa Kiswahili Sanifu kama lugha yao ya pili, hali si kwamba makosa yote yanatokana na Kikisa katika Kiswahili Sanifu. Tafiti za awali kuhusu makosa katika lugha zilionyesha makosa mengine kutohusiana na lugha ya kwanza, ya pili na hata mchanganyo wa lugha hizo mbili (Hatch 1978, Schumann 1978, Andersen 1979, Odlin 1989). Makosa mengine hutokana na namna wanafunzi walivyofunzwa na wala sio athari za lugha zao za kwanza. Licha ya kuwa kufunza ni jambo muhimu na la manufaa kwa wanafunzi wa lugha pia kufunza kunaweza kusababisha upitishaji wa makosa ambayo hayangefanyika ikiwa mwanafunzi angejifunza pekee yake (Selinker 1972, Stenson 1974, Felix 1981, Odlin 1989). Utafiti huu unatumia makosa yanayopatikana katika lugha ya pili kueleza ujifundishaji wa lugha ya pili na athari zinazotokana na lugha ya kwanza. Tafiti zilizofanywa miaka sitini kuhusu makosa ya kisarufi katika lugha zilionyesha kuwepo kwa makosa sawa yanayofanywa na wanafunzi wa historia tofautitofauti. Makosa mengine pia yalipatikana kufanywa katika upataji wa lugha ya kwanza na lugha ya pili. Hili linazua swali la iwapo kuna ubia katika upataji wa lugha (Odlin 1989, Hatch 1978). Kwa kauli hii, inakuwa vigumu kutambua makosa yaliyopata athari kamili kutoka kwa lugha ya kwanza na pia kujua ni lugha ipi iliyomwathiri mwanafunzi kwani inakuwa vigumu kujua ikiwa mwanafunzi ameathiriwa na kwa

mfano lugha ya Kikuyu au Kikisa ikiwa fonimu tunayozungumzia ipo katika lugha za Kikuyu na Kikisa na haipo katika Kiswahili Sanifu. Hali kama hii inaweza kusababisha hitimisho lisilo kamilifu.

Athari za lugha ya kwanza ni kigezo muhimu katika upokeaji wa lugha ya pili. Mifumo ya lugha ya kwanza inapoathiri lugha ya pili ya mwanafunzi ina madhara kwa uzungumzaji wake wa lugha hiyo kama vile kimatamshi. Aidha, wakati lugha hiyo inapotumika katika ufundishaji, matatizo ya mwanafunzi wa lugha ya pili huongezeka. Hili linasababisha kutoeleweka kwa dhana mbalimbali na kutomwelewa mwalimu yeyote anayefunza kwa kutumia lugha hizi kama chombo cha mawasiliano na kama lugha ya kufunzia somo lolote lile. Humfanya mwanafunzi kutokuwa mkakamavu katika uulizaji na kujibu maswali. Hali kama hii itazuia ujifunzaji mbovu na mwishowe matokeo mabaya katika sio tu lugha hii ya pili husika bali masomo yote na matokeo yake kwa ujumla. Hili laweza kumsababishia mwanafunzi mzongo wa mawazo na hata wakati mwingine kumkatisha tamaa ya masomo. Hata anapojikaza kusoma na hali hii isirekebishwe huenda mustakabali wake kimasomo ukakumbwa na matatizo kutokana na matokeo mabaya. Utangamano wake katika jamii pia waweza kuathirika kwa kutojiamini na kutotaka kuzungumza zaidi kwa kutotaka kuonyesha makosa yake. Hili laweza kuathiri hata hulka yake katika jamii. Ni kutokana na hali ya kutafuta mbinu za kupunguza kwa kiasi angaa kidogo matatizo kama haya ambapo uchunguzi na uchanganuzi wa makosa unapokuwa muhimu hata zaidi.

## 2.10 Hitimisho

Sura hii imelijadili swala la makosa, Uchanganuzi wa Makosa na Lugha Kati ili kuonyesha umuhimu wa dhana hizi katika ufanikishaji wa utafiti wa sasa. Tumetoa maelezo anuwai kutoka kwa wasomi na waandishi mbalimbali ili kuonyesha misimamo yao kuhusu lugha ya kwanza, ya pili na ufanyaji makosa. Tumeeleza kwa uchache kuhusu lugha ya Kiswahili Sanifu na lahaja za Kiluhya ikiwemo Kikisa ili kutambulisha lugha zinazohusishwa katika utafiti huu. Sura hii imeweka bayana umuhimu wa uchanganuzi makosa ili kuweka msingi wa kazi hii na kuonyesha haja ya utafiti huu kufanyika. Tofauti kati ya ufanyaji makosa kwa kushtukia na ufanyaji makosa kutokana na athari za lugha ya kwanza imewekwa wazi ili kuonyesha mwelekeo wa utafiti huu kimalengo.

## Sura ya 3
## Uchanganuzi wa Data Kutoka Nyanjani

### 3.1 Utangulizi

Sura hii inafafanua na kuweka bayana data iliyopatikana nyanjani. Sura hii inaonyesha na kueleza makosa yanayofanywa na watafitiwa katika lugha ya Kiswahili Sanifu. Makosa haya kwa sehemu kubwa yanatokana na athari za lugha ya kwanza ambayo katika muktadha huu ni lugha ya Kikisa.

Kiswahili ni lugha inayozungumzwa na thuluthi mbili ya watu nchini Kenya. Kujulikana kwa lugha ya Kiswahili kunatokana zaidi na sera za lugha zilizowekwa zinazohusu lugha hii kama vile kuipa hadhi ya kuwa lugha ya taifa na somo la lazima shuleni. Kupitia kwa sera hizi, Kiswahili Sanifu kimeweza kufunzwa na kutumiwa kufunzia na hivyo kuifanya lugha hii lingua franka na lugha inayotumiwa na wananchi wa hadhi zote nchini Kenya. Hata hivyo, wananchi hawa wote wana lugha zao asilia ambazo ndizo lugha za kwanza kujifunza kabla ya kujifunza Kiswahili Sanifu kama lugha ya pili na hata kwa wengine kama lugha ya tatu haswa watoto wa kutoka familia yenye baba na mama wanaotumia lugha mbili tofauti.

Kiswahili Sanifu, kwa kukosa kuwa lugha ya kwanza, panatokea uwezekano wa wazungumzaji wa Kiswahili walio wazungumzaji asilia wa Kikisa kuathiriwa na lugha ya kwanza wanapojifunza lugha ya Kiswahili. Sura hii inatoa mifano ya makosa wanayofanya wanafunzi walio wazungumzaji asilia wa Kikisa wanapozungumza Kiswahili Sanifu ama kwa kusudi au kwa kushtukia. Makosa yanayojadiliwa katika sura hii, yanaonyesha tofauti chache zilizopo za kimuundo na kimatumizi za maneno na miundo yake katika lugha za Kiswahili Sanifu na Kikisa.

Makosa yanayobainishwa na kuelezwa katika sura hii yamewekwa katika makundi mbalimbali yakiwemo makosa ya kileksika, makosa ya kifonolojia, makosa ya kisintaksia na makosa ya kisemantiki. Makosa haya ya kisarufi yaliyobainishwa yanatokana na sababu kama vile; ubebaji wa mifumo ya Kikisa, umakinifu kupindukia wakati wa kutumia Kiswahili Sanifu kama lugha ya pili kwa mzungumzaji asilia wa Kikisa na ujumlishaji mno wa kanuni za lugha walizofunzwa mwanzo wanafunzi ili kurahisisha ujifunzaji wao.

**3.2 Tofauti baina ya fonimu za Kiswahili na Kikisa**

Kiluhya na Kikisa ni lugha za Kibantu. Lugha hizi mbili za Kiswahili na Kikisa zina ukaribu wa kimfanano katika vipengele vyake vya kisarufi. Baadhi ya fonimu ambazo zinapatikana katika Kiswahili Sanifu na hazipo katika Kikisa ni pamoja:

/b/ /g/ /θ/ /ɟ/ /ð/ /d/ /v/ /z/

Fonimu hizi hazipatikani katika Kikisa. Hata hivyo kuna pia fonimu ambazo hazipatikani katika Kiswahili na zipo katika Kikisa kwa mfano: /ʦ/ na /β/.

**3.3 Ubadilishaji Fonimu**

Idadi kubwa ya makosa yanayotokana na athari za Kikisa yametokana na mageuzi ya kimofofonolojia yaliyofanyiwa konsonanti za Kiswahili na wasemaji wa Kiswahili walio wazungumzaji asilia wa Kikisa kama lugha yao ya kwanza. Mabadiliko haya ya kifonimu na ambayo yanasababisha athari za kisemantiki ni kama ifuatavyo:

***3.3.1 Ubadala wa /p/ > /b/***

| **(1)** | **makosa** | **sahihi** |
|---|---|---|
| | [papa] | [baba] |
| | [tusi*batɛ*] | [tusipatɛ] |
| | [*kupɛpɛa*] | [kubɛbɛa] |

Makosa kama haya yanatokana na sababu anuwai. Sababu hizi ni pamoja na:

i) /p/ na /b/ ni alofoni za fonimu moja katika Kikisa kinyume na ilivyo katika Kiswahili.

ii) Ukosefu wa fonimu /b/ katika Kikisa unasababisha matumizi ya fonimu /p/ ambayo ndiyo iliyozoeleka kwa mzungumzaji asilia wa Kikisa.

iii) Urahisi wa utamkaji wa fonimu /p/ katika Kikisa kinyume na ilivyo katika Kiswahili ambapo fonimu ya Kiswahili Sanifu inakuwa na ugumu wa kutamka. Ugumu huu unampa mzungumzaji kutumia nguvu nyingi na kwa hiyo Mkisa ana hiari kutumia nguvu chache na kusababisha kosa la kimatamshi na kimaana katika Kiswahili Sanifu.

***3.3.2 Ubadala wa /v/ > /f/***

| **(2)** | **makosa** | **sahihi** |
|---|---|---|
| | [futa] | [vuta] |
| | [amɛfunja] | [amɛvunja] |
| | [lina*fuɟa*] | [linavuɟa] |

Makosa haya yanafanyika kwa kubadiili fonimu /v/ kuwa /f/ katika 1. Kubadili huku kunabadili maana ya msemo huo kabisa. Badala ya 'vuta nikuvute' kuwasilisha ujumbe wa kuwepo kwa mvutano au kutokuelewana, maneno hayo yatapitisha ujumbe kuwa mmoja anampangusa mwenzake na mwenzake pia akifanya vilevile.

Sentensi 3 inatoa maana ya kukanganya sana kwa msikilizaji mahiri wa Kiswahili Sanifu. Kuharibu (fuja) limetumika kwa maana ya kupitisha maji (vuja). Maana ya sentensi hii imepotoka au hata kupotea kabisa.

***3.3.3 Ubadala wa /ɟ/ > /ʧ/***

| **(3)** | **makosa** | **sahihi** |
|---|---|---|
| | [*mʧusi*] | [mɟuzi] |
| | [*ma:* ʧapu] | [ma: ɟabu] |
| | [kuʧa] | [kuɟa] |

Katika sentensi *Amepatana na mchusi* ni sentensi iliyozalishwa baada ya fonimu /ɟ/ kubadilishwa na /ʧ/ na fonimu /z/ kubadilishwa na /s/. Neno hili /mɟuzi/ liliweza kusemwa na wanafunzi kwa makosa mara tatu ambayo yalitoa maana tatu tofauti katika Kiswahili Sanifu kutokana na athari za Kikisa.

Kwa mujibu wa *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (TUKI, 2013) neno 'mchusi' halipo katika msamiati wa Kiswahili Sanifu.

| **neno katika Kamusi** | **maana** |
|---|---|
| [mɟuzi] | mtu mwenye maarifa fulani ya jambo |

| | |
|---|---|
| [mɟusi] | Mnyama wa jamii yenye damu baridi mdogo kuliko kenge huishi mashimoni na miambani. |
| [mʧuzi] | Kitoweo cha majimaji kilichopikwa kwa kuchanganya. |

Kwa kutathmini maana za maneno haya yaliyotamkwa kimakosa, tunapata maana aina tatu kama zilivyojitokeza katika kamusi ya TUKI (2013). Hata hivyo, maana ya moja kwa moja inayofaa kujitokeza bila kufikiria alichotaka kusema msemaji inaonekana kutokuwepo katika msamiati wa Kiswahili Sanifu na hivyo kutoa nafasi ya kukisia tu alichokusudia kukisema. Ikiwa msikilizaji hatafikiria kuhusu neno jingine la Kiswahili alilotaka kulitamka msemaji basi mawasiliano yatakatika. Ikiwa msikilizaji hana utambuzi wa athari za Kiluhya hasa Kikisa zinazoweza kumuathiri mzungumzaji asilia wa Kikisa anapozungumza Kiswahili Sanifu, atachanganyikiwa kung’amua anachosema mzungumzaji. Hata hivyo, ikiwa msikilizaji atakuwa anayefahamu uwepo wa athari za Kikisa katika matamshi hayo atabahatisha neno moja kati ya mjusi, mjuzi na mchuzi kulingana na muktadha. Ikiwa msikilizaji atachagua neno mchuzi au mjusi atapata maana tofauti na iliyodhamiriwa na msemaji. Hivyo basi huenda sentensi hii ikaeleweka, ikaeleweka visivyo au ikakosa kueleweka kabisa.

Maneno mengine ya ubadilishaji wa fonimu /ɟ/ kuwa /ʧ/ ni kama ifuatavyo:

| (4) | makosa | sahihi |
|---|---|---|
| | [tutaʧɛɲga] | [tutaɟɛɲga] |
| | [ʧumba] | [ɟumba] |
| | [maʧi] | [maɟi] |

***3.3.4 Ubadala wa /g/ > /k/***

| (5) | makosa | sahihi |
|---|---|---|
| | [mukɔmɔ] | /mgɔmɔ/ |
| | [kuɔka] | [kuɔga] |
| | [pika] | [piga] |

Fonimu /g/ imebadilishwa hadi /k/. Maana ya neno *mgɔmɔ* imeathirika kutokana na athari za uhawilishaji wa fonimu. Madhumuni ya sentensi hii ni kuwajulisha watu kuwa kutakuwa na mgomo neno ambalo linahusika na kususia kazi au majukumu aliyopewa mfanyikazi kwa ajili ya kulalamikia haki fulani iliyokiukwa. Neno 'mgɔmɔ' linapobadilishwa kuwa 'mukomo' lina uchopekaji wa /u/ baina ya /m/ na /k/ na vilevile maana imeathiriwa. Maana ya sentensi 1 inabadilika na kuwa hali ya kufikia mwisho wa jambo.

Maneno mengine yaliyobadilishwa fonimu /g/ kuwa /k/ ni pamoja na:

| | | |
|---|---|---|
| **(6)** | **makosa** | **sahihi** |
| | [ukali] | [ugali] |
| | [pika] | [piga] |
| | [mbɔka] | [mbɔga] |

Sentensi: *Tunapikana vita vya kiroho.*

Athari za Kikisa zinasababisha mabadiliko ya fonimu /g/ kuwa /k/. Maana inaathirika na hivyo kumchanganya msikilizaji jinsi vita vinaweza kupikwa.

***3.3.5 Ubadala wa /s/ > /z/***

Hali hii hutokea kupitia uwekaji makini kupita kiasi. Mjifunzaji anaporekebishwa na kufunzwa namna ya kutamka fonimu za Kiswahili Sanifu, yeye anajumlisha hali hiyo ya baadhi ya fonimu za Kiswahili Sanifu kuwa kinyume cha fonimu za Kikisa katika fonimu zote za Kiswahili. Mjifunzaji hufanya hili ili kuepuka ufanyaji wa makosa katika uzungumzaji na uandishi wake wa Kiswahili Sanifu. Kwa kuwa makini zaidi, makosa hutokea kama mifano ifuatayo inavyodhihirisha.

| | | |
|---|---|---|
| **(7)** | **makosa** | **sahihi** |
| | [kasa] | [kaza] |
| | [kasi] | [kazi] |
| | [ʧesa] | [ʧeza] |

Mfano wa pili una neno ‘kasi’ ambalo limetokea kutokana na athari za Kikisa kwa Kiswahili cha mzungumzaji na kupelekea ubadilishaji wa /s/ kuwa /z/. Maana hapa inaathirika kwani mzungumzaji mahiri wa Kiswahili Sanifu ataelewa kama ‘haraka’ huku msemaji akiwa na maana ya ‘kazi’.

### *3.3.6 Ubadala wa /d/ > /t/*

| (8) | makosa | sahihi |
|---|---|---|
| | [batiliʃwa] | [badiliʃwa] |
| | [tari] | [dari] |
| | [batɔ] | [badɔ] |

Neno ‘batilishwa’ lina maana tofauti sana na ‘badilishwa’ kama Kamusi ya TUKI (2013) inavyoeleza kwa vidahizo hivi:

| neno katika Kamusi | maana |
|---|---|
| [batili] | Tangua maafikiano au mkataba uliokuwapo. |
| [badili] | Ondoa kitu au mtu na weka kitu au mtu mwingine. |
| [patili] | tia maanani |

Katika sentensi hii: ‘kesi yake ilibadilishwa’, ukosefu wa makini ya kutamka fonimu unaweza kusababisha maana tofauti. Huku sentensi hii ikimaanisha kesi aliyokuwa nayo mhusika imetolewa na kuwekwa nyingine, matumizi ya neno ‘batilishwa’ yatamaanisha kesi hiyo haipo tena na hakuna nyingine anayofaa kujibu. Matumizi ya neno ‘patilishwa’ yataleta maana kuwa kesi ya mhusika imetiliwa maanani na huenda ikachukuliwa kwa uzito mkubwa. Uelewa wowote mwingine isipokuwa ule ulionuiwa na msemaji utakuwa wa kupotosha maana na hivyo kueleweka vibaya.

Katika neno ‘bato’ na ‘pato’ panatokea utata wa kimaana kutokana na athari za Kikisa kwa matamshi ya msemaji.

| (9) | neno | maana |
|---|---|---|
| | [batɔ] | baka |

| | |
|---|---|
| [badɔ] | wakati wake haujafika |

Sentensi '*bato, nitakuita'* ni sentensi inayonuiwa na msemaji kupitisha ujumbe kuwa wakati wa kumuona haujafika lakini ufikapo msemewa ataitwa. Maana hii huenda isijitokeze vivyo hivyo kwa msikilizaji atakayebaki kushangaa ni vipi anatakiwa kumbaka mtu hadi atakapoitwa. Sentensi hii inakosa kueleweka kwa msikilizaji mahiri wa Kiswahili Sanifu au ikaeleweka vibaya na kusababisha kuhuzunishwa kwa msikilizaji na kauli hii kutoka kwa msemaji.

### *3.3.7 Ubadala wa /ð/ > /θ/*

Hali hii inatokana na athari za lugha ya Kikisa kukosa fonimu /ð/ katika fonimu zake. Wajifunzaji wa Kiswahili Sanifu kama lugha ya pili wanapata ugumu wa kutumia fonimu /ð/ na hivyo kutumia /θ/ mahali pa /ð/ ambayo wamezoea kuitamka na hivyo inaonekana rahisi. Kwa kutaka kurahisisha matamshi yao wanajipata wakifanya makosa ya kimatamshi katika Kiswahili Sanifu.

| **(10)** | **makosa** | **sahihi** |
|---|---|---|
| | [θambi/] | [ðambi] |
| | [θɔrupa] | [ðɔruba] |
| | [θ*ahabu*] | [ðahabu] |

Katika matamshi, fonimu /ð/ huweza kugeuzwa kuwa /θ/ au /ts/ kama vile katika maneno: *tsemanini, tsamini, tsambi na tsahapu*.

Fonimu hizi zinabadilishwa kutokana na sababu kuwa zinakosekana katika lugha ya kwanza ya wazungumzaji hawa ambayo ni Kikisa. Fonimu kama vile /j/, /z/ /d/ /g/ /b/ aghalabu hazitumiki katika Kikisa. Hata hivyo fonimu /b/ inapotumika inabadilishwa kimatamshi na kuwa fonimu katikati ya /b/ na /v/ yaani /β/.

Fonimu /θ/ haipo katika fonolojia ya Kikisa. Ukosefu wa fonimu hii ndicho kisababishi cha ugumu wa kutamka fonimu hiyo katika Kiswahili kama katika maneno *thelathini, themanini, thuluthi* nakadhalika kwa wazungumzaji asilia wa Kikisa. Badala ya fonimu /*θ*/, fonimu iliyo rahisi kwa wazungumzaji wa Kikisa ni /ts/. Hivyo basi wanafunzi wa Kiswahili Sanifu walio Wakisa, wanaweka /ts/ mahali pa /θ/ kama katika maneno hayo tuliyotaja hapo juu.

Fonimu hizi zinapobadilishwa zinaleta utata mkubwa wa kimaana. Neno kama vile 'kazi' katika mifano hii lina maana tofauti kabisa na neno 'kasi'. Athari inapojitokeza wakati neno hili linatumika katika sentensi, inakuwa vigumu kwa msikilizaji kuelewa ujumbe wa sentensi kutokana na utata wa kimaana. Pengine, kwa sababu ya neno hili kuwepo katika Kiswahili Sanifu, pakatokea hata athari potovu ya kupata maana ambayo haikunuiwa na msemaji. Kwa mfano:

**(11)** *Sentensi 1*: Nitakwenda *kasi* kisha nirudi.

*Sentensi 2:* Nitakwenda *kazi* kisha nirudi.

Katika mifano hapo juu sentensi ya 1 inawakilisha alichosema msemaji wa kauli na sentensi ya 2 ni maana ambayo msemaji alidhamiria kuiwasilisha. Sentensi ya kwanza, inakaribisha swali unaenda *wapi?* kutoka kwa msikilizaji. Kwa msemaji atakuwa sawa akilini akijua kuwa alichosema kina ujumbe kamili kama inavyojitokeza katika sentensi ya pili. Hivyo basi, huenda swali *unaenda wapi* likamuudhi kwani ashasema anakoenda. Msemaji anaona amesema kuwa *anaenda anakofanya kazi* huku msikilizaji akielewa kuwa amesema *atakwenda kwa haraka* licha ya kuwa hajasema wapi. Hali kama hii, inadhihirisha jinsi mawasiliano yanavyoweza kukatishwa na kuvunjika kabisa kutokana na athari za lugha ya kwanza.

Mifano ya utata kama huu yaweza kupatikana katika sentensi zifuatazo:

**(12)** *Sentensi 1*: Alim*pika* kuku hadi akaumia.

*Sentensi 2*: Alimpiga kuku hadi akaumia.

*Sentensi 1*: Nitakuletea *chumatatu.*

*Sentensi 2*: Nitakuletea Jumatatu.

Maneno kama vile *'msasi'* na 'mzazi' yana maana mbili tofauti kabisa katika Kiswahili ambazo hazina ukaribu wowote. Fonimu inapobadilishwa, hubadilisha matamshi ya neno husika na hubadilisha maana. Utata huu wa kimaana waweza kuonyeshwa kupitia mifano ya sentensi hizi:

**(13)** *Sentensi 1*: Huyu ni *msasi* wangu.

*Sentensi 2*: Huyu ni mzazi wangu.

Katika sentensi ya kwanza neno ‘msasi’ linarejelea mtu ambaye ni adui wa msemaji kwani ni mtu anayemuwinda kwa nia ya kutaka kumaliza maisha yake. Katika sentensi ya 2, msemaji anamtambulisha mtu aliyemzaa. Mzazi kwa kawaida, ni mtu aliye karibu naye kama mwanawe na aliye kama rafiki anayemtakia mema. Kwa kumtambulisha mhusika kwa kutumia sentensi ya kwanza akimaanisha sentensi ya 2 inakuwa ni kuleta utata mkubwa kimaana. Msikilizaji ataelewa jambo tofauti kabisa na dhamira ya msemaji anapotoa kauli hii. Msikilizaji atamwona anayerejelewa kama mwindaji. Msemaji atakuwa na maana ya aliyemzaa. Utata huu unaweza kuwa hata mkubwa zaidi wakati mwalimu anapofunza vitate ambapo maneno mawili yenye maana tofauti yanafaa kutumika kwenye sentensi moja kwa mfano ‘*Msasi* wangu ni msasi’ badala ya sentensi ‘Mzazi wangu ni msasi’. Utata huu unajitokeza katika maneno mengine kama ifuatavyo:

**(14)** *Sentensi 1a)*: *Ukali* wake umekwisha.

*Sentensi 1b):* Ugali wake umekwisha.

*Sentensi 2a): Papa* alimchapa mwanawe na kumpeleka shuleni.

*Sentensi 2b):* Baba alimchapa mwanawe na kumpeleka shuleni.

Katika sentensi 1 a) na 1 b), neno ‘ukali’ na ‘ugali’ na katika 2a) na 2b) neno ‘papa’ na ‘baba’ ni mifano ya makosa yanayofanywa na mzungumzaji wa Kiswahili aliye mzungumzaji asilia wa Kikisa. Maneno haya yana tofauti kubwa. *Papa* ni mnyama wa baharini huku *baba* akiwa mzazi wa kiume wa mtoto anayerejelewa. Inakuwa vigumu kujua ikiwa ni papa wa majini au mzazi, lakini kupeleka shuleni kunaleta dhana tofauti ambayo katu haitolewi maana na neno ‘papa’ ambalo ndilo neno asilia lililotumika. Ukali wa mtu kwa mfano, kwa kukaripia unaweza kwisha labda kwa kukutana na wakali zaidi au kwa kujinyenyekeza katika mazingira fulani. Huu ndio ujumbe anaopata msikilizaji ambao sio alioulenga kuupitisha msemaji kwani nia yake ni kusema ‘ugali’ ambacho ni chakula cha baba kimekwisha. Swala la muktadha katika sehemu hii linajitokeza kuwa muhimu kuzingatiwa ili kukisia maana aliyo nayo mtoaji wa kauli aliye na athari za lugha ya Kikisa.

Makosa ya kubadili fonimu katika muundo wa leksemu za Kiswahili yamejitokeza kwa kiwango kikubwa. Kubadili fonimu huku kunabadili maana iliyokusudiwa. Kwa mfano neno *kupaka* na *kubaka* ni maneno mawili tofauti yaliyo na maana tofauti ambapo kwa kutaja moja kwa maana ya

neno jingine kunaweza kuleta utata mkubwa. Kwa mfano hisia zitakazoibuliwa kwa wasikilizaji wanaposikia kuhusu ‘anayepaka’ na ‘anayebaka’ ni tofauti. Huenda ‘anaye*paka’* akapewa zawadi huku ‘*anayebaka’* akiadhibiwa adhabu inayoweza kuishia kuwa kifo chake. Hali hii inaonyesha uzito wa utumiaji wa fonimu sahihi katika maneno wakati wa mawasiliano. Hali hii inadhihirisha uwezo wa athari za kuhawilisha fonimu moja katika neno iwe ama kwa kusudi au kwa athari za lugha ya kwanza kwa maana ya neno hilo na kwa mawasiliano katika lugha ya pili.

### 3.4 Uchopekaji

Mweri (2010) anaeleza uchopekaji kama hali ambapo sauti huongezwa kwa zile zinazopatikana tayari katika neno. Uchopekaji ni uingizaji wa fonimu katika silabi au fonimu za neno. Uchopekaji wa fonimu huathiri muundo wa kimofolojia na kifonolojia wa neno husika.

#### *3.4.1 Uchopekaji wa /h/*

Athari hii hutokea kutokana na kuwa makini zaidi kwa mzungumzaji wa Kiswahili Sanifu aliye na athari za Kikisa. Kwa kutaka kutumia Kiswahili Sanifu kwa makini zaidi anafanya makosa ya kuchopeka fonimu /h/.

| **(15)** | **makosa** | **sahihi** |
|---|---|---|
| | [hɔwa] | [ɔa] |
| | [natumahi] | [natumai] |

#### *3.4.2 Uchopekaji wa irabu /u/*

| **(16)** | **makosa** | **sahihi** |
|---|---|---|
| | [mupira] | [mpira] |
| | [muʧɛsɔ] | [mʧɛzɔ] |
| | [mukɔnɔ] | [mkɔnɔ] |

#### *3.4.3 Uchopekaji wa Nusu Irabu /y/ na /w/*

| **(17)** | **makosa** | **sahihi** |
|---|---|---|
| | [yɛnyu] | [yɛnu] |
| | [huwɔ] | [huɔ] |

### *3.4.4 Uchopekaji wa Irabu /i/*

| (18) | makosa | sahihi |
|---|---|---|
| | [injɛ] | [njɛ] |
| | [inchini | [nchini] |
| | [wanainchi] | [wananchi] |

Fonimu /m/ inajitokeza katika Kikisa kama /mu/. Hakuna maneno yanayoweza kuanza kwa /m/ bila kuongeza /u/ katika Kikisa. Hali hii inahawilishwa vivyo hivyo na wanafunzi walio wazungumzaji asilia wa Kikisa hadi katika Kiswahili Sanifu ambako mfumo huu haukubaliki. Kinachodhihirika wazi ni kuwa, katika Kikisa maneno hayaanzi kwa nazali pekee kama silabi. Nazali sharti iongezwe vokali kama inavyodhihirika katika maneno */mupira/, /mukutanɔ/* na kadhalika. Uongezaji wa irabu /u/ unakuwa makosa katika Kiswahili Sanifu.

Fonimu hizi zinaongezwa ili kuyapa maneno mfumo wa lugha ya kwanza ambayo katika muktadha huu ni lugha ya Kikisa. Mfumo wa Kikisa ni KVKV ambapo kila sehemu palipo na konsonanti lazima vokali iwekwe pia. Hivyo basi, neno kama vile ‘mkono’ linaonekana si sahihi kwa mzungumzaji wa Kikisa kwani hakuna vokali kati ya /m/ na /k/ na hali hii inapelekea kuwekwa kwa vokali hiyo /u/ ili kuafikiana na mahitaji ya kisaikolojia kuhusu lugha aliyo nayo mzungumzaji wa Kikisa kama lugha ya kwanza. Pia, sauti /mu/ inakuwa rahisi kuwekwa na mzungumzaji mzawa wa Kikisa kutokana na mfumo wa ngeli ambapo neno lenye maana ya ‘mkono’, lipo katika ngeli ya kimofolojia ya MU - MI. Neno hilo lipo katika kundi la maneno yanayopata umoja kwa kutumia kiambishi {mu} na wingi {mi} kwa mfano:

| (19) | umoja | | wingi | |
|---|---|---|---|---|
| | [mukhɔnɔ] | *(*mkono) | [*mikhɔnɔ*] | (mikono) |
| | [*musala*] | *(*mti) | [*misala*] | (miti) |
| | [/*mukunda*] | (shamba) | [*mikunda*] | (mashamba) |

Katika mifano hapo juu panashuhudiwa matatizo yanayotokana na tofauti za semantiki inayotokana na ngeli. Vigezo vinavyotumiwa kuweka majina katika ngeli za majina katika Kiswahili Sanifu ni tofauti na ifanywavyo katika Kikisa. Kwa mfano, katika Kiswahili Sanifu, neno mkono linapatikana katika ngeli ya kimofolojia ya M/MI na Kikisa inakuwa MU/MI.

### 3.5 Udondoshaji

Udondoshaji ni hali ya kutoa sauti moja au zaidi katika neno na hivyo kupelekea mabadiliko katika matamshi ya neno hilo. Udondoshaji ni mfanyiko unaohusisha uondoshaji wa sauti katikati ya neno. Kuna aina mbili za udondoshaji: Udondoshaji Kati na Udondoshaji mwisho. Udondoshaji Kati huhusisha sauti kuachwa katika mazingira ya katikati ya neno. Udondoshaji mwisho huhusu uondoshaji wa herufi ya mwisho, silabi au sehemu ya mwisho ya neno (Mweri 2010, Massamba 1996). Kutokana na data iliyopatikana nyanjani, mifano ya udondoshaji ni pamoja na:

#### *3.5.1 Udondoshaji wa /h/*

| (20) | makosa | sahihi |
|---|---|---|
| | [muɔgɔ] | [muhɔgɔ] |
| | [maindi] | [mahindi] |
| | [asubui] | [asubuhi] |

Neno la ‘muhogo’ katika Kikisa ni ‘*muoko’*. Wanaojifunza lugha ya Kiswahili hujipata wakilazimisha kudondosha fonimu /h/ ili neno hili liafiki mfumo wa Kikisa. Kwa kurahisisha neno *mahindi* pia wanaepuka kutamka fonimu /h/. Uepukaji huu huweza kufanywa kutokana na athari za Kikisa na pia kama njia ya wanafunzi kujitafutia namna rahisi ya kusahilisha utamkaji wa maneno husika. Isitoshe, idadi kubwa ya maneno haya hutuholewa kutoka kwa Kiswahili Sanifu hadi katika Kikisa na kupitia upururaji fonimu /h/ hudondoshwa. Hali hii ya matamshi huwaathiri wanafunzi wa Kiswahili Sanifu walio wazungumzaji asilia wa Kikisa kwa kudhani kuwa wamepata maneno yale yale wanayoyajua katika Kikisa na hivyo kuyatamka maneno husika vilevile yalivyotoholewa.

### 3.6 Uongezaji Fonimu

| (21) | makosa | sahihi |
|---|---|---|
| | [nipɛkɔ] | [nipɛ] |
| | [napɛndaɲga] | [hupɛnda] |
| | [kukufa] | [kufa] |

Kiambishi ‘khu/khwo’ katika katika lugha ya Kikisa kinatumika kuonyesha upole. Kiambishi hiki kinatumika ili kuonyesha anayesema anaomba na wala hashurutushi lolote. Kwa mfano

| | | |
|---|---|---|
| **(22)** | [*mbɛxu*] | (tafadhali nipe.) |
| | [*khusayɛxu*] | (tafadhali tuombe) |
| | [*shinaxwɔ*] | (tafadhali cheza) |

Wanafunzi walio wazungumzaji asilia wa Kikisa wanajipata wakihawilisha kiambishi hiki cha 'upole' hadi katika Kiswahili Sanifu na hivyo kutafuta njia ya kukitofautisha na Kikisa kwa 'kukiswahilisha' kwa kutoa /h/ au /hw/ ili kubaki na 'ko' kwa mfano:

| | | |
|---|---|---|
| **(23)** | [n*ipɛkɔ*] | (tafadhali nipe) |
| | [*tuɔmbɛkɔ*] | (tafadhali tuombe) |
| | [*chɛzakɔ*] | (naomba ucheze) |

Hali iwapo hivi kwa msikilizaji mahiri wa Kiswahili Sanifu na asiye na ufahamu mzuri wa historia ya mzungumzaji, huenda asipate maana ya maneno haya na hivyo kutomwelewa msemaji.

Kiambishi 'nga' hutumika katika lugha ya Kikisa kwa kuonyesha hali ya mazoea. Kiambishi cha hali ya mazoea katika Kiswahili ni 'hu'. Kiambishi hiki 'nga' huhawilishwa kutoka kwa lugha ya Kikisa na matumizi yake kuletwa katika Kiswahili Sanifu kama inavyoonekana katika sentensi hizi:

| | | |
|---|---|---|
| **(24)** | 1. Mimi napendanga kusoma vitabu | '*isie nyanzanga khusoma vitapu'* |
| | 2. Naendanga nyumbani Jumatatu | '*Enzitsanga ingo Jumatatu'* |
| | 3. Nasomanga usiku | *'esomanga eshiro'* |

### 3.7 Makosa Yatokanayo na Ngeli

Baadhi ya makosa ya kingeli yaliyobainishwa ni pamoja na:

| | | |
|---|---|---|
| **(25)** | **makosa** | **sahihi** |
| | [makɔnɔ] | [mikɔnɔ] |
| | [mapaka] | [paka] |

[ɲɔmbɛ hiyɔ]  [ɲɔmbɛ huyɔ]

Ipo tofauti katika Kikisa kati ya neno la mkono mzima na viganja vya mikono. Kwa mfano, mtu anapoosha mikono yake basi atakuwa anaosha mikono (*saba mikhono*). Lakini hali hii hubadilika wakati anapoosha viganja (*saba makhono*). Mfumo huu unapobebwa hadi katika Kiswahili haukubaliki. Hali hii huleta utata kimaana. Hali hii hutokea pia katika maneno mengine ambayo kwa kawaida katika lugha ya Kikisa huwa na viambishi vya umoja na wingi huku viambishi vya Kiswahili vikiwa tofauti hasa pale kiambishi cha umoja na wingi katika lugha ya Kiswahili ni mofu kapa. Maneno haya yanaonyesha hali hii:

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **(26)** | **umoja** | | **wingi** | |
| | Ǿ [nyumba] | (***i****nyumba)* | Ǿ [nyumba] | ***(tsi****nyumba)* |
| | Ǿ [sahani] | (**i**s*ahani)* | Ǿ [sahani] | ***(tsi****sahani)* |
| | Ǿ [chapati] | (***i****chapati)* | Ǿ [chapati] | ***(tsi****chapati)* |

Licha ya kuwa neno *sahani* na neno *chapati* ni maneno ya mkopo kutoka Kiswahili, yamejipata katika lugha ya Kikisa na hivi kupururwa ili kuafikiana na mfumo wa kifonolojia na kimofolojia wa Kikisa. Hii ni kupitia mchakato wa ukopaji uitwao utohozi (Iribemwangi na Mukhwana 2011). Hivyo basi, maneno haya hupokezwa kwa wanafunzi hawa yakiwa kwenye mifumo hii na hivyo athari zake hazianzi katika lugha ya Kiswahili Sanifu bali katika lugha ya Kikisa kwa wanafunzi wanaojifunza Kikisa kabla ya kujifunza Kiswahili Sanifu.

### *3.7.1 Idadi katika Kiswahili Sanifu na Kikisa*

Baadhi ya nomino katika Kikisa huchukua viambishi vya umoja na wingi lakini hali ni tofauti katika Kiswahili Sanifu. Hali hii ndiyo inayosababisha makosa kama yafuatayo:

**(27)** 1. Nilikuwa karibu kuumwa na *maumbwa*

2. Nilisikia *mapaka* yakilia

3. Wezi waliiba *mang'ombe* katika kijiji chetu.

Uundaji wa umoja na wingi wa sampuli hii unatokana na hali kuwa maneno kama haya yanaunda wingi na yana viambishi vya umoja na wingi katika Kikisa kwa mfano:

| (28) | umoja | | wingi | |
|---|---|---|---|---|
| | [*lipaka*] | (paka) | [*mapaka*] | (paka) |
| | [*Iɲɔmbɛ*] | (ng'ombe) | [*tsiɲɔmbɛ*] | (ng'ombe). |

Hali kama hii hutokea katika takriban nomino zote za mkopo katika Kikisa lakini muundo wa mfanyiko na ngeli ambazo maneno hayo huingia si moja kwa mfano:

| (29) | umoja | | wingi | | ngeli |
|---|---|---|---|---|---|
| | [ikabati] | (kabati) | [tsikabati] | (kabati) | I/TSI |
| | [mutɔka] | (gari) | [mitɔka] | (magari) | MU/MI |
| | [liʧuŋgu] | (panya) | [maʧungu] | (paka) | LI/MA |

Katika mifano hii (29), majina haya matatu yamekopwa kutoka kwa Kiswahili Sanifu lakini yakaingizwa kwa kutumia ngeli tofauti. Idadi kubwa ya maneno mkopo katika Kiswahili huingia na ngeli ya I/ZI (Mukhwana na Iribe 2011). Katika Kikisa nomino mkopo nyingi hutumia ngeli ya I/TSI isipokuwa katika hali chache kama hizi. Wanafunzi wa Kikisa wanapojifunza lugha ya pili katika utambuzi wa lugha hii, hujipata wakihamisha mitindo ya umoja na wingi kama hii. Uhamishaji huu unatokana na hali tofauti za kingeli zinazozikumba lugha hizi mbili. Katika mifano hii, majina *paka, ng'ombe,* na *panya* yangekuwa katika ngeli moja kwani ni majina ya vitu vyenye uhai ambavyo huwekwa katika ngeli ya A/WA.

Wanafunzi wakiwa na uwezo wa kubaini mfumo huu wa lugha ya Kikisa kuwa majina mengi ya mkopo yanawekwa aghalabu katika ngeli ya I/TSI basi itakuwa rahisi kwa wao kubeba dhana hiyo na kuitumia kujifunza kwa urahisi hali ya Kiswahili Sanifu kuyaweka maneno mkopo aghalabu katika ngeli ya I/ZI. Hii itakuwa sehemu mojawapo ya athari chanya za Kikisa kwa Kiswahili Sanifu.

### 3.8 Sababu za Ufanyaji Makosa

Kutokana na tathmini ya makosa yaliyopatikana katika data iliyopatikana nyanjani, baadhi ya sababu zilizobainishwa kama chanzo cha ujitokezaji wake ni kama ifuatavyo:

### *3.8.1 Uhawilishaji Hasi*

Makosa haya hutokea pale mwanafunzi wa lugha ya pili anatumia mfumo wa lugha ya kwanza kuunda sentensi. Makosa mengine yanayofanywa na wanafunzi ni kukosa kufuata mfumo wa kimofolojia na kisintaksia wa Kiswahili Sanifu unaokubalika kutokana na uhawilishaji wa fonimu wa moja kwa moja kutoka Kikisa. Sentensi zifuatazo ni mfano wa makosa haya:

**(30)** 1. Nilinyamaza *nisijua* la kusema. (nisijue)

2. Kila mtu *ako na* nia njema (ana)

3. Tulienda *kukula* samaki *kukubwa* (kula, kubwa)

Sentensi ya pili inaonyesha makosa ambayo hutokana na mfumo wa mazungumzo ya Kikisa ambapo *ali (*ako) hufuatwa moja kwa moja na *nende (na)*. Hivyo basi sentensi: *ali nende lienya lilayi* inatafsiriwa pamoja na mfumo wake vivyo hivyo kuwa *ako na nia njema*. Hali kama hii inapotosha. Hali hii inakuwa sehemu ya makosa yanayosababishwa na athari za Kikisa kwa Kiswahili Sanifu. Sentensi hizi zinaweka wazi mfumo wa matumizi ya maneno katika Kikisa lakini ambao ni tofauti na Kiswahili na hivyo kupelekea ubebaji wa mfumo huo kuwa athari hasi za Kikisa kwa Kiswahili.

Sentensi hizi zinaonyesha mifumo mbalimbali ya uhawilishaji wa fonimu hasi na wa moja kwa moja kutoka lugha ya Kikisa hadi katika Kiswahili Sanifu. Sentensi ya 1 inaonyesha makosa ya kimofolojia yanayotokana na mwanafunzi ambaye Kikisa ni lugha yake ya kwanza na hivyo kuathiriwa kutokana nayo. Neno la Kikisa lenye maana ya *jua* ni *manya* huku neno la kutojua likiwa '*shimanya tawe'* (si-*jua (sijui)* kutokana na mfumo huu tunaweza kueleza hali kama hii kuwa mfumo anaoubeba mwanafunzi huyu ili kurahisisha uundaji wake wa sentensi katika Kiswahili. Hali hii inasababishwa na mfumo uliozoeleka wa kimatamshi katika Kikisa.

### *3.8.2 Ujumlishaji Mno*

Haya ni makosa yanayotokea pale mwanafunzi wa lugha ya pili anapotumia kwa kupindukia sheria au kanuni moja ya kisarufi na hivyo kuishia kuunda mifumo isiyokubalika katika lugha husika. Kanuni au sheria zinazotumika katika Kiswahili Sanifu hufunzwa wanafunzi kabla ya wao kujua jinsi ya kuzungumza Kiswahili Sanifu chenyewe. Upataji wa kanuni unawasaidia sio tu kujua maneno ya Kiswahili Sanifu bali pia mpangilio wa maneno hayo katika lugha hii. Hata hivyo,

wakati wa uelewaji wa sarufi ya Kiswahili Sanifu, hutokea kanuni sahili ambazo wanafunzi huzijumuisha ili kurahisisha uzungumzaji wao.

| **(31)** | **makosa** | **sahihi** |
|---|---|---|
| | Mada yatakayozungumzwa | Mada zitakazozungumzwa |

Katika mfano 31, kwa kuwa maneno mengi yanayopata wingi wake kwa kiambishi ‘ma‘ yanawekwa katika ngeli yenye kiambishi cha wingi *ya*, mjifunzaji anajumlisha katika maneno yote likiwemo neno hili ‘mada‘ ambao ni uelewa wa kupotosha. Swala hili laweza kuelezwa pia kama makisio yasiofaa ya dhana husika.

**(32)** *Wanakijiji wamesababisha maji kuwa chafu (machafu)*.

Neno ‘machafu’ linatumika pia kama neno mkopo katika lugha ya Kikisa na hivyo mwanafunzi anashindwa kulitumia kwa kutaka kumakinika zaidi katika matumizi ya lugha ya pili. Pia kwa kufunzwa kuwa neno ‘safi’ ambalo ndilo kinyume cha ‘chafu’ haliongezwi kiambishi awali ili kuafikia upatanifu wa kisarufi, mjifunzaji wa Kiswahili anajumlisha kanuni hii hadi katika kivumshi ‘chafu’ na hivyo kuepuka kukipa kivumishi hicho kiambishi awali.

***3.8.3 Umakinifu Kupindukia***

Ifuatayo ni data iliyopatikana nyanjani na iliyobainishwa makosa yake kusababishwa na umakini zaidi wakati wa kutamka baadhi ya vitamkwa:

*3.8.3.1 Ubadala wa /s/ > /z/*

| **(33)** | **makosa** | **sahihi** |
|---|---|---|
| | [zima] | [sima] |
| | [walizɛma] | [walisɛma] |
| | [zana] | [sana/ |

*3.8.3.2 Ubadala wa /k/ > /g/*

| **(34)** | **makosa** | **sahihi** |
|---|---|---|
| | [niliɔgɔlɛwa] | [niliɔkɔlɛwa] |
| | [gamba] | [kamba] |

| | | |
|---|---|---|
| | [ganda] | [kanda] |

*3.8.3.3 Ubadala wa /ʧ/ > /ɟ/*

| | | |
|---|---|---|
| **(35)** | **makosa** | **sahihi** |
| | [ɟuba] | [ʧupa] |
| | [ɟumba] | [ʧumba] |
| | [ɟaɲga] | [ʧaɲga] |

*3.8.3.4 Ubadala wa /p/ > /b/*

| | | |
|---|---|---|
| **(36)** | **makosa** | **sahihi** |
| | [bata] | [pata] |
| | [bɔkɛa] | [pɔkɛa] |
| | [badiliʃa] | [batiliʃa] |

*3.8.3.5 Ubadala wa /s/ > /z/*

| | | |
|---|---|---|
| **(37)** | **makosa** | **sahihi** |
| | [matuzi] | [matusi] |
| | [mikɔzi] | [mikɔsi] |
| | [mzaada] | [msaada] |

*3.8.3.6 Ubadala wa /ʃ/ > /zw/*

| | | |
|---|---|---|
| **(39)** | **makosa** | **sahihi** |
| | [utapitizwa] | [utapitiʃwa] |
| | [alipizwa] | [alipiʃwa] |
| | [pigizwa] | [pigiʃwa] |

*3.8.3.7 Ubadala wa /t/ > /d/*

| | | |
|---|---|---|
| **(40)** | **makosa** | **sahihi** |
| | [umɛdubu] | [umɛtubu] |
| | [naðari] | [naθari] |
| | [duɲga] | [tuɲga] |

*3.8.3.8 Uchopekaji Fonimu /h/*

| | | |
|---|---|---|
| **(41)** | **makosa** | **sahihi** |
| | [natumahi] | /natumai/ |

Kutokana na utambuzi wa makosa yanayoweza kufanyika kwa kuhawilisha mfumo wa lugha ya kwanza hadi lugha ya pili, wajifunzaji wa lugha ya Kikisa wanaonekana kuwa makini ili kutofanya makosa. Hili linatokana na semi kuwa lafudhi humtambulisha msemaji, hadhi yake, kiwango cha elimu na hata eneo atokalo. Walio na athari za hali ya juu zaidi huchukuliwa kama wale ambao wana kisomo cha chini na hivyo wanahusishwa na kiwango cha chini cha masomo na hadhi ya chini katika jamii. Hali hii yaweza kuwa ni hali ya kutaka kuonyesha umahiri katika lugha ya Kiswahili ambapo mzungumzaji wa Kiswahili huamua kutilia maanani matamshi bora. Pia, hali hii inaweza kunasibishwa na mazungumzo rasmi na yenye umuhimu ambapo mtu huzingatia matamshi sahihi ya maneno ili kuonyesha utaalamu na kutowachosha hadhira au kuwaudhi kutokana na matamshi mabovu. Hali hii inasababisha umakini zaidi katika mazungumzo na kwa upande mwingine umakini huu hupelekea mzungumzaji wa Kiswahili kuepuka fonimu zozote anazojua ni za lugha ya kwanza ambayo hapa ni Kikisa. Katika mchakato wa kuepuka sauti na fonimu hizo, makosa hufanyika kwani kuna fonimu nyingine ambazo zipo katika lugha zote mbili. Kwa mfano: kwa kutotaka kutamka fonimu /s/ kwa kuhofia ni ya Kikisa, msemaji hujipata akitumia /z/ na hivyo kuharibu maana aliyokusudia kwa kutamka *'naza'* badala ya 'nasa'. Mifano mingine:

| | | |
|---|---|---|
| **(42)** | 1. Matuzi badala ya matusi | (*kuepuka fonimu /s/)* |
| | 2. Juba badala ya chupa | (*kuepuka fonimu /ʧ/ na /p/*) |
| | 3. Nimegwama kwa gari | (*kuepuka fonimu /k/)* |

Vilevile makosa hayajitokezi tu katika kiwango cha sauti au fonimu tu bali pia katika kiwango cha sentensi. Kiwango cha kisintaksia chaweza kuathiriwa na Kikisa kwa namna fulani na hivyo kujitokeza na mfumo wa mpangilio wa maneno usiokubalika katika Kiswahili Sanifu.

| | | |
|---|---|---|
| **(43)** | **makosa** | **sahihi** |
| | Nipatie hiki kitabu. | Nipatie kitabu hiki. |

| | |
|---|---|
| Kula hiki chakula | Kula chakula hiki. |
| Vaa hii nguo. | Vaa nguo hii. |

Tatizo hili linatokea kutokana na kujihadhari kwingi ili kutohawilisha mfumo wa lugha ya Kikisa hadi katika Kiswahili Sanifu. Kwa mfano, kwa sababu katika Kikisa kuna mfuatano wa nomino kuja kabla ya kivumishi, mwanafunzi anabadilisha anapofika katika Kiswahili Sanifu ili kivumishi kianze kabla ya nomino kutajwa.

*3.8.3.8 Makosa Mengine Yanayotokana na kuwa Makini Zaidi*

**(44)** Waliotuma *hudhuru*

Sentensi hii (44) inadhihirisha makosa yanayotokana na mwanafunzi kuwa makini zaidi baada ya kukosa kuweka katika maneno mengine fonimu /h/ ilipohitajika kama vile katika mifano; s*herehe, huzuni*, na *nawasihi*. Wanafunzi wa Kiswahili Sanifu walio wazungumzaji asilia wa Kikisa wanaishia kujumlisha hali hii katika maneno mengine yasiyohitaji fonimu hiyo /h/ au hata fonimu nyinginezo walizotahadharishwa kuzitumia au kutozitumia.

**(45)** *Msitumie maji nyingi (mengi) kupita kiasi inayotakikana (kinachotakikana)*

Katika Kikisa '*a-matsi manji'* ni kauli yenye maana ya 'maji mengi'. Mfuatano huu na uwiano wa maneno wa 'ma' na 'ma' katika nomino na kivumishi ungeonekana kumsaidia mwanafunzi huyu moja kwa moja kuweza kutambua mfuatano na uwiano huo wa kisarufi katika Kiswahili Sanifu. Lakini tofauti na inavyotarajiwa amebuni maneno tofauti ili kuepuka mfumo aliouzoea wa Kikisa. Vivyo hivyo, katika *'inavyotakikana'* na 'kinachotakikana' makosa ya kingeli yanatokana na umakinifu wa kupindukia.

**(46).** *Wanakijiji wamesababisha maji kuwa chafu (machafu).*

Neno 'machafu' linatumika pia kama neno mkopo katika lugha ya Kikisa na hivyo mwanafunzi anashindwa kulitumia kwa kutaka kumakinika zaidi katika matumizi ya lugha ya pili. Pia kwa kufunzwa kuwa neno 'safi' ambalo ndilo kinyume cha 'chafu' haliongezwi kiambishi awali ili kuafikia upatanifu wa kisarufi, mjifunzaji wa Kiswahili anajumuisha kanuni hii hadi katika kivumshi 'chafu' na hivyo kuepuka kukipa kivumishi hicho kiambishi awali.

*i). Ajali *iliotokea*.

*ii). *Tueze* kushinda yote.

Katika mfano wa (i), mwanafunzi anajaribu kuwa makini zaidi ili asitumie mfumo wa Kikisa. Kutokana na ukweli kuwa Kikisa pia kina o-rejeshi (yo) anaamua kutumia /o/ badala ya *yo*. Mfano wa (ii), unaonyesha hali tofauti ambapo mwanafunzi anaamua kuacha nje /w/ ambao si mfumo wa Kikisa wala Kiswahili. Hali hii inaendeleza haipothesia kuwa si makosa yote yanayofanywa na wanafunzi hutokana na athari za lugha ya kwanza bali yapo maswala na masiala mengine kama vile mazingira anamokulia mwanafunzi, lugha wanayotumia vijana katika vikundi vyao, umakini alio nao mwanafunzi wakati wa kuandika miongoni mwa mengine. Hali hii ni zao la Lugha Kati ambayo ina sifa zisizo za Kikisa wala Kiswahili Sanifu.

**(47)** *Maiti **ambao** hawajulikani watokako nimetenga mahala pao ambapo **yatazikwa***

Sentensi hii inatoa ugumu unaojitokeza katika sheria na kanuni za kujifunza Kiswahili Sanifu. Kauli hii ina mkanganyiko wa ngeli jambo ambalo halitarajiwi kutokea kwa mzungumzaji wa lugha yenye asili ya Kibantu na haswa Kikisa ambacho mfumo wake wa ngeli unataka kufanana sana na ule wa Kiswahili. Licha ya kuwa kisemantiki anaona maiti kama watu na hivyo kutumia urejeshi unaoambatishwa kwa ngeli ya A /WA, anagundua tena ni kama maiti ni kitu kisichokuwa na uhai na kubadili ngeli hadi LI/YA. Hali kama hii imejitokeza sana katika mazungumzo na maandishi mengi kwani swala la ngeli za maneno mengine kama vile *maiti* zina utata unaotokana na hali ya Kiswahili kuweka makundi ngeli yake kisemantiki haswa katika ngeli ya A/WA. Hali hii pia yaweza kuelezwa kwa kuihusisha na athari za Kikisa kwa lugha ya mwanafunzi huyu. Katika Kikisa hakuna neno la moja kwa moja lenye maana ya maiti. Katika utamaduni wa Wakisa aliyefariki hurejelewa kwa jina lake na hivyo kusalia katika ngeli ya watu au hurejelewa kama *mwili* ambao sasa huingia kama nomino ya ngeli tofauti yenye nomino ya mwili/miili na sio A/WA. Hata hivyo, si rahisi neno mwili kutumika bali jina la aliyeaga dunia na hivyo kumuacha katika viumbe vyenye uhai katika ngeli moja na watu walio hai. Mkorogano wa mambo haya humchanganya mjifunzaji wa Kiswahili na kupelekea utoaji wa sentensi kama hizi.

**(48).** Nilianza *kusikia* baridi.

Sentensi hii inaonyesha dhana inayopatikana katika tamaduni za lugha zote mbili lakini zina istlahi tofauti za kurejelea hali hiyo. Dhana ya 'kuhisi baridi' ipo katika Kiswahili na hata Kikisa lakini katika Kikisa kusikia na kuhisi zinarejelewa kwa istlahi moja tu: kusikia. Ni kutokana na hali hii

ambapo mwanafunzi kwa kuathiriwa na Kikisa anajipata akihawilisha sentensi *euliranga (nasikia) obushindu (baridi)* moja kwa moja hadi katika Kiswahili na hivyo kujipata na sentensi 'nasikia baridi' ambayo katika Kiswahili itapoteza maana yake, maana 'kusikia' kunachukuliwa kuwa mchakato unaopitia katika masikio tu.

Mifano 47 na 48 inaonyesha umuhimu wa uelewa wa utamaduni wa wajifunzaji wa lugha ya pili kabla na wakati wa ufundishaji wa lugha hiyo ya pili na dhana zake. Kupitia uelewa wa utamaduni pamoja na lugha ya kwanza ya mjifunzaji, anayefundisha lugha ya pili anaweza kubaini changamoto hizi mapema na hivyo kubuni mikakati ya kuzikabili wakati wa ufundishaji.

### *3.8.4 Makosa Yasio na Msingi wa Kikisa*

#### *3.8.4.1 Udondoshaji wa /a/*

| | makosa | sahihi |
|---|---|---|
| **(49)** | **makosa** | **sahihi** |
| | [nja] | [njaa] |

#### *3.8.4.2 Udondoshaji wa /ma/*

| | | |
|---|---|---|
| **(50)** | **makosa** | **sahihi** |
| | [tukaandama] | [tukaandamana] |

#### *3.8.4.3 Udondoshaji wa /h/*

| | | |
|---|---|---|
| **(51)** | **makosa** | **sahihi** |
| | [nawasii] | [nawasihi] |
| | [uzuni] | [huzuni] |
| | [ili] | [hili] |

#### *3.8.4.4 Udondoshaji wa Silabi /hɛ/*

| | | |
|---|---|---|
| **(52)** | **makosa** | **sahihi** |
| | /shɛrɛkɛa/ | /shɛrɛhɛkɛa/ |

#### *3.8.4.5 Udondoshaji wa /w/*

| | | |
|---|---|---|
| **(53)** | **makosa** | **sahihi** |
| | [kukua] | /kuwa/ |
| | [kuʧukua] | /kuʧukuwa/ |

*3.8.4.6 Uchopekaji wa /ɔ/ na /y/*

| (54) | **makosa** | **sahihi** |
|---|---|---|
| | [iliyɔɔngɔjɛwa] | [iliyɔngɔjwa] |
| | [washangayɛ] | [washangaɛ] |

*3.8.4.7 Udondoshaji wa /n/*

| (55) | **makosa** | **sahihi** |
|---|---|---|
| | [lɛgɔ] | [lɛngɔ] |

*3.8.4.8 Uchopekaji wa /n/ na /m/*

| (56) | **makosa** | **sahihi** |
|---|---|---|
| | [bandɔ] | [badɔ] |
| | [wanasubukana] | [wanasumbukana] |
| | [alijimbiwa] | [alijibiwa] |
| | [Mkumbwa] | [mkubwa] |

*3.8.4.9 Ubadala wa /i/ > /u/*

| (57) | **makosa** | **sahihi** |
|---|---|---|
| | [kunyunyuzia] | [kunyunyizia] |

Makosa haya yamejitokeza katika insha za wanafunzi lakini hayadhihirishi uwepo wa athari zozote za Kikisa kwani maneno husika hayana sifa zozote za kileksia au kimuundo zinazotokana na Kikisa.

### 3.9 Makosa ya Kawaida

Burt & Kiparsky (1972) wanafafanua kuwa, makosa ya kawaida ni aina ya makosa ambayo hutokea katika miundo ya lugha ya pili ya sentensi na haiathiri uelewa au kuwa kizingiti cha mawasiliano licha ya sentensi kutokuwa sawa kimuundo. Sintaksia ni tawi la isimu linalojishughulisha na jinsi maneno ya lugha husika yanavyopangwa ili kuunda sentensi. Sintaksia kama taaluma hujihusisha na mahusiano ya maneno katika sentensi. Hivyo basi, makosa ya kisintaksia ni makosa yanayotokea kutokana na utumizi mbaya wa maneno katika sentensi. Makosa yafuatayo yanaenda kinyume na sintaksia ya Kiswahili ila maana haibadiliki.

| | | |
|---|---|---|
| **(58)** | **makosa** | **sahihi** |
| | Naenda hapana. | Siendi. |
| | Niliiba hapana. | Sikuiba. |
| | Alipiga mimi. | Alinipiga. |

Hali kama hii hutokana na mfumo wa sintaksia wa lugha ya Kikisa. Katika Kikisa, lipo neno zima la kuonyesha kupinga au hali ya ukanusho kwa mfano:

| | | |
|---|---|---|
| **(59)** | 1. *nditsa* ***tawe*** | (Sitakuja) |
| | 2. *Shimanyire* ***tawe*** | (sijui) |

Neno *'tawe'* hapa linatumika kuonyesha ukanusho au kupinga au kukataa jambo fulani. Mzungumzaji wa Kikisa akishazoea mfumo huu anajipata kila mara akiuhawilisha moja kwa moja hadi lugha ya pili atakayojifunza ambapo katika muktadha huu ni Kiswahili Sanifu. Katika mifano hii, mfano wa 1 na wa 2, aliyeathirika kwa uhawilishaji huu wa moja kwa moja atasema:

| | | |
|---|---|---|
| **(60)** | 1. *nditsa tawe* | ( nitakuja hapana) |
| | 2. *Shimanyire tawe* | (najua hapana) |

Kisaikolojia anaona lazima yawe maneno mawili. Na kwa sababu amefunzwa kuwa '*hapana'* lina maana ya *kukataa* au *kupinga* basi analiweka moja kwa moja. Mifano mingine ni kama vile:

| | | |
|---|---|---|
| **(61)** | **makosa** | **sahihi** |
| | samaki *moja* | samaki mmoja |
| | ng'ombe *za* watu | ng'ombe wa watu |
| | *mashule mingi* | shule nyingi |

Makosa haya yamechanganyika yakiwemo ya ngeli, urudiaji wa dhana kama vile dhana ya 'ndani ya', namna isiyosahihi ya wingi na umoja ambayo ni hali inayoletwa na athari za Kikisa pale kuna viambishi vya wingi vinavyowekwa kwenye neno hilo katika Kikisa lakini neno lenye maana sawa la Kiswahili Sanifu halichukui viambishi vya umoja na wingi, tofauti za ngeli zinazosababishwa

na maneno kuwa katika ngeli mbili tofauti katika Kikisa ilhali katika Kiswahili Sanifu yanapatikana katika ngeli moja.

Sentensi kama vile *Samaki moja* inaletwa na kuwa katika Kikisa neno linalorejelea idadi 'moja' si lazima liwe na kiambishi. Ngeli ya neno ng'ombe inaonekana kuwatatiza wanafunzi wengi kutokana na kuwa 'ng'ombe' ni mnyama aliye katika ngeli tofauti na ile ya wanadamu katika Kikisa huku katika Kiswahili Sanifu 'ng'ombe' ni nomino inayowekwa katika ngeli ya A/WA sawa na viumbe vingine vyenye uhai akiwemo binadamu.

### 3.10 Makosa ya Kileksika

Yapo makosa ya matumizi ya leksemu ambazo si mwafaka kutumika katika sehemu zilipotumika. Kwa mfano:

**(62)** 1. Mama *alinimwagia* chai kwa kikombe.

Makosa haya yamefanywa kwa kutofuata kikamilifu kanuni zote za Kiswahili Sanifu kwani tofauti hii ipo hata katika lugha ya Kikisa.

**(63)** *Sundula (mwaga) tsukha (tia)*

1. Nitilie chai (nzushila ichai)

2. Mwaga chai (sundula ichai)

Maana ya mwaga ni 'sundula' katika Kikisa na 'tia' ni '*tsukha*' katika Kikisa. Maana zake zinafanana kabisa na tofauti zake ni zile zile zinavyojitokeza katika Kiswahili. Hivyo basi, swala la kuwa hali hii inatokana na ukosefu wa maana mwafaka katika Kikisa halipo. Swala kuwa 'kumwaga' na 'kutia' vina maana sawa katika Kikisa halipo vilevile. Huu ni ukosefu wa kutilia maanani sheria za leksimu za lugha ya pili kikamilifu.

### 3.11 Hitimisho

Sura hii imejaribu kubainisha makosa yanayofanywa na wanafunzi na kutoa baadhi ya sababu za upatikanaji wa makosa hayo. Makosa yamejitokeza kuwa mengi katika insha za watafitiwa kiasi cha kwamba utafiti huu unaonekana muhimu sana na wa msaada kwa wakuza mtaala, walimu na hata wanafunzi kama tulivyodokeza awali.

Makosa yamebainika kuwa ni ya aina aina. Makosa mengine yanafanywa kutokana na watafitiwa kutojua kuandika vizuri au hata kutojua neno au mfumo kamili wa kutumia. Hali hii inatokea kutokana na mchanganyiko wa maneno na mifumo akilini mwa watafitiwa kufuatia lugha yao ya kwanza na ya pili. Makosa yaliyojitokeza ni ya aina mbili; makosa yanayotokana na athari za lugha ya kwanza na makosa yasio na msingi wowote wa lugha ya kwanza tuliyoishughulikia yaani Kikisa. Uwepo wa asilimia kubwa ya makosa kama makosa yanayohusishwa na athari za Kikisa kunadhihirisha umuhimu wa utafiti wa makosa haya kuchukuliwa kwa uzito na mikakati kuwekwa ili kuwasaidia walimu pamoja na wanafunzi kusuluhisha changamoto hizo za ujifunzaji.

Makosa mengine yamebainika kuwa nje ya athari zinazoweza kutajwa kama za Kikisa kwa Kiswahili Sanifu. Makosa haya yanaonyesha kuwepo kwa masiala na masuala mengi yanayoweza kuathiri ujifunzaji wa wanafunzi wa lugha ya pili haswa Kiswahili. Kuwepo kwa vijilugha vingine kwaweza kusababisha hali hii. Hata hivyo, uwepo wa wanafunzi katika shule zilizo katika maeneo ya wazungumzaji wa Kikisa si sababu tosha ya kuthibitisha kuwa wanafunzi hao wanazungumza Kikisa kama lugha yao ya kwanza. Huenda wengine wakawa wamesafiri kutoka maeneo mengine ya nchi ambako wamejifunza lugha tofauti na Kikisa kama lugha ya kwanza na hivyo Kiswahili chao kuathiriwa na lugha hizo husika na wala si Kikisa.

Makosa yaliyobainishwa katika sura hii ni makosa ya kisarufi yanayohusiana na lugha na miundo yake na makosa ya kimuktadha yanayoendelea kwa vipengele zaidi ya sarufi. Sura hii inaangazia aina hizi zote za makosa ili kubaini makosa yanayofanywa katika kujifunza kwa vipengele vya sarufi kama vile fonimu na mofimu zinazounda maneno. Pia, sura hii imefafanua jinsi sheria za uundaji wa sentensi zinavyoweza kufanikisha uundaji wa sentensi sahihi palipo na ufasiri mwema na zisizo sahihi kimuktadha palipo na ufasiri wa kukanganya kimaana.

Ubainishaji na uchambuzi huu wa makosa katika sura hii ni muhimu kwani umewezesha kubaini, kufafanua na kutabiri ruwaza na miundo ya maneno inayoweza kuleta utata na changamoto katika ujifunzaji wa lugha ya pili. Kubainishwa na kuchanganuliwa kwa makosa yafanywayo na wanafunzi kama ilivyofanywa katika sura hii, kunakuza na kuboresha hali ya ufunzaji na ujifunzaji wa Kiswahili kupitia kubuni mbinu za kupunguza vikwazo vya ujifunzaji wake. Hivyo basi, sura hii ina umuhimu mkubwa katika kuupa utafiti huu manufaa makubwa kwa wakuza mtaala wa elimu, walimu na hata wanafunzi wa Kiswahili kama lugha ya pili.

# Sura ya 4

# Kueleweka na Kutokueleweka kwa Maana

## 4.1 Utangulizi

Sura hii inaendeleza mjadala kuhusu makosa yanayotekelezwa na watafitiwa kutokana na athari za Kikisa kwa uzungumzaji na uandishi wa Kiswahili Sanifu. Makosa haya kama yalivyojitokeza katika sura ya tatu ni yenye athari kubwa kwa ufanikishaji wa mawasiliano. Makosa haya ni muhimu kutambuliwa kwani ni kupitia kwa utambuzi wake ambapo yanaweza kuangaziwa na kutafutiwa suluhu.

Sura hii inayajadili makosa yaliyobainishwa katika sura ya tatu na aina zake ili kutathmini ni vipi makosa hayo na aina zake yanatatiza mawasiliano. Isitoshe, sura hii inatathmini uwezekano wa kutokea makosa ambayo licha ya kuwepo katika neno, sentensi au usemi hayatatizi uelewa wa msikilizaji na msomaji wa alichokisema mzungumzaji au mwandishi. Sura hii pia inalenga kutathmini makosa ambayo yamefanywa na watafitiwa na ambayo kwa kiasi kikubwa yanapotosha maana lengwa kutoka kwa msemaji.

Makosa yasiyo na msingi katika athari za Kikisa kwa mzungumzaji wa Kiswahili yamejadiliwa katika sura hii ili kuonyesha mchakato wa uathirianaji na mambo anuwai yanayoweza kusabibisha athari. Makosa haya ni muhimu kuchanganuliwa kwani yanatoa picha kamili ya aina za wanafunzi wanaopatikana shuleni kwa wakati huu ambapo si moja kwa moja kuwa kuna sehemu ya wanafunzi wanaozungumza lugha moja ya kwanza bila athari kutoka kwa lugha nyingine. Isitoshe, makosa hayo yametusaidia kuonyesha ugumu uliopo wa kujifunza Kiswahili Sanifu hasa katika mazingira ambamo vijana wameweza kubuni ‘aina’ yao ya Kiswahili ambacho kinawawezesha kuelewana na kujitambulisha kama kikundi tofauti na watu wengine.

Sura hii inayaangalia makosa yaliyofanywa na wanafunzi kiasilimia ili kubaini ni kiasi gani cha watafitiwa wanaofanya kila aina ya makosa na kupata sababu zake. Kupitia asilimia hizi inaweza kubainika kikundi wakilishi cha watafitiwa kinachofanya makosa fulani mahsusi mara kwa mara na aina ya makosa yanayofanywa zaidi. Hali iwapo hivi, mchakato huu wa Uchanganuzi wa Makosa utakuwa wa manufaa zaidi kwa walimu na wanafunzi wa lugha ya pili haswa Kiswahili Sanifu walio wazungumzaji asilia wa Kikisa.

### 4.2 Idadi na Asilimia za Makosa

Makosa yaliyochanganuliwa yameonyeshwa katika jedwali lifuatalo ambapo kila kauli imepewa nambari yake mahsusi.

| **kikundi cha makosa** | **kadirio la makosa** | **kauli** | **kodi** |
|---|---|---|---|
| 0 | hakuna makosa | vyema | 0 |
| 1-2 | makosa machache zaidi | vizuri sana | 1 |
| 3-4 | makosa machache | vizuri | 2 |
| 5-6 | makosa wastani | wastani | 3 |
| 7-8 | makosa mengi | vibaya | 4 |
| zaidi ya 9 | makosa mengi zaidi | vibaya sana | 5 |

Insha tulizozisoma zilikuwa na viwango tofauti vya makosa yanayodhihirisha athari za Kikisa katika Kiswahili. Baada ya kusoma kwa makini insha za wanafunzi wa shule tulizozichagua, makosa yanayodhihirisha athari za Kikisa kwa Kiswahili Sanifu yalijitokeza kama ifuatavyo:-

| **kikundi** | **kadirio la makosa** | **kodi** | **asilimia** |
|---|---|---|---|
| 0 | hakuna makosa | 0 | 0 |
| 1-2 | makosa machache zaidi | 1 | 4 |
| 3-4 | makosa machache | 2 | 36 |
| 5-6 | makosa wastani | 3 | 52 |
| 7-8 | makosa mengi | 4 | 79 |
| zaidi ya 9 | makosa mengi zaidi | 5 | 39 |

Idadi kubwa ya makosa yamejitokeza kuwa zaidi ya 5 na chini ya 8. Takwimu hizi za makosa zinaonyesha kuwa zipo athari chanya za Kikisa katika Kiswahili zinazohusu kupata muundo sahihi

wa maneno na mfumo wa Kiswahili Sanifu. Athari hizi chanya zinapunguza idadi ya makosa yanayojitokeza.


Utafiti huu ulihusisha shule za upili na za msingi na data iliyopatikana ilionyesha idadi ya makosa kama ifuatavyo:

| **shule** | **idadi ya makosa** | **asilimia** |
|---|---|---|
| shule za msingi | 97 | 54.2 |
| shule za upili | 82 | 45.8 |

Asilimia kubwa ya makosa yalifanywa na wanafunzi wa shule za msingi. Data hii inaonyesha kuwa wanafunzi wanaokuwa na athari wasipofuatiliwa kwa makini huendeleza athari zao hata katika shule za upili na hivyo kuweka uwezekano wa kuathirika hata katika mazungumzo na maandishi yao baada ya maisha ya shuleni. Asilimia kubwa ya makosa yaliyofanywa na wanafunzi wa shule za msingi yanaonyesha kuwa wanafunzi hawa wangali wageni kwa lugha hii kwani wamejifunza kwa muda mchache, kigezo ambacho ni muhimu katika kukadiria uelewaji na ufikiaji wa uwezo wa mzungumzaji mzawa wa lugha ngeni na hivyo kusababisha ufanyaji wa makosa mengi (Ringbom 1987, James 1971). Makosa mengine yametokana na hoja kuwa wanafunzi wengine wana shida za kuandika vizuri maneno na hivyo kuwa katikati ya kujifunza lugha na kujifunza kuandika. Katika hali kama hii hatuwezi kutaja moja kwa moja kuwa makosa yao yote yanatokana na athari hasi za Kikisa kwa umilisi wao wa Kiswahili Sanifu.

Chati ifuatayo inaonyesha idadi ya makosa ya kila kipengele cha kisarufi kwa namna kilivyojitokeza:-

**Makosa ya Kisarufi**




Makosa ya kifonolojia yamejitokeza kama yaliyo mengi pale sauti zinabadilishwa au kuongezwa na hivyo kupotosha matamshi sahihi ya neno husika. Hata hivyo, makosa hayo ya kifonolojia pia ni makosa yaliyopelekea kuibuka kwa makosa ya kisemantiki na hivyo kupotosha au hata kupoteza maana iliyodhamiriwa.

## 4.3 Athari za Makosa kwa Mawasiliano

Makosa katika vipengele vyote vya sarufi yamekuwa na athari za kisemantiki kwa maneno husika. Athari hizi za kisemantiki zimeathiri mawasiliano kwa namna tatu ikiwemo maana kueleweka japo kwa matatizo, maana kueleweka tofauti na ilivyodhamiriwa, na maana kutokueleweka kabisa. Katika sehemu hii, tutazijadili hali hizi tatu.

### *4.3.1 Athari za Makosa Zisizoathiri Mawasiliano*

Utafiti huu umetambulisha maneno yasiyo sahihi katika Kiswahili Sanifu na miundo ya sentensi isiyokubalika katika Kiswahili Sanifu inayotokana na athari za Kikisa. Hata hivyo, ipo miundo mingine ya maneno na sentensi iliyoathiriwa lakini maana bado inaeleweka kwa msikilizaji. Yaani, maana aliyonuia kuiwasilisha msemaji inamfikia msikilizaji mahiri wa lugha ya Kiswahili

licha ya muundo wa maneno kuwa na shida za kikanuni. Mifano ya pale mawasiliano hayakatiki kabisa ni kama vile katika sentensi zifuatazo:

**(64)** 1. Siku *iliyoongojewa*

2. Mswada *upitizwe* bungeni

3. Anapenda ku*futa* sigara

Sentensi hizi licha ya kuwa na makosa yanayotokana na athari za Kikisa kwa Kiswahili Sanifu, zinaweza kueleweka na wasikilizaji. Hili linaweza kuelezwa kama mazoea ya kuwasikia watu wakitumia maneno haya au hata mchakato wa kunasibisha neno msikilizaji asilolielewa na neno jingine la karibu linaloweza kuleta maana. Hata hivyo, maneno haya si rahisi kueleweka na mtu aliye mahiri wa lugha ya Kiswahili Sanifu na anayetaka kupata maana ya maneno yanayotumika bila kuzingatia muktadha kwa namna yoyote. Katika hali kama hiyo sentensi kama vile anapenda *kufuta sigara* itamtatiza sana msikilizaji huyu kwani hataelewa ni vipi mtu 'anafuta' sigara na kwa maana gani.

Miundo ya kisintaksia na kimofolojia isiyo sahihi inasababisha mabadiliko yasiokuwa na athari kubwa kwa maana bali kutatizika kwa sheria za lugha ya Kiswahili Sanifu kwa mfano:

**(65)** 1. Michezo *huchangamusha* akili.

2. *Kuzungumuzia* ufisadi.

3. Najua *mumesikia*.

Pia makosa yatokanayo na ngeli huenda yakafikisha maana licha ya kutatiza sarufi.

**(66)** 1. *Makaratasi haya yanapendeza kuandikia*.

2. Kikombe *yangu imepasuka*.

3. Ng'ombe *za jirani zilipigana*.

Makosa ya kisintaksia yanayosababishwa na masuala mbalimbali yakiwemo ngeli, utamaduni, mifumo ya Kikisa na hata umakinifu wa kupindukia na yanaweza kufikisha maana au jumbe zilizokusudiwa. Mifano ifuatayo inasadifu kutokana na data iliyopatikana nyanjani:

**(67)** 1. Sikujua alichotaka kufanyia pesa *hiyo.*

2. Sherehe ya kumuaga babangu *zilifanyika*.

3. Gari *ilikuja* kwa kasi.

Katika mifano hii, sentensi zinaeleweka hata wakati mzungumzaji amekosea. Hali hii inatokana na ukweli kuwa, maneno yaliyokosewa hayana maana nyingine katika Kiswahili Sanifu. Kukosekana kwa maana kamili katika Kiswahili Sanifu kunamsababishia msikilizaji kunasibisha neno hilo na jingine la karibu nalo. Hata hivyo hali hii si ya moja kwa moja.

### *4.3.2 Athari za Makosa Zinazosababisha Kueleweka Vibaya*

Utafiti huu umeweza kubainisha maneno na miundo ya maneno inayoathiriwa na Kikisa na hivyo neno husika kupata maana tofauti na ile iliyonuiwa na msemaji. Hali kama hii hukatisha mawasiliano na kusababisha watu kukosa kuelewana. Hali hii aghalabu hutokea wakati neno lililoathiriwa na Kikisa ama kwa kuongezwa au kupunguzwa fonimu au silabi zake linakuwa na maana tofauti katika Kiswahili Sanifu. Sentensi zifuatazo na zitokanazo na data iliyopatikana nyanjani ni mifano ya hali hii:

**(68)** 1. Swala la *ubakaji* linaendelea vizuri kama tulivyopanga.

2. *Wasasi* walikutana uwanjani.

3. Tuliingia kwa *paa* na kujificha.

Sentensi hizi zinaonyesha utata uliopo katika ujitokezaji wa athari za Kikisa katika mawasiliano yahusisha Kiswahili Sanifu. Sentensi ya kwanza inatolewa na msemaji wakati akiwahutubia wazazi shuleni. Msemaji anataka kuwajulisha kuhusu kazi nzuri inayofanyika shuleni humo ya kupaka rangi majengo ya shule lakini kutokana na athari za Kikisa kwa Kiswahili chake anaishia kutoa kauli ambayo huenda ikazua hisia hasi na kukasirisha sana hadhira yake. Maana anayotaka kufikisha msemaji huyu inatatizika na kueleweka vibaya kwani huku akimaanisha kuwa wanafanya kazi nzuri ya kunadhifisha majumba kwa kuyapaka rangi, maana inapotoka na kuonekana kama anayefurahia na hata kupanga uendelezwaji wa unyama wa kubakwa kwa watoto wa wazazi anaohutubia.

Sentensi ya pili inatolewa na msemaji ili kueleza kuwa watu waliokutana uwanjani walikuwa wazazi wa wanafunzi lakini kauli yake inatekwa na athari za Kikisa kwa Kiswahili na hivyo kuonekana kama anayezungumzia wasasi wanaowinda kama kazi yao ya kila siku. Maana inapotoka kwani watu hawa wote wawili, wazazi na hata wasasi, wanaweza kukutana uwanjani kujadili maswala yao. Hivyo basi maana inaweza kwenda pande zote mbili lakini ikampoteza msikilizaji kutoka kwa maana iliyokusudiwa na hivyo kueleweka lakini vibaya.

Sentensi ya tatu inazungumzia kuingia paa kwa ajili ya kujificha. Msemaji anajaribu kueleza jinsi walivyomwona mtu, kisha ili kujificha, wakaingia kwenye baa kunakouzwa vileo. Anapojipata akitumia neno ‘paa’ inakuwa hali tata na tofauti na lengo lake la kutumia neno hilo kwani ‘paa’ hapa inaeleweka kwa msikilizaji mahiri wa Kiswahili Sanifu kama kuwa waliingia ‘sehemu ya juu ya nyumba’ yaani kisusi huku msemaji akiwa na maana ya ‘mahali pa burudani’.

Sentensi hizi tatu zinawakilisha utata mkubwa unaojitokeza wakati athari za Kikisa zinapojitokeza katika mawasiliano ya Kiswahili. Neno linaloonekana au kusikika linakuwa na maana tofauti na iliyokusudiwa na mzungumzaji. Kueleweka vibaya huku kunatokana na hali kuwa maneno yaliyodhamiriwa hayakutamkwa na yaliyotamkwa au kuandikwa badala yake yakawa na maana tofauti katika Kiswahili Sanifu. Kwa mfano, neno ‘baka’ lilipotumika badala ya ‘paka’ linazua maana nyingine katika Kiswahili Sanifu na ambayo ni hasi katika muktadha huo. Neno ‘wazazi’ linapokosewa na ‘wasasi’ kuchukuwa nafasi yake maana inabadilika kwani neno hilo lina maana tofauti katika Kiswahili Sanifu. Neno lililonuiwa ‘baa’ halijitokezi katika maandishi wala mazungumzo na hivyo neno ‘paa’ linabadilisha maana na hivyo kueleweka kivingine na alivyodhamiria mzungumzaji anayetoa kauli husika.

Kueleweka vibaya kwa maana iliyokusudiwa hutokea aghalabu kutokana na athari ambazo husababisha kutajwa kwa neno au kuandikwa kwa neno ambalo lina maana yake tofauti katika Kiswahili Sanifu. Hili hupelekea maana ile nyingine kueleweka vizuri kwa msikilizaji huku msemaji akiwa na maana tofauti isiyo karibu na maana hiyo katika akili za msikilizaji. Hata hivyo, utata huweza kutokea kwa msikilizaji wakati muktadha ambamo neno husika limetumika unakanganya. Kwa mfano:

**(69)** T*uliingia kwa paa na kuagiza vinywaji*.

Sentensi hii itamkanganya msikilizaji kwani itakuwa vigumu kwake kuelewa inakuwaje watu waingie sehemu ya juu ya nyumba na kujiburudishia kule. Hata hivyo, wanaagiza vinywaji kutoka kwa nani na mbona vinyaji hivyo viwe kule juu ni maswali yatakayomtatiza msikilizaji. Katika hali hii, neno 'paa' limeeleweka kwa maana yake ya Kiswahili Sanifu kinyume na alivyokusudia kusema msemaji. Hata hivyo, muktadha hauruhusu uelewa huo. Hivyo basi, mkanganyiko wa kuelewa sentensi hii unamwacha msikilizaji na maswali si haba.

### *4.3.3 Athari za Makosa Zinazosababisha Kutokueleweka Kabisa*

Hali hii hutokea wakati maneno yanayotumiwa na msemaji hayapatikani katika msamiati wa Kiswahili Sanifu. Hapa ni pale ambapo mzungumzaji anatumia maneno kwa kuathiriwa na lugha ya kwanza ya Kikisa na ambayo hayana maana nyingine katika Kiswahili Sanifu. Uhawilishaji wa fonimu za Kikisa katika Kiswahili unasababisha ugumu kwa msikilizaji kulinasibisha neno hilo na neno jingine lolote la Kiswahili. Hadhira inapokuwa ya wajifunzaji au wanafunzi yapo mazoea ya kudhani kuwa mwalimu wao anatumia maneno mapya ilhali ni yale yale yaliyo katika Kiswahili wanachokijua. Hali kama hii itakosesha mawasiliano na hivyo ujifunzaji wa lugha hii kwa wanafunzi unakosa kuwepo. Wanafunzi huenda wakaiona lugha hii kuwa ngumu na hivyo kusababisha mielekeo hasi. Sentensi zifuatazo na zilizotokana na data tuliyoipata nyanjani ni mifano ya hali hii:

**(70)** 1. *Tulimuusa* ng'ombe wetu.

2. Alipiga *hoti*

3. *Amepatana na mchusi*

Maneno haya *'usa' 'hoti'* na *'mchusi'* hayana maana kamili katika Kiswahili Sanifu. Jambo hili linafanya maana isieleweke kabisa katika sentensi hizi. Msikilizaji hawezi kuelewa sentensi hizi kutokana na kuwa hawezi kuunganisha maana kutoka kwa maneno yanayounda sentensi zenyewe. Hivyo basi, maana hukosa kueleweka kabisa wakati neno linalotumiwa na msemaji halieleweki au halina maana bayana katika Kiswahili Sanifu.

## 4.4 Makosa ya Kiathari na Makosa Yasiyotokana na Athari za Kikisa

Kuna idadi kubwa ya makosa yaliyofanywa na watafitiwa yaliyo na misingi ya athari za Kikisa kwa Kiswahili kuliko makosa yasiyohusika na athari hizo za Kikisa. Hali hii inaonyesha kuwa,

makosa yanayotokana na athari za lugha ya kwanza (Kikisa) ni mengi. Hali hii inamulika umuhimu uliopo wa kutathmini lugha ya kwanza katika ujifunzaji wa lugha ya pili. Ikiwa makosa ya athari za lugha ya kwanza kwa lugha ya pili kama vile Kikisa kwa Kiswahili yataweza kubainishwa na kufafanuliwa kama utafiti huu unavyofanya, itakuwa rahisi kutafuta suluhu na hivyo asilimia kubwa ya makosa yanayofanywa katika mazungumzo na insha za wanafunzi yataweza kukabiliwa na hivyo kufanikisha upokeaji wa lugha ya pili bila matatizo.

Uwepo wa makosa yasiyotokana na athari za Kikisa kwa Kiswahili unaweza kuashiria uwepo wa maswala na masiala mengi yanayoathiri upokeaji wa lugha ya pili mbali na lugha ya kwanza. Kwa mfano, vijana wengi wanazungumza vijilugha ibuka na hivyo huenda ikawa na athari fulani kwa mazungumzo yao na matumizi yao leksemu na miundo yake huku vijilugha ibuka hivi vikiwa si lugha yao ya kwanza.

Uwepo wa makosa haya yasiyotokana na athari za lugha ya kwanza pia unaweza kudokeza jambo kuhusu makosa kuweza kutokea sio tu kwa athari za lugha ya kwanza bali pia kwa masiala ya kiuanafunzi kama vile uvivu, kutojua kuandika vizuri, kutokuwa makini anapoandika mwanafunzi, kuwa na wasiwasi wa mtihani na hivyo kuchanganyikiwa na hata kuandika kwa haraka bila kurudia kusoma alichoandika na hivyo kufanywa makosa bila kunuia au kujua. Dhana hii inaweza kupigwa jeki na utambuzi wa data ya utafiti huu inayoonyesha kuwa asilimia 80 ya makosa ya kuacha herufi moja katika maneno yalipatikana katika insha za wanafunzi wa shule za msingi huku asilimia ishirini tu ikipatikana katika insha za wanafunzi wa shule za upili. Hali hii yaweza kutokana na masiala tuliyoyataja kimbele maana wanafunzi wa shule ya msingi huwa bado ni wadogo, hawajajua kuandika vizuri, pia wana uoga wa mitihani wakilinganishwa na wale wa shule za upili. Utafiti wa Shirika moja Lisilokuwa la Kiserikali ulionyesha kuwa wanafunzi wengi humaliza masomo ya shule ya msingi kabla ya kujua kusoma na kuandika (Ripoti ya Uwezo 2010).

### 4.5 Athari Chanya za Kikisa kwa Kiswahili

Wafula na wenzake (2016) wanaonyesha kuwa lahaja za Kiluhya zina mfumo wa kisintaksia unaoweka pamoja mtenda au kitenda na kitenzi. Hali hii ni sawa na ilivyo kwa Kiswahili Sanifu. Hivyo basi kwa wanafunzi wanaosoma Kiswahili ambao ni wazungumzaji wa Kikisa kama lugha ya kwanza wanaingiana na mfumo wa Kiswahili kwa haraka. Kwa mfano katika kusema:

**Nzi-**tsa-nga (**ni-**na-end-a), neno moja linaunda sentensi kamili iliyo na mtenda/kitenda na kitenzi. Katika mfano huu tunaona uambishaji ukijitokeza. Viambishi vimebainishwa vikiwemo vya awali kama vile wakati au njeo, mzizi na hata viambishi tamati kama vile vya mnyambuliko.

**4.6 Asilimia ya Makosa**

Katika jedwali lifuatalo, tumeorodhesha aina za makosa yaliyobainika kutokana na utafiti wetu.

| **aina ya makosa** | **idadi** | **asilimia** |
|---|---|---|
| ubadilishaji fonimu | 65 | 36.3 |
| uongezaji fonimu | 14 | 7 |
| uongezaji mofimu | 10 | 5 |
| makosa ya ngeli | 9 | 5 |
| umakinifu zaidi | 24 | 13.4 |
| makosa ya kawaida | 16 | 8.9 |
| udondoshaji fonimu | 5 | 2.8 |
| makosa ya idadi | 3 | 1.7 |
| makosa ya kileksia | 1 | 0.6 |
| uhawilishaji wa mfumo | 11 | 6.1 |
| ujumlishaji mno | 1 | 0.6 |
| yasio na athari za Kikisa | 20 | 11.2 |
| jumla ya makosa | 179 | 85.2 |

Makosa ya ubadilishaji fonimu yanatokea kuwa mengi, asilimia 36.3, yakilinganishwa na makosa mengine. Makosa haya yanaweza kuelezwa kwa jinsi lugha hizi mbili zilivyo na mifumo yenye ukaribu sana. Kwa sababu ya kuwa na mifumo inayokaribiana, lugha hizi zinawiana vyema kwa mifumo na hivyo makosa machache ya kimfumo kutokea (asilimia 6.1) yakilinganishwa na

asilimia 36.3 ya makosa ya ubadilishaji wa fonimu ambayo yanatokea katika maneno wala si zaidi katika sentensi. Makosa ya kisintaksia katika Kiswahili vile vile yanatokea kwa uchache (asilimia 8.9) ikilinganishwa na makosa ya kubadilishwa sauti au fonimu katika neno.

Kwa kulinganisha makosa yanayotokea katika neno na yanayotokea katika sentensi tunapata asilimia zifuatazo:

| **makosa** | **idadi** | **asilimia** |
|---|---|---|
| makosa katika neno | 138 | 77.1 |
| makosa katika sentensi | 412 | 2.9 |

Kutokana na data ya utafiti, makosa yaliyo katika neno au yanayohusu fonimu katika maneno ni kama vile ya kubadilisha fonimu, kuongeza na hata kudondosha fonimu huku makosa katika sentensi yakihusisha ujumlishaji, makosa ya ngeli, makosa ya kawaida na makosa ya umoja na wingi.

Jumla ya makosa 179 yalipatikana katika insha 210 zilizosomwa na makosa yaliyomo kubainishwa. Insha zote (asilimia 100) zilipatikana na makosa ama yanayotokana na athari au yasiyo na msingi wa athari zake katika Kikisa. Makosa mengine yaliweza kujirudia kupitia kufanywa na wanafunzi zaidi ya wawili hadi sita. Hili linaonyesha kuwa bado kuna makosa katika insha za wanafunzi na kubainisha makosa hayo, kuyachanganua ili kutoa sababu za kutokea kwake kutasaidia kubuni mikakati ya ufunzaji na ujifunzaji wa lugha ya pili hasa Kiswahili Sanifu kwa mzungumzaji asilia wa Kikisa.

Makosa yanayotokana na athari za Kikisa kwa Kiswahili Sanifu ni mengi yakilinganishwa na yale yaliyo na msingi wake kwa lugha na vijilugha vingine. Asilimia zake, kama data ya utafiti huu ilivyodokeza, ni kama ifuatavyo:

| **makosa** | **idadi** | **asilimia** |
|---|---|---|
| makosa yenye athari za Kikisa | 159 | 88.8 |
| makosa yasiyo na msingi wa Kikisa | 20 | 11.2 |

Asilimia kubwa za athari zinazohusiana na Kikisa zinaonyesha jinsi Kikisa kinavyoathiri Kiswahili hasa kwa wanafunzi ambao hii ndio lugha yao ya kwanza. Wingi wa makosa haya unadhihirisha umuhimu wa kuwepo kwa mikakati ya kuwasaidia wanafunzi wa Kiswahili kwa kutilia maanani ushawishi na uwezo wa lugha ya kwanza.

Takriban walimu kumi na nne walihojiwa. Walimu walifanya makosa yanayotokana na athari kwa kiasi kilichotofautiana kama ifuatavyo:

| **kikundi** | **kadirio la makosa** | **kodi** | **asilimia** |
|---|---|---|---|
| 0 | hakuna makosa | 42 | 8.6 |
| 1-2 | makosa machache zaidi | 64 | 2.8 |
| 3-4 | makosa machache | 42 | 8.6 |
| 5-6 | makosa wastani | 0 | 0 |
| 7-8 | makosa mengi | 0 | 0 |
| zaidi ya 9 | makosa mengi zaidi | 0 | 0 |

Asilimia 42.8 ya walimu wazungumzaji asilia wa Kikisa walizungumza Kiswahili kwa kufanya makosa yaliyotokana na athari za Kikisa kama lugha yao ya kwanza. Ukubwa wa idadi hii unadhihirisha kuwa, licha ya kuwepo kwa walimu asilimia 28.6 ambao hawadhihirishi athari zozote za Kikisa kwa Kiswahili, kunao walimu asilimia 71.4 ambao wanaonyesha makosa yanayotokana na athari za lugha ya Kikisa. Hii ni idadi kubwa na ina athari kubwa kwa ujifunzaji wa wanafunzi wanaofunzwa na walimu hawa. Hata hivyo ni muhimu kutaja kuwa, makosa mengi yalifanywa na walimu wa shule za msingi kama inavyodhihirika katika takwimu hizi:

| **kategoria** | **idadi** | **m.machache zaidi** | **m.machache** | **asilimia** |
|---|---|---|---|---|
| walimu wa shule za msingi | 7 | 2 | 4 | 28.6, 57.1 |
| walimu wa shule za upili | 7 | 4 | 0 | 57.1, 0 |

## 4.7 Athari za Mtagusano wa Kikisa na Kiswahili Sanifu

Weinreich (1953) anaeleza athari zinazotokana na mtagusano kati ya mifumo miwili ya kifonolojia na ambapo anatofautisha kati ya aina nne za kimsingi. Aina hizi nne na ambazo zilijibainisha katika utafiti huu ni kama ifuatavyo:-

### *4.7.1 Kutofautisha kwa Hali ya Chini kwa Fonimu*

Hali hii hutokea wakati fonimu mbili za mifumo ya lugha ya pili ambazo fonimu lingani katika mfumo wa lugha ya kwanza hazijatofautishwa huchanganywa. Mifano ifuatayo inaonyesha jinsi hali hii ilivyosababisha athari za Kikisa kwa Kiswahili kama data yetu ilivyodhihirisha:-

1. Alipofika mtoni alianza *kufua* samaki.
2. Ukitaka *mβaka* uketi chini.
3. Tusivae nguo ambazo zina*tupana.*

Fonimu /p/ na /b/ katika Kiswahili Sanifu zimetofautishwa huku katika Kikisa fonimu hizi zikiwa hazijatofautishwa ila fonimu /b/ haijitokezi wazi katika Kikisa. Fonimu nyingine ni kama /f/ na /v/ na /ʧ/ na /ɟ/.

Isitoshe, Kiswahili kina fonimu /p/ iliyo na alofoni zake /p/ na /$p^h$/. Hata hivyo katika Kikisa fonimu hii ni moja tu /p/ na haina alofoni nyingine. Hali hii husababisha wazungumzaji walio wazungumzaji asilia wa Kikisa kukosa kutofautisha /p/ na /$p^h$/ wanapotamka maneno ya Kiswahili Sanifu. Kwa mfano katika neno /paka/ na /$mp^haka$/.

### *4.7.2 Kutofautisha kwa Hali ya Juu kwa Fonimu*

Kutofautisha kwa hali ya juu kwa fonimu huhusisha ulazimishaji wa tofauti za kifonolojia kutoka kwa mfumo wa lugha ya kwanza kwa fonimu za mfumo wa lugha ya pili, pale ambapo hazihitajiki. Data ya utafiti huu ilibainisha kuwa, kuna fonimu zinazoongezwa kwa maneno ili kukidhi mfumo asilia wa Kikisa katika Kiswahili Sanifu. Mifano ifuatayo inaafiki hili:

Data iliyopatikana nyanjani ilidhihirisha maneno kama vile:

| | | |
|---|---|---|
| **(71)** | **makosa** | **sahihi** |
| | [mupira] | [mpira] |

[muʧɛsɔ]    [mchezɔ]

[mukɔnɔ]    [mkɔnɔ]

Aidha, data ya utafiti ilizibaini sentensi kama vile:

**(72)** 1. Kuwanyanyasa w*anainchi*.

2. *Hamujambo* wanafunzi wenzangu.

3. Mia moja na *hamusini*.

### *4.7.3 Ufafanuzi Tena*

Hali hii hutokea wakati mwanauwililugha anapotofautisha fonimu za mfumo wa lugha ya pili kwa nduni ambazo katika mfumo huo ni za pamoja na hazihitajiki, lakini ambazo ni muhimu katika mfumo wa lugha ya kwanza. Tofauti za makundi yanayounda ngeli moja na nyingine katika Kikisa na Kiswahili Sanifu zinaonyesha hali hii. Katika Kiswahili kuna ngeli moja tu ya viumbe vyenye uhai yaani A/WA huku katika Kikisa ngeli zikiwa tofauti zikiwemo ngeli za wanyama na binadamu. Tofauti hizi ndizo zinazopelekea uwepo wa makosa kama vile:

**(73)** 1. Kuku yangu *imekufa*.

2. Ng'ombe *hiyo ilitupa* maziwa.

3. Paka *lake liliuliwa*.

### *4.7.4 Ubadilishaji Fonimu*

Mchakato huu huhusisha fonimu ambazo zinafanana kabisa katika lugha zote mbili lakini ambazo kutamkwa kwazo kwa kawaida kunatofautiana. Kutokana na data ya utafiti, hali hii imejitokeza kwa kiasi kikubwa katika Kikisa haswa kupitia matamshi. Fonimu /b/ ni mfano mzuri wa sauti ambayo inaonekana katika lugha zote mbili lakini matamshi yake ni tofauti kabisa katika Kikisa na Kiswahili. Utofauti huu katika matamshi unasababisha makosa katika matamshi ya maneno ya Kiswahili kutokana na athari za Kikisa kwa mzungumzaji wa Kiswahili Sanifu. Kwa mfano:

**(74)** Nilii*β*a hapana

Wali*β*adilisha mienendo *zao*

Licha ya fonimu hizi kuonekana kama /b/ hutamkwa kimakosa kama fonimu /β/. Hata kwa zile sentensi zilizobadilishwa fonimu kutoka /p/ kwenda /b/ na mzungumzaji mwenye athari, bado hali kama hii hutokea kwa mfano:

**(75)** *Alitubatia sawati* kwa maana ya 'alitupatia zawadi'.

### 4.8 Hitimisho

Sura hii imejadili makosa yanayojitokeza wazungumzaji wa Kikisa wanapowasiliana kwa kutumia Kiswahili Sanifu. Tumeonyesha asilimia za makosa na sababu zinazoweza kuwa zinapelekea makosa haya kutendeka. Hivyo basi, makosa yameweza kuchanganuliwa na athari zake kimaana kuwekwa wazi.

Sura hii ilinuia kuafiki lengo mojawapo muhimu la utafiti huu ambalo ni kutathmini hali kuwa maneno na matamshi ya mzungumzaji wa Kiswahili aliye mzungumzaji asilia wa Kikisa yanaweza kueleweka, kubadili maana iliyonuiwa au kutoeleweka kabisa. Kupitia kuyaweka maneno na kauli zenye makosa kama hizi katika mizani ya uelewekaji tunaweza kuonyesha athari za kisemantiki zinazotekelezwa na athari za Kikisa kwa Kiswahili Sanifu.

Idadi kubwa ya makosa yafanywayo na wazungumzaji asilia wa Kikisa inasababisha athari hasi katika mawasiliano ambapo maana inaonekana kubadilika. Mabadiliko katika fonimu moja katika neno yanatoa mabadiliko ya maana ya neno husika. Neno hilo linapokuwa na maana tofauti katika Kiswahili Sanifu linazua maana tofauti kabisa na iliyodhamiriwa na msemaji wa Kiswahili aliye mzungumzaji asilia wa Kikisa na hivyo kupelekea msikilizaji kupata ujumbe tofauti. Hali hii hukwamisha mawasiliano wakati neno linalojitokeza baada ya fonimu kubadilishwa huwa halina maana yoyote katika Kiswahili kwani linamuacha msikilizaji bila kujua aliloambiwa au aliloelezwa.

Kupitia uchanganuzi huu wa makosa, wanafunzi na walimu wanaweza kuona fonimu au sauti zinazowasumbua sana wanafunzi wa Kiswahili walio wazungumzaji asilia wa Kikisa kama lugha yao ya kwanza na hivyo kuwasaidia katika ujifunzaji wao wa Kiswahili Sanifu. Kazi hii imeonyesha athari chanya zilizopo kati ya Kikisa na Kiswahili. Licha ya kuwa Kikisa kina athari nyingi hasi kwa Kiswahili, kupitia kuwa wanafunzi wa Kikisa kama lugha ya kwanza, wanafunzi wanapata urahisi wa kuelewa mengi kuhusiana na muundo wa Kiswahili Sanifu. Hali hii yaweza kufafanuliwa na asilimia tano tu iliyojitokeza ya makosa ya ngeli zisizofaa katika Kiswahili.

## Sura ya 5
## Muhtasari, Mahitimisho na Mapendekezo

### 5.1 Utangulizi

Sura hii ndiyo ya mwisho katika utafiti huu. Sura hii inatoa kwa kifupi hitimisho kuhusu utafiti huu na yaliyozungumzwa na kujadiliwa katika utafiti huu. Sura hii inatoa pia mapendekezo ya tafiti nyingine zinazoweza kufanywa kwa mada hii, kuhusiana na mada hii, zinazokaribiana na mada hii na hata mada zingine zilizoibuka wakati wa utafiti huu. Hili limefanywa kwani utafiti huu haujaangazia kila kitu kinachoweza kutafitiwa kuhusu uathirianaji au athari za lugha ya kwanza kwa lugha ya pili bali sehemu tu. Utafiti huu umechunguza na kujadili athari za Kikisa kwa Kiswahili Sanifu pekee bila kuhusisha lugha nyinginezo nchini Kenya na nje ya mipaka ya Kenya. Hitimisho pia limetolewa ili kutoa kauli za mwisho kuhusu malengo ya utafiti na kiwango cha uafikiaji wake.

### 5.2 Muhtasari na Mahitimisho

Athari za Kikisa zinajitokeza katika mazungumzo na maandishi ya wazungumzaji na waandishi wa Kiswahili walio wazungumzaji asilia wa Kikisa kama lugha yao ya kwanza. Jambo hili linaathiri mawasiliano kama ilivyojitokeza katika kazi hii. Athari za Kikisa pia zinajitokeza miongoni mwa wanafunzi kupitia mazungumzo, mijadala yao shuleni na katika majibu yao katika mitihani haswa katika insha zao.

Athari hizi zilijitokeza kwa wanafunzi wa lugha ya Kiswahili na kwa walimu wao. Athari za Kikisa zinapojitokeza kwa wanafunzi zinawafanya kujihisi wasio na thamani, kuanguka mitihani ya lugha ya Kiswahili Sanifu na kuogopa kuzungumza Kiswahili hadharani kwa kuhofia kuchekwa na wenzao. Athari hizi zinapotokea kwa walimu husababisha kutokueleweka kwa kinachofundishwa, wanafunzi kuchukua muda mrefu kumwelewa mwalimu wao na wanafunzi kuelewa mambo tofauti na anavyomaanisha mwalimu. Hali kama hii husababisha kuanguka kwa mitihani ya Kiswahili kwa wanafunzi hawa wazungumzaji asilia wa Kikisa. Hili halitokei kwa sababu walimu hawajui kufundisha au wanafunzi wana matatizo ya kuelewa bali kwa sababu ya matatizo yanayotokana na athari za lugha ya kwanza. Tatizo la ukosefu wa maelewano kati ya mzungumzaji na msikilizaji ndilo shina la utafiti huu. Athari za lugha ya kwanza ambayo ni Kikisa katika muktadha huu zinapojitokeza katika Kiswahili zinaathiri maana. Maana ni mhimili mkuu wa

mawasiliano. Kwa sababu hii, palikuwa na umuhimu mkubwa wa utafiti kufanyiwa athari hizi na uhusiano wake na uelewekaji wa maana iliyobebwa na jumbe au kauli za mzungumzaji.

Wafula (2016) anasema kuwa Kiluhya kina lahaja nyingi lakini zina sintakisia inayofanana kutokana na kufanana kwa fahiwa za kileksia. Lahaja za Kiluhya hutumia maneno yale yale lakini tofauti ni kwa sifa nyingine kama vile matamshi, shadda na urefu wa vokali. Kwa kufanana huku basi matokeo ya utafiti huu yatasaidia sio tu wanafunzi na watu ambao Kikisa ni lugha yao ya kwanza pekee bali jamii nzima ya Waluhya.

Athari za Kikisa kwa Kiswahili Sanifu zimeweza kubainishwa katika kazi hii na kuchanganuliwa ili kutoa sababu na athari za makosa yanayofanyika kimaana kutokana na maana aliyokusudia mzungumzaji na aliyopokea msikilizaji. Sababu hizi zimejitokeza kama zinazoweza kuzua utata kimaana na hata kukatisha mawasiliano. Hata hivyo, kazi hii imeweza kubaini kuwa, kwa kutambua makosa haya na sababu zinazopelekea makosa hayo husika kutendeka, pana uwezekano wa kubuni mikakati ya kuyasuluhisha kwa kuyakabili ili kuyapunguza kama sio kuyatatua.

Utafiti huu una umuhimu mkubwa kama tulivyojadili. Walimu, wanafunzi, wataalamu wa nyanja mbalimbali wanaotumia Kiswahili katika mawasiliano yao, na waundaji wa mitaala nchini Kenya watafaidi sana kutokana na utafiti huu kwani dhima kuu ya kuzungumza ni kuwasiliana ambako hutokea tu panapokuwa na maelewano ya kimaana baina ya mzungumzaji na msikilizaji. Dhima hii hufikiwa vyema wakati wawili hawa wanazungumza lugha husika katika mawasiliano hayo kwa usawa. Lakini, panapotokea athari kama vile za Kikisa basi utafiti kama huu utakuwa wa muhimu kwa msikilizaji katika muktadha huo.

Ni muhimu kutaja kuwa nchini Kenya lugha yenye athari za Kikisa inatumika katika mazungumzo ila katika miktadha isiyokuwa rasmi. Lugha iliyo na athari hizi za lugha ya kwanza inatumiwa katika vyombo vya habari kwa mfano wakati wa matangazo ya mauzo. Kuchangamkiwa kwa athari za lugha za kwanza katika Kiswahili kinachozungumzwa na Wakenya kunaonyesha uwepo wa uelewa wa athari anuwai zinazoletwa na lugha hizo za kwanza na wazungumzaji wa lugha mbalimbali tofauti za kwanza. Hata hivyo, hili halijawafikia wasomi katika Kiswahili Sanifu kama taaluma na wazungumzaji wa Kiswahili kama lugha ya kwanza ikikumbukwa kuwa nchini Kenya Kiswahili Sanifu kinafunzwa kama somo la lazima katika shule za msingi na shule za upili lakini si lugha ambayo sheria za matumizi yake zinatiliwa maanani na Wakenya kwani wanaonekana

kuwa makini katika Kingereza huku ikiwa si hoja ‘kuvunja’ kanuni za Kiswahili. Utafiti huu basi unawasaidia wanataaluma na wasomi wa Kiswahili wanapomsikiliza mzungumzaji aliye na athari za Kikisa kama lugha yake ya kwanza kuwa na matarajio fulani ya uvunjwaji wa kanuni na hivyo kusaili panapokuwa na utata bila kuchukulia maneno na uelewa mmoja tu anaoujua. Hili linasaidia kuelewana na kuepusha mawasiliano chapwa.

### 5.3 Mapendekezo

Kazi hii imejikita katika kuangalia uhawilishaji wa fonimu unaosababisha maana kutoeleweka, kueleweka vibaya au kueleweka bila tatizo licha ya tofauti za fonimu zinazofaa. Pendekezo letu ni kuwa utafiti unahitajika katika sehemu ya fonolojia ili kutambulisha fonimu zinavyobadilika kifonolojia kutoka kwa fonolojia ya Kikisa hadi fonolojia ya Kiswahili Sanifu. Wazo hili linatokana na ukweli kuwa hata tunaposema kuwa sauti moja hubadilishwa ili kuwa sauti inayopatikana katika lugha ya kwanza sauti hiyo haitamkwi moja kwa moja jinsi inavyoonekana kimaandishi kama tulivyoandika katika kazi hii.

Lugha ya Kiswahili haiathiriwi na lugha ya Kikisa pekee bali lahaja zote za Kiluhya na lugha nyingine nchini Kenya kama vile Kikuyu, Kikamba na Kikisii na Kijaluo. Utafiti unahitajika kwa lahaja nyingine za Kiluhya na hata lugha nyingine zote zinazotangamana na Kiswahili Sanifu kutokana na ukruba wake nazo ili kutambua ni athari gani zinazoingizwa katika Kiswahili Sanifu. Hili litasaidia kutambua ni maneno gani ambayo si msamiati wa Kiswahili Sanifu bali yanatumika katika Kiswahili cha mazungumzo kutokana na makubaliano ya Kijamii ambapo maana ya neno husika imehawilishwa hadi katika Kiswahili na kueleweka na watu wa jamii tofauti. Pia kwa kujua athari za matamshi ya lugha mbalimbali kwa Kiswahili Sanifu itakuwa rahisi kwa mawasiliano kuendelezwa bila kutatizika. Wanafunzi wataweza kumuelewa mwalimu aliye na athari kwa urahisi na hivyo kuboresha uelewa wa masomo. Watu na wafanyikazi mbalimbali katika miji mikuu iliyo na watu kutoka jamii na makabila tofauti wataweza kuelewana kwa urahisi kutokana na kujua sauti zinazobadilika kwa kubebwa kwa urahisi na watu kutoka jamiilugha mbalimbali.

Githiora (2008) anazungumzia lugha ya taifa kama kitambulisho cha taifa. Githiora anafafanua kuwa, licha ya Kiswahili kuwa lugha ya taifa kwa mataifa kama Kenya, Uganda na Tanzania na hutumika katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati, kila taifa lina kile kinachoweza kuitwa Kiswahili cha nchi husika. Kwa mfano, upo uwezekano wa kuonyesha sifa za Kiswahili cha Kenya, cha Uganda na cha Tanzania. Sifa zilizopo zinaweza kutambulisha Kiswahili husika kama

cha nchi fulani na kukitofautisha na Viswahili vingine. Githiora anasema kuwa Kiswahili cha Tanzania ni Kiswahili kimoja kinachozungumzwa na Watanzania wote huku Kiswahili nchini Kenya kikiwa na sifa ya kuwa na athari za lugha iliyo na athari za pale wazungumzaji wanapotoka. Hata wanaosemekana kuwa Waswahili wa Pwani nchini Kenya nao pia wanazungumza Kimvita, Kiamu, Kijomvu, Kitikuu, na lahaja nyingine ambazo ni tofauti na Kiswahili Sanifu ambacho kimekitwa msingi wake kwa Kiunguja ambayo ni lahaja ya nchini Tanzania. Hali hii inasababisha uhawilishaji wa mifumo ya lahaja za Kiswahili pia katika Kiswahili Sanifu (Gaithuma 2016). Hili linapelekea matokeo mabaya katika mitihani ya Kiswahili ya kitaifa kwa wanafunzi wa eneo la Pwani (Githiora 2008, Mazrui & Mazrui 1999). Hali hii inaonyesha kuwa upo umuhimu wa kuweka pamoja sifa za Kiswahili cha Kenya katika utafiti ili kupata sura kamili inayoweza kueleza utambuzi na ubainshaji wa Kiswahili cha Kenya kama lugha ya kitaifa.

Utafiti unahitajika kufafanua ni vipi watu wa mijini wanavyoweza kuelewana katika mazingira yaliyokithiri uhawilishaji fonimu za lugha tofauti za kwanza katika Kiswahili kinachotumika.

Tunapendekeza kuwa ushawishi wa vijana kuhusu ubora wa Kiswahili wanachotumia na athari zake unahitaji kufanyiwa utafiti. Hili linatokana na makosa mengi yaliyopatikana ambayo hayatokani na athari za Kikisa kwa Kiswahili Sanifu ilhali hawa ni wanafunzi ambao lugha yao ya kwanza ni Kikisa. Vijana wengi wanaonekana kukwepa kutumia Kiswahili Sanifu katika mazungumzo yao ya kawaida na hivyo kusababisha athari tofauti kabisa katika lugha mbalimbali wanazojifunza mbali na lugha yao ya kwanza. Kwa vijana kama hawa, athari za kimsimbo au vijilugha ibuka zina athari kubwa kwa matamshi na maandishi yao.

Utafiti huu umebaini kuwa wanajamii wanaowazunguka wanafunzi wana athari kubwa kwa jinsi wanavyoelewa na kutumia Kiswahili. Wazazi, marafiki na baadhi ya walimu wengine hawatumii Kiswahili Sanifu huku wengine wakiwa na athari za Kikisa katika matumizi yao ya Kiswahili. Hali hii inarithishwa kwa wanafunzi kwani watu hawa ndio vielelezo vinavyofuatwa na wanafunzi hawa. Hili linasababisha kujirudia kwa athari zile zile. Mwalimu anapofunza kwa athari wanafunzi huzungumza vile vile wakidhani kuwa ndiyo njia mwafaka ya kuyatamka maneno ya Kiswahili. Hili linazua mjadala ambao waweza kuwa pia pendekezo jingine la utafiti kuhusu ikiwa mwalimu wa Kiswahili Sanifu mwenye athari anafaa kuruhusiwa kuwafunza wanafunzi na ikiwa akiruhusiwa kuwafunza wanafunzi au la kutakuwa na uelewa kamili bila matatizo wa dhana anazowasilisha. Uhusishaji wa athari za uhawilishaji na matokeo ya wanafunzi katika mitihani.

## 5.4 Marejeleo


Abdulaziz, M. & Osinde, K. (2009). *Sheng and Engsh: Development of Mixed Codes among the Urban Youth in Kenya.* International Journal of the Sociology of Language, 125(1), pp. 43-64.

Amidu, A. (2007). *Semantic Assignment Rules in Bantu Classes.* Koln: Rudiger Koppe Verlag

Angogo, K. (1983). *Unity in Diversity – A Linguistic Survey of the Abaluyia of Western Kenya*. AFRO-PUB: The University of Virginia.

Arabski, J & Adam, W. (2011). *Individual Learner Differences in SLA.* UK: Techset composition Limited

Brown, (1987). *Principles of Language learning and teaching.* Prentice Hall: Regents.

Chepkwony, J. G. (1993). *Makosa Yanayofanywa na Baadhi ya Wanandi Katika Matumizi ya Kiswahili*. Tasnifu ya Uzamili (haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi.

Chimerah, R. (1998). *Kiswahili: Past, Present and Future Horizons*. Nairobi: Nairobi University Press.

Chiraghdin, S.& Mnyampala, M. (1977). *Historia ya Kiswahili*. Nairobi: Oxford University Press.

Cook, V. (1993). *Linguistics and Second Language Acquisition.* London: Macmillan Press Ltd.

Corder, S. P. (1969). *The Significance of Learners Errors: Error Analysis: Prospective in Second language Acquisition*. Essex: Longman.

_________ (1986). *Error Analysis and Interlanguage*. London: OUP

David, C. (1997). *A Dictionary of Linguistics and Phonetics*. 4th Ed. Blackwell.

Ellis, R. (1986). *Error Analysis and Interlanguage*. London: OUP.

_______. (1989). *Understanding Second Language Acquisition.* Oxford: Oxford University Press.

Dechert, W. & Raupach, M. (1989). *Transfer in Language Production.* Norwood: Ablex Publishing Corporation.

Fasold, R. (1984). *The Sociolinguitics of the Society.* NewYork: Blackwell Publishers

Gaithuma, W. V. (2016). *Athari za Kifonolojia za Lahaja ya Kiamu na Kitikuu katika Kiswahili Sanifu.* Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Gass, S. M. & Selinker, L. (2008). *Second Language Acquisition*. New York: Routledge.

Gass, M. et al (2013). *Second Language Acquisition: an introductory course.* NewYork: Routledge

Gergely, T. (2007). *Linguistic Interference and First Language Attrition*. NewYork: Peter Lang Publishing Inc.

Iribemwangi, P. I. & Mukhwana, A. (2011). *Isimujamii.* Nairobi: Focus Publishers Ltd.

Jacobs, H. (1994). *Using a Second Language: Language Introductory Readings.* NewYork: St. Martin's Press.

Kenya National Bureau of Statistics (2009). *Population & Housing Census Results*. Ministry for Planning and National Development.

King'ei, K. & Musau, P. (2000). *Utata wa Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Didaxis.

Khachula, A.N. (2013). *Semantic Shift in Lumarama: A Lexical Pragmatics Approach*. Tasnifu ya Uzamili (haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Nairobi.

Labov, W. (1991). *Sociolinguistic Patterns*.Philadelphia: University of Pennysyvania Press.

Lado, R. (1957). *Linguistics across Cultures: Applied Linguistics and Language Teachers.* Ann Arbor: University of Michigan.

Langacker, R. (1995). *Language and its Structure: Some Fundamental Linguistic Concepts*, Cambridge: Harvard Brace.

Lodhi, A. Y. (2002). *Verbal extensions in Bantu: the case of Swahili and Nyamwezi*. Africa & Asia 2:4-26.

Massamba, D.P.B. (1990). *The Development and Modernization of Kiswahili Language in Tanzania* katika *Language Adaptation.* Cambridge: Cambridge University Press.

Marlo, M. R. (2002). *Reduplication in Lusaamia*. Indiana University Working Papers in Linguistics Online 2.

_______. (2006). *CV- root expansion in three Luyia languages*. In N. Kula & R. Letsholo (eds), African Linguistics in the New Millennium, Linguistic Analysis, 32(3-4):293-326.

______. (2007). *The verbal Tonology of Lumarachi and Lunyala-West: Two Dialects of Luluyia* (Bantu, J.30, Kenya). University of Michigan Doctoral dissertation.

Mbaabu, I. (1985). *Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Kenya Pub. & Book Marketing Co.

_________ (1991). *Language Policy in East Africa.* Educational Research and Publication. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

________ (1995). *Usahihishaji Makosa katika Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Mbula, J. (2011). *Uchanganuzi wa Makosa ya Kifonolojia Yanayofanywa na Wazungumzaji wa Kikamba Wanapojifunza Kiswahili Sanifu*, Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Nairobi.

McMahon, A. (1994). *Understanding Language Change*. New York: Cambridge University Press.

Mgullu, R. S. (1999). *Mtalaa wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia, Mofolojia ya Kiswahili.* Nairobi: Longhorn publishers.

Mudhune, (2008). *Matatizo ya Kimofosintaksia Yalinayowakumba Wanafunzi Katika Jamii ya Waluo Katika Kujifunza Lugha ya Kiswahili*.Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Islamic, Uganda.

Mugenda, O. M., & Mugenda, A. G. (2003). *Research Methods. Quantitative and Qualitative Approaches*. Nairobi. Acts Press.

Myers-Scotton, C. M. (Ed.) (2000). *Language in Kenya.* New York: Oxford University Press.

Mweri, G. (2010). *Utangulizi wa Isimu.* Nairobi: Kenya Literature Bereau.

Nassenstein, N. & Hollington, A. (2016). *Youth Language Practices in Africa and Beyond.* DeGruyter: Mouton

Odlin, T. (1989). *Language Transfer: Cross linguistic influence in Language Learning*. Cambridge: Cambridge University Press.

Ondondo, E. (2015). *The Kisa Verb Phrase.* International Journal of English Language and Linguistics Research Vol.3, No.5, pp.9-24

Onyango, J.O. (1997). "*Uziada wa Kisarufi katika Kiswahili cha Wanafunzi wa Kinyala: Mtazamo wa Uchanganuzi Linganuzi*." Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Osogo, J. (1966). *A History of the Baluyia.* Nairobi: Oxford University Press.

Otiende, M. A. (2013). *Athari za Mofofonolojia ya Kibasuba katika Matumizi ya Kiswahili kama Lugha ya Pili*. Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Polome, E. C. (1967). *Swahili Language handbook.* Washington

Rapando, M. (2005). *Makosa ya Kimofo-sintaksia Yanayojitokeza Katika Kazi za Kiswahili Zilizoandikwa na Wanafunzi wa Shule za Upili Jijini Nairobi*. Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Rugemalira, J. M. (2007). *The structure of the Bantu noun phrase*. SOAS Working Papers in Linguistics 15.135-48.

Sascha, W. (1980). *Second Language Development: Trends and Issues.*Tubingen: Gunter Narr Verlag.

Selinker, L. (1992). *Rediscovering Interlanguage*. London: Longman.

Simpson, A. (2008). *Language and National Identity in Africa*. Oxford: Oxford University Press

Susan, G. M. & Selinker, L. (2001). 2nd Ed. *Second Language Acquisition: An Introductory Course*. Lawrence Erlbaum Associates Inc Publisher, 10 Industrial Avenue.

Traugott, E. and Dasher, R. (2002). *Regularity in Semantic Change*. Cambridge: Cambridge University Press.

TUKI (1990). *Kamusi ya Isimu na Lugha.* Dar es Salam: TUKI.

Ullmann, S. (1962). *An Introduction to the Science of Meaning.* Oxford: Blackwell.

Yule, G. (2006). *The Study of Language*. Cambridge: Cambridge University Press.

Wafula, R.M. & Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*, Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wardhaugh, R. (2006). *An Introduction to Sociolinguistics* – 5th ed.UK: Blackwell Publishing Ltd.

Weinreich, U. (1953). *Language in Contact: Findings and Problems.* New York: Linguistic circle of New York.

Welmers, W. E. (1973). *African Language Structures* Berkeley, California: University of California Press.

Were, G. (1967). *A history of the Abaluyia of Western Kenya*. Nairobi: East African Publishing House.

Wolff, H. E. (2016). *Language and Development in Africa*. Cambridge: Cambridge University Press.

# Viambatisho

**Kiambatisho 1**

**Data ya ziada**

| **makosa** | **sahihi (Kiswahili Sanifu)** |
|---|---|
| *wakanga* | waganga |
| *kari* | gari |
| *Thambi sako sote simesamehewa.* | Dhambi zako zote zimesamehewa. |
| *mesa* | meza |
| *mapatiliko* | mabadiliko |
| *kuruti* | kurudi |
| *tarasa* | darasa |
| *msasi* | mzazi |
| *papa* | baba |
| *tata* | dada |
| *mchomba* | mjomba |
| *ukali* | ugali |
| *uongosi* | uongozi |
| *charipu* | jaribu |
| *tulifathaika sana* | tulifadhaika sana |
| *Nilishangaswa na machumba marefu Nairobi*. | Nilishangazwa na majumba marefu Nairobi. |
| *pika* | piga |
| *chuta* | juta |
| *ipa* | iba |
| *impa* | imba |
| *pakuli* | bakuli |
| *machi* | maji |
| *tsemanini* | themanini |

| | |
|---|---|
| *tsalatsini* | thelathini |
| *kasi* | kazi |
| *chumatatu* | Jumatatu |
| *Viongozi wanavuja mali ya umma*. | Viongozi wanafuja mali ya umma. |
| *Maana ya nche ya methali.* | Maana ya nje ya methali. |
| *Tusivae nguo ambazo zinatupana* | Tusivae nguo ambazo zinatubana. |
| *Ukitaka chakula mbaka uketi chini.* | Ukitaka chakula mpaka uketi chini. |
| *Alipofika mtoni alianza kufua samaki.* | Alipofika mtoni alianza kuvua samaki. |
| *kufuta sigara kuvuta sigara* | kunywa bombe kunywa pombe |
| *changa la kitaifa* | janga la kitaifa |
| *machambasi* | majambazi |
| *kusawasishwa na wenzao* | kusawazishwa na wenzao |
| *koti ya jumba* | kodi ya chumba |
| *gari la isikochi* | gari la izikochi |
| *mazahibu* | masahibu |
| *sichakuwa* | sijakuwa |
| *walisipa mashimo yote* | waliziba mashimo yote |
| *tamatuni* | tamaduni |
| *Wanasimama kwa parapara* | wanasimama kwa barabara |
| *ni maachapu sana* | ni maajabu sana |
| *pila kuuliswa* | bila kuulizwa |
| *fumbi* | vumbi |
| *chua ikiwaka*. | jua likiwaka |
| *Tuliingia kwa paa.* | tuliingia kwa baa |
| *wanatuteza* | wanatutesa |
| *pato tumekaa* | bado tumekaa |
| *pahati yetu* | bahati yetu |

| | |
|---|---|
| *alitutanganya* | alitudanganya |
| *baada ya kuuswa* | baada ya kuuzwa |
| *uchofu* | uchovu |
| *kujinazua* | kujinasua |
| *Walichukuwa mifuko yetu*. | Walichukuwa mifugo wetu |
| *Asanteni kwa kukucha* | Asanteni kwa kuja |
| *Watakutana na wasasi baataye* | Watakutana na wazazi baadaye |
| *vitu hiso* | vitu hivyo |
| *kisiaki* | kisiagi |
| *hapari* | habari |
| *sapapu* | sababu |
| *akapiga hoti* | akapiga hodi |
| *haki sa watoto* | haki za watoto |
| *Ameipuka na tabia mbaya* | Ameibuka na tabia mbaya |
| *Uchungu wa mwana aujuaye ni msasi*. | Uchungu wa mwana aujuaye ni mzazi. |
| *Basi letu lilisafiri kwa kazi sana* | Basi letu lilisafiri kwa kasi sana |
| *Aliomba kupewa uridhi* | Aliomba kupewa urithi |
| *Aliwalazimisha wazazi kumridhisha shamba* | Aliwalazimisha wazazi kumrithisha shamba |
| *Hakuamuka kwa haraka* | Hakuamka kwa haraka |
| *Tumechumuika hapa leo* | Tumejumuika hapa leo |
| *jinzi siku ilivyo* | Jinsi siku ilivyo |
| *Tumefuka mbuzi na kondoo* | Tumefuga mbuzi na kondoo |
| *tuwape nithamu* | Tuwape nidhamu |
| *Hatutaki kuhaibishwa* | Hatutaki kuaibishwa. |
| *Siku ya wasasi shuleni* | Siku ya wazazi shuleni |
| *Swala la ubakaji linaendelea* | Swala la upakaji linaendelea |
| *Mukutano* | mkutano |

| | |
|---|---|
| *Hamujambo wanafunzi wenzangu?* | Hamjambo wanafunzi wenzangu? |
| *mia moja na hamusini* | mia moja na hamsini |
| *alitushika mukono* | Alitushika mkono |
| *Michezo huchangamusha akili* | Michezo huchangamsha akili. |
| *Kuzungumuzia ufisadi* | Kuzungumzia ufisadi |
| *Najua mumesikia* | Najua mmesikia |
| *uzuni* | huzuni |
| *nawasii* | nawasihi |
| *naendanga* | huenda |
| *nipatieko* | nipatie |
| *muchamaa* | jamaa |
| *abebeko* | abebe |
| *Sijawahi kumuonako* | Sijawahi kumuona |
| *manyumba haya* | nyumba hizi |
| *makaratasi haya* | karatasi hizi |
| *Kuku yangu imekufa* | Kuku wangu amekufa |
| *Kikombe yangu imepasuka* | Kikombe changu kimepasuka |
| *Mkate yangu iko wapi?* | Mkate wangu uko wapi? |
| *Chakula yangu ni nzuri*. | Chakula changu ni kizuri. |
| *Ng'ombe hiyo ilitupa maziwa* | Ng'ombe huyo alitupa maziwa |
| *Ng'ombe za watu*. | Ng'ombe wa watu. |
| *Paka lake liliuliwa* | Paka wake aliuawa |
| Baada ya wazazi *kukufa*, alitoroka nyumbani. | (**kufa**) |
| Baba *akipigana na ujasiri*. | (**akipigana kwa ujasiri**) |
| Alitia *chumbi* kwenye mboga | (**chumvi**) |
| Nimewakosea heshima kwa *kukuja* hapa. | (**kuja**) |
| *Niko na* furaha | (**nina**) |

| | |
|---|---|
| *Tuko na* majirani | (**tuna**) |
| *Tuko na* kasuku nyumbani. | (**tuna**) |
| Gari *lilibingirika na ushindo* mkubwa | (**lilibingirika kwa ushindo**) |
| *Kijana aliuzunika sana* | Kijana alihuzunika sana |
| *Asubui* | asubuhi |
| *kuukumiwa* | kuhukumiwa |
| *Anachotaka kufanyia pesa hiyo.* | Anachotaka kufanyia pesa hizo. |
| *Wasiwasi ulinijaa.* | wasiwasi ilinijaa |
| *Sherehe ya kumuaga babangu zilifanyika.* | Sherehe ya kumuaga babangu ilifanyika |
| *mazishi ilipokamilika* | mazishi yalipokamilika |
| *Walibadilisha mienendo zao.* | Walibadilisha mienendo yao. |
| *Gari ilikuja kwa kasi.* | Gari lilikuja kwa kasi. |